

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Ishirini na Tano – Tarehe 10 Mei, 2019

(Bunge lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulla Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Tukae, Katibu.

NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI: Maswali.

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Maswali, Waheshimiwa Wabunge tutaanza na Ofisi ya Rais TAMISEMI. Mheshimiwa Joel Mwaka Makanyaga Mbunge wa Chilonwa, sasa aulize swalii lake.

Na. 200

Kukamilisha Ujenzi wa Zahanati ya Kijiji – Chilonwa

MHE. JOEL M. MAKANYAGA aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha ujenzi wa Zahanati ya Kijiji cha Chilonwa iliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi ambayo kwa sasa imefikia kwenye linta?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joel Mwaka Makanyaga, Mbunge wa Chilonwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Chilonwa ni miongoni mwa Kata 36 za Wilaya ya Chamwino, ina vijiji viwili vya Nzali na Mahama, Kata ina huduma za Zahanati moja iliyopo katika Kijiji cha Nzali. Wananchi wa kijiji cha Mahama walianzisha ujenzi wa Zahanati ya Kijiji ambayo kwa sasa jengo limefikia hatua ya Ilinta. Katika kuunga mkono juhudzi za wananchi, Halmashauri ya Chamwino katika mwaka wa fedha 2019/2020 kupitia mapato yake ya ndani imetenga shilingi milioni 30 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa zahanati hiyo katika Kijiji cha Mahama. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Joel Makanyaga, swali la nyongeza.

MHE. JOEL M. MAKANYAGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nashukuru kwa majibu mazuri sana ya Serikali ambayo ameyatoa hapa Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini kwa umuhimu wa eneo lile niombe tu Mheshimiwa Naibu Waziri tupate nafasi twende sote kwa pamoja tutembee katika kijiji kile tuone jiografia ya pale na umuhimu wake ili Serikali iweze kuona inaisaidia vipi Halmashauri ya Chamwino katika kukamilisha zahanati ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Namshukuru Mheshimiwa Mbunge wa Chamwino Makao Makuu ya Ikulu ya Nchi kwa kukubali na kutupongeza, lakini mimi nipo tayari sana wakati wowote mwezi huu wa Tano twende katika Jimbo lake tukatembee. Ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mary Pius Chatanda, swali la nyongeza.

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kijiji cha Kitifu kipo Kata ya Mgombezi Kimejenga zahanati na kimekamilisha, isipokuwa tu tunaomba mtusaidie majengo ya daktari pamoja na majengo mengine ambayo hayajakamilika. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana, je, mtakuwa tayari kutusaidia angalau tuweze kupata fedha kwa ajili ya jengo la mganga?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge mwanamke wa Jimbo ambaye anafanya kazi kubwa sana pale Korogwe. Naomba nimhakikishie kwamba mimi, Wizara na Serikali tupo tayari kuwasaidia Wabunge wanawake ili waendelee ku-*maintain* Majimbo yao. Tutafanya kazi hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Alex Gashaza, swali la nyongeza.

MHE. ALEX R. GASHAZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Wiki tatu zilizopita niuliza swali kuhusu Zahanati ya Kigarama ambayo wananchi wamejenga kwa nguvu zao, miaka miwili wamekamilisha *OPD*, lakini kuna upungufu wa choo na nyumba ya Mganga na haiwezi kufunguliwa kabla ya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Serikali itaweza kukamilisha majengo hayo yanayopungua ili Kituo hiki kiweze kutoa huduma kwa wananchi ambao wanahangaika muda mrefu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Jambo hili tunalifahamu na kama nilivyojibu tangu wiki iliopita ni kwamba tupo kwenye mchakato wa kupeleka fedha za kumalizia maboma ya Zahanati na Vituo vya Afya na naomba jambo hili tulichukue kwa uzito, tutalifanyia kazi, Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Hasna Sudi Katunda Mwilima, Mbunge wa Kigoma Kusini, sasa aulize swali lake. (*Makofi*)

Na. 201

Hitaji la Shule ya Kidato cha Tano na Sita – Mwambao wa Ziwa Tanganyika

MHE. HASNA S. MWILIMA aliuliza:-

Jiografia ya Halmashauri ya Uvinza ni mbaya na kusababisha wanafunzi wanaomaliza Kidato cha Nne kutoka mwambao wa Ziwa Tanganyika kusafiri zaidi ya kilometra 200 kufuata Shule za Kidato cha Tano na Sita zilizopo katika ukanda wa Reli:-

(a) Je, kwa nini Serikali isianzishe Shule za Kidato cha Tano na Sita kwenye Kata nane za Ukanda wa Ziwa Tanganyika ili kuwapunguzia usumbufu wanafunzi hao?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati na kuongeza miundombinu katika Shule za Kidato cha Tano na Sita Rugufu Wasichana na Wavulana ambazo miundombinu yake ni chakavu na haitoshelez?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba nijibu swalii la Mheshimiwa Hasna Sudi Katumba Mwilima, Mbunge wa Kigoma Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza inaundwa na Tarafa tatu za Nguruka, llagala na Buhingu. Shule za Sekondari za Kidato cha I – IV ziko 20 (18 za Serikali na 2 za binafsi) zote zikiwa na jumla ya wanafunzi 11,622. Shule za Kidato cha Tano na Sita zipo tatu ambazo ni Lugufu Wavulana, Lugufu Wasichana, zote za Tarafa ya Nguruka na Kalenge iliyopo Tarafa ya llagala.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uanzishaji wa Shule za Kidato cha Tano na Sita ni la kisera, Iakini Serikali inaendelea kuboresha na kupanua miundombinu katika Shule za Sekondari Buhingu katika Tarafa ya Buhingu na Sunuka katika Tarafa ya llagala ambazo zinatarajiwaa kupandishwa hadhi na kuanza kutoa elimu ya Kidato cha Tano na Sita ifikapo Julai, 2020.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Shule za Sekondari za Lugufu Wavulana na Wasichana ni mionganini mwa Shule za Sekondari zilizoanzishwa kwenye maeneo yaliyokuwa Makambi ya Wakimbizi Mkoani Kigoma. Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri imekuwa ikitumia mapato ya ndani ya Halmashauri na kukamilisha vyumba vitatu vya maabara za Sayansi.

Vile vile Serikali Kuu kuititia programu ya EP4Rimepeleka fedha za ukarabati wa matundu manane ya vyoo na shilingi milioni 150 kwa ajili ya ujenzi wa mabweni mawili mapya kuititia Mamlaka ya Elimu Tanzania.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hasna Mwilima, swalii la nyongeza.

MHE. HASNA S. MWILIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Naibu Waziri na ninaishukuru pia Serikali kwa hiyo fedha ambayo imetuletea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. Swalii la kwanza, ni kweli kwamba tunazo hizo *High School*/mbili kwa maana ya *Lugufu Boys* na *Lugufu Girls*. Shule hizi kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, zimeanzishwa kwenye majengo chakavu yaliyokuwa yakinumika na wakimbizi. Hali ya hizo shule ni mbaya sana na hata hiyo shilingi milioni 150 waliyoleta, yaani inakuwa haionekani imefanya nini kutokana na mazingira halisi tuliyonayo pale. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata umeme na maji kwenye hizi shule, hakuna. Sasa swalii langu kwa Naibu Waziri: Je, ni lini sasa Serikali itaweza kutatua changamoto ya miundombinu iliyoko *Lugufu Boys* na *Lugufu Girls* sambamba na kuwapelekea umeme na maji? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii langu la pili ni kweli kabisa kwamba Halmashauri inaangalia uwezekano wa kuanzisha Kidato cha Tano na cha Sita kwenye Sekondari zetu za Buhingu na Sekondari ya Sunuka. Kwenye majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ameonyesha kwamba Halmashauri inatumia pesa zake za ndani. Sisi wote ni mashahidi, hali ya kipato cha Halmashauri sasa hivi ni mbaya sana. Kwa hiyo, naiomba Wizara; swalii langu ni: Je, Wizara halioni sasa ni vyema ituletee fedha kwa ajili ya kuendeleza miundombinu kwenye Shule ya Sekondari ya Sunuka na Shule ya Sekondari ya Buhingu ili tuweze kuwa na Kidato cha Tano na cha Sita? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, hawa ni mionganoni mwa Wabunge jembe wanawake wa Majimbo ambao wanafanya kazi kubwa sana kuwatetea Watanzania wenzao na hasa katika

suala zima la elimu na unaona anazungumza habari ya wanawake ili na wao wafikie hatua kama yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza anataka kujua ni namna gari Serikali imejipanga kuboresha majengo ya shule hasa ambazo amezitaja ambazo ni chakavu. Ni utaratibu wa Serikali kuboresha majengo haya na bahati nzuri kwenye Bunge hili Tukufu ambalo linaendelea tumeishapitisha bajeti ya TAMISEMI na tuna fedha mle karibu shilingi bilioni 90 ambayo itakwenda kufanyakazi *EP4R*. Kwa hiyo, tutagawa fedha katika maeneo yale na ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge tutazingatia hili katika kupeleka fedha kwenye eneo hilo kwa shughuli ambayo ameitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, amezungumza habari ya Kidato cha Tano na Kidato cha Sita. Siyo kwamba Serikali imejitoa kushiriki. Tunachosema ni kwamba Halmashauri lazima ianze. Kuna mambo ya msingi kwa mfano ardhi, iwe na umiliki hatuna fedha ya kulipa fidia, lakini wachangie kupitia mapato yao ya ndani, nasi kama Wizara tunaongezea pale na kuboresha pamoja na kupeleka wataalam na maabara nyininge. Kwa hiyo, tutachangia jambo hili ila walianzishe. Kipaumbele ni kwamba kila Tarafa angalau iwe na *High School* moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kusema kwamba ni muhimu tungeomba kuhimiza, pamoja na kuanzisha Shule za Kidato cha Tano na cha Sita, ukweli ni kwamba hizi shule ni za Kitaifa, zikianzishwa maana yake utapeleka watoto kutoka nchi nzima. Kwa hiyo, unaweza kubadilisha miundombinu mingine ili watoto wa eneo lile kama ni Uvinza, utaenda kuwasaidia Nguruka. Ni muhimu kuhimiza elimu ya msingi, sekondari, halafu wengine tunaenda huko mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe kuuliza maswali mafupi ili watu wengi wapate fursa. Ukiuliza kwa kirefu maana yake nitakukata hapa mbele. Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso.

MHE. SELEMANI M. KAKOSO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika wamejitalidi sana kwa kushirkiana na wananchi, wamejenga shule za sekondari zipatavyo sita, lakini kwa bahati mbaya sana bado baadhi ya majengo hayajapata kuezekwa. Kwa hiyo, tulikuwa tunauliza, Serikali ina mchango gani wa kuwasaidia hao wananchi ambao wametumia nguvu kubwa ili waweze kukamilisha hayo majengo? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mwezi wa Pili mwanzoni tumepeleka fedha zaidi ya shilingi bilioni 29.9 kumalizia majengo kwa maana ya maboma katika Shule za Sekondari. Ninaamini Halmashauri karibu zote, kuna baadhi ya maeneo tu hatukupeleka, lakini maeneo mengi tumepeleka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la misingi, ni kwamba vile vile mwaka huu wa fedha tuna miradi mingi na fedha ambazo zipo kwenda kumalizia maboma. Sasa kama kuna changamoto katika eneo hili kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, tutazingatia maombi yake ili tuweze kumalizia majengo haya na watoto wetu waweze kukaa sehemu salama na waweze kupata elimu kama ambavyo ndiyo makusudio na matarajio ya Serikali ya Awamu ya Tano. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka, swali la nyongeza.

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Hali ya Jimbo la Same Mashariki na Shule za *High School* haiko tofauti sana na ile ya Kigoma Kusini. Serikali ilishatupa hela ya kujenga bweni la wasichana ili Kidato cha Tano kianze na bweni hilo la kuchukua wanafunzi 80 limeisha. Sasa hivi wananchi wameshatengeneza matofali na wanaanza ujenzi wa

kupandisha madarasa mawili ili *Form Five* ianze. Je, Serikali inaweza kutusaidia katika vile vifaa kama mabati na kumalizia umeme? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri nadhani maswali mengi yanahu su nguvu za wananchi ambao wamefikia hatua fulani na kwa hiyo, nadhani ukitoa jibu la ujumla ili Wabunge wapate picha kwamba hatua ambazo wananchi wamezifikia huko, Serikali itachukua hatua gani? Kwa sababu naona maswali mengi yako hapo kwenye kuhusisha nguvu za wananchi lakini pia kuona mchango wa Serikali utakuwa ni nini kwenye hizo nguvu ambazo wananchi wameshazitoa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kama ambavyo umesema, tunaposema Serikali inamalizia maboma, tumepeiga mahesabu maana yake ni pamoja na kumalizia majengo yenye, kuezeka kuweka madirisha na kuweka madawati ndani ya vyumba vile. Tumekadiria karibu shilingi milioni 12,500,000/= kila boma moja kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu tumeshapeleka fedha mwezi wa Pili kama nilivyosema, ambapo sasa tunarajia watakuwa wanaendelea kumaliza, kwenye bajeti hii pia kuna mpango wa kupeleka fedha za kumalizia maboma ya Shule za Msingi na Sekondari. Kwa hiyo, nimtie moyo Mbunge kwamba tutapeleka fedha hizo. Hayo aliyozungumza ya umeme na miundombinu mingine itazingatiwa katika kurekebisha. Hiyo ni nchi nzima kwenye Majimbo yote. Ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu.

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Mara chache nimeuliza kwenye sehemu ya Walimu. Nnataka kuuliza, kwa nini kwenye Shule za Halmashauri na nje ya Halmashauri Walimu wanatengwa na wake zao wanapelekwa shule nyingine

hata zaidi ya kilomita 100? Hamwoni hiyo itaathiri familia ile ya Walimu na kwamba ni hatari kwa watoto kupata mimba? (*Makof/Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nia ya Serikali tungependa kila mtu akae na mwenza wake karibu, kwa maana kwamba mume akae na mke na mke akae na mume. Hayo ndiyo yalikuwa mapenzi na matarajio ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Waheshimiwa Wabunge wenyewe mmekuwa mkilalamika kwamba kuna maeneo mengine walimu hawapo kwa sababu wanahama sana; na sababu kubwa ni hiyo kwamba anamfuata mume wake au mke wake au sababu nyinginezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulisema, jambo hili baada ya kupata malalamiko hata kutoka kwa wananchi na Wenyeviti wa Halmashauri, Madiwani, Wabunge na wananchi wengine, kwamba kuna upungufu na kwa hiyo, ikama hai-*balance* katika maeneo yetu. Serikali ikalichukua na kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatengeneza mfumo ambao kama Mwalimu anataka kuhama kutoka shule A kwenda shule B, pale anapotoka asilete shida, na hapo anapoenda asiende kujaza watu kuliko mahitaji yake. Mfumo huo unaikaribia mwisho. Ukipamilika, hii shida ya walimu kuhama na ku-*balance* haitakuwa shida, tutaimaliza hilo tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo; hata Mbunge ukiomba, ukiwaambia mkoa mzima usambazaji ukoje, Halmashauri ikoje, hakutakuwa na shida. Kwa hiyo, naombaa Mheshimiwa Mbunge avute subira. Pia Walimu wanalalamika

sana, kuna mambo mengi ya uhamisho. Tutayafanya kazi yote na hii kero itaisha. Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Ofisi ya Rais Utumishi ya Utawala Bora. Mheshimiwa Zainab Mussa Bakar, Mbunge wa Viti Maalum sasa uulize swalii lake.

Na. 202

Haki ya Walimu Kupewa *Increment* Nchini

MHE. ZAINAB MUSSA BAKAR aliuliza:-

Walimu wote nchini wameingia katika Mkataba na Mwajiri ambao pamoja na mambo mengine unaonyesha uwepo wa *increment* kila ifikapo mwezi Julai; tangu iingie madarakani Serikali ya Awamu ya Tano Walimu hawajapewa stahiki hiyo.

Je, ni lini Walimu watalipwa stahiki hiyo kama malimbikizo au haki hiyo imeshapotea?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA - MHE. MWITA M. WAITARA (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naomba nijiblu swali la Mheshimiwa Zainab Mussa Bakar, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikitekeleza miongozo mbalimbali iliyowekwa kuhusu maslahi ya walimu ikiwa ni pamoja na kutoa nyongeza za mwaka za mishahara kulingana na utendaji mzuri wa kazi na kwa kuzingatia tathmini ya utendaji kazi ya kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kanuni E.9(1) ya kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma za mwaka 2009 Toleo la Tatu, Nyongeza ya Mwaka ya Mishahara haipaswi kuombwa au kudaiwa na Walimu, bali Serikali ndio yenye uamuzi wa kutoa au kutotoa nyongeza hiyo kutokana na Sera za kibajeti kwa mwaka husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watumishi wa Umma wakiwemo walimu wanastahili kupewa nyongeza ya mwaka ya mshahara iwapo bajeti ya mishahara inaruhusu. Kutokana na ufinyu wa bajeti, nyongeza hiyo haikutolewa kwa watumishi katika mwaka wa fedha 2003/2004, 2004/2005, 2008/2009, 2011/2012, 2012/2013 na 2016/2017. Hata hivyo, kwa kutambua utendaji mzuri wa kazi, Serikali ya Awamu ya Tano ilitoa nyongeza ya mwaka ya mshahara kwa watumishi wote wakiwemo walimu katika mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali itaendelea kutoa nyongeza ya mwaka ya mshahara kwa watumishi wote kadri uwezo wa kulipa utakavyoruhusu. Hata hivyo, walimu hawapaswi kudai malimbikizo ya nyongeza ya mwaka ya mshahara kwa miaka ambayo nyongeza hiyo haikutolewa. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zainab Bakar, swali la nyongeza.

MHE. ZAINAB MUSSA BAKARI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Sijaridhika na majibu ya Serikali. Swali la kwanza, ni takribani miaka sita au saba huko nyuma, kwamba hizo nyongeza hazitolewi na Serikali. Je, hatuoni kwamba Serikali inafanya makusudi kufinya bajeti ili kuwakosesha Walimu hao nyongeza hizo za mishahara?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, kama hii ipo kisheria, ni kwa nini Serikali inashindwa kutoa hiyo nyongeza ya mishahara na mara ya mwisho imetoa lini?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA - MHE. MWITA M. WAITARA (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA): Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge maswali yake ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma hapa kwenye jibu la msingi kwamba kulingana na kanuni za kiutumishi ambazo watumishi wote Tanzania sio Walimu tu watumishi wote wanajua, kwamba Serikali inapanga kuamka, kwa mfano kwaka huu wa fedha 2019/2020 kwenye bajeti yetu, kama hatukuuingiza kipengele cha nyongeza ya mishahara ambapo najua kuna tamko pale litatolewa kwenye Sherehe za Mei Mosi, maana yake ni kwamba mwaka huu kama hawataongeza mishahara halipaswi kuwa deni. Hili kwa mujibu wa kanunu za kiutumishi watumishi wote wanajua.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Serikali kutathimini, tumesema mara ya mwisho nyongeza ya mishahara imetolewa mwaka 2017/2018, kwa hiyo hili kimsingi sio deni. Serikali inapanga kuinua mapato yake kama kuna uwezo wa kuongeza inaongeza na haya hayapaswi kuwa malalamiko.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zacharia Issaay, swalii la nyongeza.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, moja ya tatizo linalopoteza *morality* ya utendaji kazi katika watumishi wetu wa umma ni pamoja na kutokuweka wazi namna ambavyo Serikali italipa madeni ya huko nyuma ya watumishi wetu; na kwa kuwa kwa jambo hili watumishi wanakosa moyo wa kufanya kazi, je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kukaa na vyama vya wafanyakazi ili waweze kuona namna gani ya kutatua tatizo hili la madeni ya huko nyuma ili watumishi wetu wote waweze kufahamu

namna ambavyo Serikali kama mlezi wao na mwajiri wao itawatendea katika jukumu hili la kulipa madeni?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA - MHE. MWITA M. WAITARA (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA): Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeshafanya kazi madai ya Walimu na watumishi wengine na ilishakutana na viongozi wa vyama vya wafanyakazi na utaratibu upo wa kuweza kulipa fedha hizi. Kwa sasa hakuna mgogoro kati Serikali na wafanyakazi, madeni yanajulikana. Tunatafuta fedha na uwezo wa Serikali kuanza kulipa madeni haya. Hata hivyo tunalipa kila muda, sio kwamba bajeti ni kubwa kiasi hicho, kwa hiyo madeni yanalipwa, lakini pia tumeshakubaliana namna ya kwenda, deni halisi linajulikana kwamba kila mtu anadai kiasi gani na hilo linafanyiwa kazi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim usiwe unafanya fujo lakini Mheshimiwa Masoud unasimama tu sio lazima upige meza, karibu.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kukosekana kwa nyongeza ya mwaka kwa Walimu na wafanyakazi wengine (*annual increment*) kunapelekea wakati wakistaafu wanakosa haki yao ya msingi ya mafao ya kijumla, sambamba na *pension* yao wakati watakapostaafu.

Je, Serikali inawaambia nini Walimu ambao tayari wamestaafu mwaka jana na mwaka juzi ndani ya awamu

hii ambao sasa wamekosa hiyo *increment* ambapo inaenda kuathiri mafao yao ya kustaafu na *pension* yao ya kila mwezi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA - MHE. MWITA M. WAITARA (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA): Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Masoud kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe maelezo kwa ufupi sana. Jambo la kwanza kuna tofauti kati ya madai na nyongeza ya mishahara. Tumesema kwenye nyongeza ya mshahara Serikali inapanga bajeti kulinga na mwaka husika wa bajeti. Kama hujaongezewa hilo sio deni la hupaswi kudai na nimejibu kwenye jibu la msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, madeni, haya ndio haki ya watumishi kudai na utaratibu wake ni kama nilivyooleza namna ya kuweza kuyafidia. Walimu hata juzi Waziri wa Nchi ametoa tamko hapa, hata kupandisha madaraja imeelekezwa vizuri kwenye Waraka wa Waziri kwamba ni muhimu izingatiwe kama kuna watu wanakaribia kustaafu na hawajapandishwa daraja na wamekidhi vigezo, tuanze na hao.

Kwa hiyo hilo jambo la kuwa karibu na kustaafu limezingatiwa na hakuna mtu atakayenyimwa haki yake, deni ni deni hata kama mtu atakuwa amestaafu, atapewa na tutakapoanza kulipa madeni kimsingi tunaangalia wale wenye shida, wale waliostaafu ndiyo tunaanza kuwalipa na wengine wanaendelea. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 203

Ujenzi wa Barabara ya Mlima Nyoka-Songwe

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA aliuliza:-

Je, ni lini ujenzi wa barabara ya mchepuo ya Mlima Nyoka - Songwe yenye urefu wa kilometra 48.9 utaanza baada ya ya usanifu na upembuzi yakinifu kukamilika?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
(MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa ujenzi wa barabara ya mchepuo inayoanzia Uyole yaani Mlima Nyoka hadi Songwe kilomita 48.9 ni mahsus kwa ajili ya kupunguza msongamano wa magari katika barabara kuu ya *TANZAM* katika Jiji la Mbeya.

Mheshimiwa Spika, upembuzi na usanifu wa kina wa barabara hii ulikamilika chini ya usimamizi wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Hata hivyo, ilionekana kuwa ipo haja ya kufanya mapitio ya usanifu huo ambao katika mwaka wa fedha 2018/2019 kiasi cha shilingi milioni 2.6 kimetengwakwa ajili kupitia na kukamilisha usanifu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi huu umeingizwa kwenye mradi wa ukarabati wa barabara kuu ya *TANZAM* kuanzia Igawa hadi Tunduma unaofandhiliwa na Benki ya Dunia kwa kushirikiana na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba ulisainiwa tarehe 18 Disemba, 2018 kati ya Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) na Mhandisi Mshauri *Studio International* ya Tunisia ikishirikiana na *Global Professional Engineering Service* ya Tanzania kwa ajili ya kazi ya mapitio ya usanifu wa kina wa barabara hii. Kazi hii inatarajiwaa kukamilika tarehe 18 Februari, 2020. Hadi sasa Mhandisi Mshauri yupo eneo la mradi anaendelea na kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii itakapokamilika na Serikali kupata fedha, ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami utaanza.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swalii nyongeza.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Naibu Spika kutohana na jibu la msingi la Wizara nataka kujua kwanza, je, Serikali haioni kwamba inapoteza muda katika utekelezaji wa miradi mbalimbali hususan miradi ya barabara kwa kufanya upembuzi yakinifu, usanifu kwa muda mrefu?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, barabara hii ni barabara muhimu sana katika uchumi wa Mkoa wa Mbeya na Mkoa wa Songwe. Je, hawaoni kuna umuhimu wa kuongeza muda wa kufanya kazi kwa haraka ili hii barabara iweze kukamilika na wananchi wa mikoa hii miwili waweze kufaidika katika ujenzi wa kiuchumi katika Taifa hili la Tanzania?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mwakagenda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, upembuzi yakinifu, usanifu wa kina utaratibu wa manunuzi na ujenzi ni utaratibu wa

kimataifa na maana yake ni kuhakikisha kwamba hiyo kitu inaitwa *value for money* inapatikana vizuri kwa sababu msipofanya taratibu mkaainisha mahitaji yote, matokeo yake ndio kufanya upembuzi ambao ni pungufu na mkiingia tenda mnaweza msipate *value for money*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, hoja yake ya kwenda haraka Serikali inaenda haraka ili kuhakikisha na sehemu kubwa ni msongamano wa pale Mbeya Mjini, ndio maana tunataka kuchepusha iili tutajenga mchepuo kwa ajili ya malori, lakini pale katikati kwa ajili ya kupanua ili msongamano usiwe mkubwa pale mjini Mbeya.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, swali la nyongeza.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu na mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri; kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri alikuwepo Mbeya kwenye ziara na Mheshimiwa Rais Mkoani Mbeya na aliona mwenyewe msongamano ulivyo kwa barabara hiyo ya *TANZAM*, ambayo kwa kweli inahudumia sio Mikoa ya Mbeya na Songwe tu, ni nchi nzima pamoja na nchi ya *DRC*, *Zambia*, *Malawi* pamoja na nchi zingine.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza ujenzi wa barabara hiyo kwa fedha yake yenyewe ikisubiri fedha za Benki ya Dunia?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali moja dogo la nyongeza la Mheshimiwa Mwambalaswa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kuanza kabla ya kukamilisha usanifu, lakini suala la msongamano wa magari lina *solution* nyingi pia ukisimamia taratibu za kiusalama na

ndio maana tuna Jeshi la Polisi bado wanameneji vizuri ili msongamano ule usiwe mkubwa na ndio maana msongamano upo kwa muda fulani fulani tu, lakini muda mwingine panakuwa pamekaa vizuri.

Mheshimiwa Mwambalaswa, hili tunalifanyia kazi, Serikali inatambua hiyo changamoto, kwa hiyo asiwe na wasiwasi, baada ya muda mambo yote yatakwenda vizuri. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Allan Kiula, swali la nyongeza.

MHE. ALLAN J. KIULA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa daraja Sibiti sasa limekamika kwa maana magari yanapita pale juu na Mheshimiwa Rais alitoa ahadi ya ile lami, sasa tungependa kujua kwamba ujenzi wa hizo kilomita 25 za lami umefikia wapi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali moja dogo la nyongeza la Mheshimiwa Kiula kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa Daraja la Sibiti limekamilika na tayari tumesaini mkataba na mkandarasi yule yule ili aweze kujenga zile kilomita 25 za lami. Kwa hiyo, fedha ipo na mkandarasi yupo na mkataba umesainiwa, anaendelea kujenga kwa kiwango cha lami hizo kilomita 25. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde, Mbunge wa Mtera, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Felister Bura.

Na. 204

**Hitaji la Maktaba ya Kumbukumbu ya Mwalimu
Nyerere – Dodoma**

**MHE. FELISTER A. BURA (K.n.y. MHE. LIVINGSTON J.
LUSINDE) aliuliza**

Kwa kuwa Serikali imehamia Dodoma, je, kwa nini Serikali isijenge Maktaba yenye kumbukumbu za kazi za Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ambayo pia itakuwa sehemu ya utalii kwa watu wa ndani na nje ya Mkoa wa Dodoma?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA
MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, napenda kijibu swali na Mheshimiwa Livingstone Lusinde, Mbunge wa Mtera, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kuzingatia umuhimu wa kuhifadhi kumbukumbu za Waasisi wa Taifa ambao ni Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Hayati Abeid Aman Karume, ilitunga Sheria ya Kuwaenzi Waasisi ya mwaka 2004. Sheria hii inaelekeza uhifadhi wa kumbukumbu hizo na kuanzishwa kwa kituo cha kutunza kumbukumbu. Aidha, Umoja wa Afrika uliiteua Tanzania mwaka 2011 kuwa Mratibu wa Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika ambayo, pamoja na mambo mengine, imetoa kipaumbele katika uhifadhi wa kazi ambazo alifanya Baba wa Taifa na mashujaa wenzake katika ukombozi wa Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni katika msingi huo Serikali kwa kushirikiana na UNESCO, imekarabati studio za iliyokuwa Redio Tanzania Dar es Salaam zilizopo barabara ya Nyerere na kuwa kituo adhimu cha kuhifadhi na rejea ya kazi za Baba wa Taifa. Serikali vilevile, inaunga mkono juhudzi za taasisi

kadhaa nchini katika kuhifadhi amali za urithi wa kumbukumbu za Baba wa Taifa. Baadhi ya taasisi hizo ni kama ifutavyo:-

Maktaba ya Taifa, Dar es Salaam; Makumbusho ya Taifa, Dar es Salaam; Makumbusho ya Mwalimu Nyerere, Butiama; Ofisi ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa; Taasisi ya Mwalimu Nyerere; na Vituo vya Television vya *TBC* na *ITV*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika, Serikali imeteua Wilaya ya Kongwa, Dodoma kuwa Kituo Kikuu cha Kumbukumbu za Ukombozi wa Nchi yetu ambapo miundombinu kadhaa ya uhifadhi wa historia itajengwa zikiwemo kazi adhimu za Baba wa Taifa. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Felister Bura, swali la nyongeza.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa majibu mazuri ambayo tumeyapata. Pamoja na majibu hayo, nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza, tunaipongeza Serikali kwa uamuzi wa kujenga Kituo Kikuu cha Kumbukumbu Wilayani Kongwa kwa sababu Kongwa ina historia ya wapigania uhuru. Je, kituo hicho kitaanza kujengwa lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa ushirikishwaji wa wadau huharakisha shughuli za maendeleo na nimeona katika Maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wadau wameshirikishwa, Wachina wamejenga majengo mazuri na makubwa pale chuo kikuu Dar es Salaam. Je, Serikali ina mpango wowote wa kushirikisha wadau ili jengo hilo likamike katika uongozi wa Awamu ya Tano?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi

hii kumpongeza Mheshimiwa Felister Bura kwa niaba ya Mheshimiwa Livingstone Lusinde kwa maswali yake mazuri ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilianza na kwanza ameanza kwa kutoa pongezi kwa Wizara, tumepokea pongezi hizo. Vile vile swali lake la msingi la kwanza ametaka kujua, je, ni lini kituo hicho kitaanza kujengwa rasmi. Tayari ujenzi wa hiyo kituo ulishaanza na tulishaanza tangu mwaka 2015 ambapo ukarabati wa hicho kituo uliana. Hata hivyo, kwa sababu ni suala la kibajeti na kwenye bajeti yetu ya mwaka jana kuna fedha ambayo ilitengwa kwa ajili ya kwenda kukarabati kituo hicho. Kwa hiyo, naomba nichukue nafasi hii kuweza kumhakikisha Mheshimiwa Bura kwamba ukarabati wa hicho kituo na kuweka miundombinu mingine unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni kwa sababu lengo la Wizara ni kuhakikisha kwamba hicho kituo kinakuwa pia center kwa ajili ya masuala mazima ya utalii. Kwa hiyo mipango ambayo ipo pale ni mikubwa mpango mmojawapo ni kuhakikisha kwamba tunajenga kituo cha ndege lakini vilevile tuweze kujenga *hotel/za five stars* pale ili kiweze kuwa kituo kikubwa cha masuala ya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake pili ametaka kujua kwamba kuhusiana na kuweza kushirikisha wadau. Kama ambayo nimejibu kwenye jibu langu la msingi ni kwamba sisi kama Wizara suala hili hatufanyi peke yetu tumekuwa tukishirikiana na wadau. Kwa hiyo, nitumie fursa hii kuweza kuwashamsisha wadau mbalimbali waweze kushiriki katika kuhakikisha kwamba tunatunza hizi kumbukumbu za Mwalimu Nyerere. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwanne Mcemba, swali la nyongeza.

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la dogo nyongeza. Kwa kuwa Serikali imetamka Vituo vya

Kumbukumbu ya Baba wa Taifa na kadhalika, lakini Mkoa wa Tabora una historia kubwa, nilitegemea kwamba leo Mheshimiwa Waziri atatamka kwamba Tabora nayo iwemo katika orodha ya Kumbukumbu ya Baba wa Taifa. Nasema hivi kwa sababu uhuru na maelekezo mengine yote ya Baba wa Taifa yalitoka Mkoa wa Tabora, karata tatu zimetoka Mkoa wa Tabora. Baba Taifa ameacha historia kubwa katika Mkoa wa Tabora kwa kusoma na kadhalika.

Kwa hiyo, kwa kutokuweka orodha ya Kituo cha Tabora kikitambua rasmi kwa kweli hawautendei haki Mkoa wa Tabora. Je, ni lini sasa Serikali itaingiza katika orodha ya Kumbukumbu ya Baba wa Taifa kwenye vituo hivyo ambacho vimetamkwa hivi leo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Mwanne Nchemba, mama yangu kwa maswali ya nyongeza. Napenda nitumie fursa hii kumhakikishia kwamba kwa suala hili la uhifadhi wa Kumbukumbu za Mwalimu Nyerere kitu ambacho kama Wizara tunafanya, kwa sababu tulitaka tufanye katika mapana makubwa, tunayo sasa hivi Programu yetu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika.

Kwa hiyo, kupitia hiyo program Mkoa wa Tabora ni mkoaa mmojawapo kati ya mikoa 15 ambayo imeteuliwa na Wizara ili kuweza kuyabaini yale maeneo maalum ambayo yallitumika katika ukombozi wa Bara la Afrika. Kwa hiyo Mkoa wa Tabora upo, lakini ni katika ile Program kubwa ya Ukombozi wa Bara la Afrika. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mohammed Juma Khatibu, Mbunge wa Chonga, sasa aulize swalii lake.

Na. 205

Askari Polisi Kutesa Watuhumiwa

MHE. MOHAMMED JUMA KHATIB aliuliza:-

Je, ni katika mazingira gani Askari Polisi anapaswa au hulazimika kumtesa Mtuhumiwa wa makosa mbalimbali wakati akiwa mikononi mwake au kwenye Kituo cha Polisi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohammed Juma Khatib, Mbunge wa Chonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20, kifungu cha 11 kinaelekeza namna ya ukamataji. Aidha, kifungu hiki mahsusini cha ukamataji, hakimruhusu askari kumpiga au kumtesa mtuhumiwa wa makosa mbalimbali wakati akiwa mikononi mwa Polisi au kwenye Kituo cha Polisi.

Mheshimiwa Spika, Kanuni za Kudumu za Utendaji wa Jeshi Polisi la (*PGO*) zinakataza na kuelekeza utendaji mzuri wa Askari Polisi, ambapo askari ye yeyote atakapobainika kufanya vitendo vya kumpiga au kumtesa mtuhumiwa huchukuliwa hatua za kunidhamu ikiwepo kufukuzwa kazi na au kufikishwa Mahakamani.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mohammed Khatib, swali la nyongeza.

MHE. MOHAMMED JUMA KHATIB: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu hayo nina maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwa mujibu wa Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai pamoja na Kanuni za Utendaji wa Jeshi Polisi bado jambo hili linaendelea na ni suga sana.

Je, Serikali haioni kwamba iko haja ya kubadili mfumo wa utendaji kazi wa Polisi likaingizwa suala la haki za binadamu ili kuwa-*conscientious* Polisi katika utendaji wao wa kazi wakazizingatia hizo haki za binadamu? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swali la pili, kwa kuwa Katiba yetu inakataza uteswaji na pia kwa kuwa kuna Mkataba wa Kimataifa wa *Convention Against Torture*, je, Serikali haioni kwamba iko haja ya kuridhia Mkataba huu ili hawa watu wanaoteswa wakapata fursa ya kwenda kushtaki katika Mahakama za Kimataifa? Ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:
Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mohamed Khatib, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na pendelezo lake la kuubadili mfumo, tunadhani tatizo siyo mfumo, mfumo wa Jeshi letu la Polisi uko vizuri kwani Askari Polisi kabla hajaajiriwa tuna utaratibu mzuri wa kutoa mafunzo. Moja katika mambo ambayo tunayazingatia kuwaelimisha kuhusiana na sheria na kanuni pamoja na kutenda kazi zao kwa uadilifu kwa kufuata sheria na kanuni hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini inapotokea changamoto ambazo zinahusu ukiukwaji wa sheria, ni matatizo ya baadhi ya Askari mmoja mmoja. Kama nilivyojibu katika swali lake la msingi kwamba tunapogundua kwamba kuna Askari ambaye anafanya vitendo hivyo vya kunyanyasa raia huwa tunachukua hatua mbalimbali ikiwemo kuwashtaki na kuwafukuza kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi kwa maelezo hayo naona nimejibu maswali yake yote mawili kwa pamoja.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kumekuwa na malalamiko kutoka kwa watuhumiwa wanaoteswa wakiwa mikononi mwa Polisi kwa lengo la kulazimishwa kusema ukweli, hasa ule ambaao Polisi wanautaka wakati mtuhumiwa ana haki ya kutoa hoja yake au kuzungumza ukweli akiwa na Wakili au Mahakamani.

Je, Serikali haioni ni muda muafaka wa kufuatilia mateso haya ambayo watuhumiwa wanapewa na Askari ili kuondoa malalamiko haya?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Aida Khenani, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Ushahidi ya mwaka 1967, kifungu cha 31, inaeleza kuhusu namna ambavyo Polisi wanaweza kutumia nguvu kiasi katika kumhoji mtuhumiwa ili waweze kupata ushahidi. Pia sheria hiyo hiyo inaeleza kwamba ushahidi ambaao utapatikana si lazima Mahakama uuzingatie, Mahakama itazingatia ukweli wa jambo husika. Tafsiri yake ni nini? Tafsiri yake ni kwamba inapelekea kuwa-*discourage* Polisi kutumia nguvu katika kupata ushahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimezungumza katika jibu la msingi la swali kwamba tunapogundua kwamba kuna raia ambaye amefanyiwa vitendo ambavyo si kwa kibinadamu na Polisi basi sisi huwa tunachukua hatua. Tunaomba tutoe wito na rai kwa wananchi wote pale itakapotokea wananchi

kupata madhara kama hayo basi wachukue hatua stahiki za kutoa taarifa ili tuweze kuchukua hatua. Hatuwezi kuliruhusu au kukubali wananchi wetu wanyanyaswe na baadhi ya skari wetu ambao pengine hawaifi maadili ya kazi zao.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Daniel Edward Mtuka, Mbunge wa Manyoni Mashariki.

Na. 206

Ajali za Barabarani Singida

MHE. DANIEL E. MTUKA aliuliza:-

Kumekuwa na ajali za barabarani za kutisha katika Milima ya Sukamahela eneo la Mbwasa, Manyoni na Sekenke Shelui:-

(a) Je kwa kipindi cha miaka miwili yaani 2016 na 2017, ni ajali ngapi zimetokea katika milima tajwa?

(b) Je, ni watu wangapi wamepoteza maisha na wangapi walijeruhiwa katika kipindi hicho?

(c) Je, Serikali inatoa tamko gani ili kupunguza au kukomesha kabisa ajali katika maeneo haya ndani ya Mkoa wa Singida?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Edward Mtuka, Mbunge wa Manyoni Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya ajali 28 zimetokea katika kipindi cha miaka miwili yaani tarehe 1 Januari, 2016 mpaka tarehe 31 Disemba, 2017 katika sehemu hiyo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya watu 33 wamepoteza maisha na jumla ya watu 26 walijeruhiwa katika kipindi tajwa.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Jeshi la Polisi inawataka madereva kuwa makini wanapoendesha vyombo vya moto barabarani na wazingatie sharia, kanuni, taratibu na alama na michoro ya barabarani. Pia waendeshe kwa kuzingatia udereva wa kujihami (*defensive driving*) ili kuepusha ajali, kwani ajali nyingi zinazotokea katika maeneo haya zinasababishwa na uzembe wa madereva, ubovu wa magari, uchovu wa madereva hususani kwenye uwepo wa kona kali, milima na miteremko mikali.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Daniel Mtuka, swali la nyongeza.

MHE. DANIEL E. MTUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali lakini nina maswali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, uzembe na uchovu wa madereva, ubovu wa barabara, hii ni kampeni ya kila siku ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuzuia ajali lakini katika eneo hili bado ajali zinaendelea kutokea. Nilidhani labda Wizara ya Ujenzi itoe jibu la kiufundi zaidi kwa maana ya kurekebisha eneo hilo. Je, Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi iko tayari kufanya usanifu upya katika eneo hilo na kufanya marekebisho ili kupunguza ajali? (*Makofj*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa ajali zimekuwa nyingi sana katika eneo hilo, kwa mfano magari ya mafuta yamekuwa yakidondoka pale na moto unalipuka, majeruhi ni wengi lakini tumekuwa na tatizo la magari ya zimamoto pamoja na *ambulance*.

Je, Serikali iko tayari kutuletea magari ya zimamoto pamoja *ambulance* katika Wilaya ya Manyoni? Ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kujibu swalii la nyongeza kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kwamba kabla ya ujenzi wa barabara katika eneo ambalo analitaja, ajali ziliikuwa nyingi sana kuliko ilivyo sasa. Pamoja na ajali kuendelea kutokea, sisi Wizara ya Ujenzi baada ya ujenzi mara zote huwa tunaendelea kufanya tafiti ili kuona changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge eneo ambalo analitaja tutaweka msukumo mkubwa tuone kwa nini hizi ajali zinaendelea kutokea kutokana na hali ilivyo pale ili tuweze kuchukua hatua muafaka. Ni muhimu tu niendelee kusisitiza kama ilivyo kwenye jibu la msingi watumiaji wa barabara maeneo yote wazingatle alama za barabarani zinazowekwa kwa sababu maeneo ambayo ni hatari, sisi Wizara ya Ujenzi tumejitahidi kuweka alama kutoa tahadhali kwa watumiaji wa barabara ili muda wote tuwe salama tukiwa barabani.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumwambia Mheshimiwa Mtuka kwamba eneo hilo tutaliangalia kwa macho mawili ili tuone nini la kufanya. Hata hivyo, jambo hili lazima tushirikiane na watumiaji wengine wa barabara. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Fatma Toufiq, swalii la nyongeza.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo taarifa kuwa vituo vikubwa vinapima ulevi lakini kuna baadhi ya madereva wa magari makubwa wenye kuendesha masafa marefu wanavyopata muda wa kupumzika vituo vya njiani wanakesha wakinywa pombe na kusababisha ajali.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwadhibiti madereva hawa ili kupunguza ajali za barabarani? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Dodoma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ambazo tunachukua katika kudhibiti madereva walevi, likiwemo kusimamisha magari hasa haya ambayo amezungumza yanayobeba abiria na mizigo na kuwapima vilevi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tukifanya kazi hiyo maeneo mbalimbali nchini na kwa kiwango kikubwa tumefanikiwa kupunguza kwa kiasi kikubwa aina ya madereva ambao wanaendesha magari hali wakiwa wamelewa. Pale ambapo tunawabaini basi hatua za kisheria zinachukuliwa dhidi yao.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 207

Kupeleka kwa wakati Pembejeo katika Mkoa wa Katavi

MHE. TASKA R. MBOGO aliuliza:-

Mkoa wa Katavi unapata mvua za masika kuanzia mwezi Septemba na Oktoba lakini mara nyingi pembejeo zimekuwa zikichelewa kupelekwa wakati mwingine hadi mwezi Novemba:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka kwa wakati pembejeo Mkoani Katavi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA)
alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatumia Mfumo wa Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja (*Bulk Procurement System - BPS*) kuagiza mbolea ya kupandia (*DAP*) na mbolea ya kukuzia (*UREA*). Mfumo huo unawezesha upatikanaji wa mbolea kwa wakati na kwa bei nafuu na kudhibiti upandishaji wa bei za mbolea kiholela.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inakamilisha zabuni ya kuagiza mbolea tani 280,000 ambapo tani 170,000 ni mbolea ya kupandia na tani 110,000 ni mbolea ya kukuzia kwa ajili ya msimu wa 2019/2020 kuitia mfumo wa *BPS*. Mbolea hiyo inatarajiwa kufikishwa hapa nchini mwezi Agosti, 2019 na kusambazwa kwa wakulima wa Mkoa wa Katavi na Mikoa mingine nchini kabla ya mwezi Septemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, ziada ya mbolea iliyopo nchini inaendelea kusambazwa katika maeneo mbalimbali kulingana na msimu wa kilimo, ambapo hadi tarehe 30 Machi, 2019 kulikuwa na mbolea tani 147,913 za mbolea zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo imeyaelekeza makampuni yanayoingiza na kusambaza mbolea ya *Premium Agrochem*, *OCP* na *Export Trading Group* kuhakikisha kwamba ifikapo Julai, 2019 kampuni hizo ziwe na maghala ya kuhifadhi mbolea na mawakala wa kusambaza mbolea katika mikoa inayotumia mbolea kwa wingi ukiwemo Mkoa wa Katavi ili kuondoa changamoto ya upungufu wa mbolea kwa wakulima katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imelielekeza Shirika la Reli Tanzania kutoa kipaumbele cha kusafirisha mbolea ili kusafirisha mbolea nyingi kwa wakati mmoja na gharama nafuu ili kumfikia mkulima kwa wakati na bei nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inakusanya mahitaji ya mbegu bora na viuatilifu katika mikoa mbalimbali ili kuhamasisha kampuni na wafanyabiashara kupeleka pembejeo hizo kwa wakulima kabla ya msimu wa kilimo kuanza na wakati na kwa kuuza kwa bei ya mauzo na bei nafuu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Taska Mbogo, swalii la nyongeza.

MHE. TASKA R. MBOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri wa Kilimo, ninayo maswali maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la kwanza, kwa kuwa Mfumo wa Uagizaji wa Mbolea kwa pamoja unatumika tu kwa mbolea za *DAP* na *UREA*. Je, ni kwa nini sasa Serikali isitumie mfumo huu kwa kuagiza mbolea nyingine za *NPK*, *CAN*, *SA* na pembejeo nyingine? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa Mkao wa Katavi ni umbali wa kama kilimita 1,500 kutoka Dar es Salaam, kwa hiyo, mbolea inaposafirishwa na magari inakuwa na bei juu zaidi.

Ni kwa nini sasa Serikali isiweke utaratibu wa kusafirisha mbolea hiyo kwa njia ya treni ili mkulima wa Mkao wa Katavi apate bei nafuu ya mbolea? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA): Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Taska Mbogo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Taska Mbogo alitaka kujua kwa nini Serikali tuisitumie Mfumo huu wa Uagizaji wa Mbolea kwa Pamoja (*BPS*) kwa mbolea zingine kama *NPK*, *CAN* na *SA*. Kwanza, mfumo huu tumeanza kuutumia mwaka jana na umeonyesha matokeo mazuri. Tusingeweza kuingiza mbolea zote kwa wakati mmoja lakini baada ya mafanikio tuliyoyaona katika mfumo huu, mwaka huu tumeshaanza kuutumia mfumo huu kwa ajili ya mbolea ya *NPK* kwa wakulima wa tumbaku na sasa tutaendelea na utaratibu ili kuingiza mbolea tajwa, viuatilifu na pembejeo zingine katika mfumo wa *BPS* ili kurahisisha upatikanaji wa mbolea kwa haraka na bei nafuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, anasema kwa sababu Mkao wa Katavi uko mbali na Dar es Salaam, ni vizuri tungesafirisha mbolea hizi kwa njia ya treni ili kupunguza gharama za usafiri. Tunachukua mawazo haya na tulishayafanyia kazi, tangu mwaka jana kama nilivyo sema hii mbolea ya *NPK* tulisafirisha kwa kutumia treni na gharama za usafiri zilishuka na mbolea hii kufika kwa wakulima kwa wakati. Mawazo yake tunayachukua ili tuyahamishie katika mazao mengine. Kama nilivyojibu kwenye swali langu la msingi, tayari tumeshalielekeza Shirika letu la Reli Tanzania ili

kutoa kipaumbele kwenye kusafirisha bidhaa ya mbolea ili kushusha gharama za usafiri.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Joram Hongoli swali la nyongeza.

MHE. JORAM I. HONGOLI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya asilimia 75 ya wananchi wa Tanzania ni wakulima na wanaishi maeneo ya vijijini. Hawa wafanyabiashara aliotataja Mheshimiwa Naibu Waziri wenge makampuni wanaonunua mbolea hizi, wamekuwa wakinunua na kuziweka mjini na inawapasa wakulima sasa watoke vijijini kwenda kununua hizo mbolea mjini kitu ambacho kimekuwa kikiwasababishia gharama za mbolea kupanda sana? Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba mbolea hizi zinapatikana kwenya Kata au Tarafa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Halmashauri ya Wilaya ya Njombe tuna maghala na maeneo mengi ya Njombe kuna maghala kwenye Kata hizi. Je, Serikali ina mpango gani ili kuhakikisha hawa wafanyabiashara wanapeleka mbolea hizi kwenye Kata ili gharama za usafirishaji ziweze kupungua kwa wakulima? Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA): Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joram Hongoli, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli wakulima wengi wanaishi vijijini na kama nilivyojibu kwenye swali la msingi, tumeshayaelekeza makampuni yote yanayoingiza mbolea hapa nchini na wasambazaji wawe na mawakala kila Mkoa

na Wilaya na pia wawe maghala ili kuwezesha mbolea hizi zinapoingia Dar es Salaam kufika kwenye mikoa yote inayotumia mbolea kwa wingi. Pia tumevielekeza Vyama vyat Msingi vyat Ushirika na Vyama Vikuu, kuwa mawakala kwa ajili ya usambazaji wa mbolea kwenye Kata na Vijiji katika Mikoa na Wilaya zinazolima mazao mbalimbali.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, Mbunge wa Msalala sasa aulize swali lake.

Na. 208

Ujenzi wa Kiwanda cha Kuunganisha na Ku-coat Mabomba

MHE. EZEKIEL M. MAIGE aliuliza:-

Serikali ya Tanzania ni mdau mkubwa wa Mradi wa Bomba la Mafuta ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga na Serikali pamoja na wawekezaji katika mradi huu walishateua eneo la kujenga kiwanda cha kuunganisha na ku-coat mabomba katika Mji Mdogo wa Isaka.

Je, ni hatua gani imefikiwa katika ujenzi wa kiwanda hicho?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, Mbunge wa Msalala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania) linalojulikana kama bomba la Afrika Mashariki (*East*

Africa Crude Oil Pipe – EACOP Project) umeainisha maeneo ya ardhi kwa ajili ya kazi za awali. Maeneo hayo yanazingatia vipaumbele vya mradi ikiwa ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ya kiwanda cha upigaji rangi mabomba uliopo kati ya Kijiji cha Sojo, Kata Igusule, Wilaya ya Nzega, Mkoa wa Tabora karibu na eneo la reli inayoenda Isaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa kiwanda hicho muhimu katika mradi wa bomba utaanza mara tu baada ya kukamilika kwa zoezi la kuthaminisha na kutoa ardhi husika na kukabidhiwa mkandarsi wa ujenzi. Kwa sasa, taratibu za utoaji ardhi ziko katika hatua za mwisho na zinatarajia kukamilika mapema mwezi Julai, 2019. Mkandarasi anatazamia kukabidhiwa eneo la mradi na kupeleka vifaa mwezi Septemba 2019. Aidha, mpango wa usimamizi wa mazingira na jamii umekamilika na kuidhinishwa na Baraza la taifa la usimamizi wa mazingira *NEMC*.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ezekiel Maige swali la nyongeza.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake pamoja na majibu hayo naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati utafiti wa awali unafanyika kuhusu maeneo yanayofaa kwa ajili ya mradi huu waliokuwa wakifanya utafiti walifika pia Isaka na Igusule kama ambavyo jibu limesema na baada ya maamuzi kufanyika kwamba mradi huu unajengwa Igusule walisema bado kuna miundombinu muhimu ya Isaka ambayo itatumika ikiwa ni pamoja na Ofisi za *TRA*, Bandari ya Nchi Kavu, Reli, Umeme pamoja na ofisi zingine za Kiserikali.

Sasa nilitaka kufahamu kwa sababu pia walisema wataweka *transit yard* pale Isaka nilitaka kujua hatua gani imefikiwa kwa ajili ya upataji wa eneo hilo la *transit yard* na maandalizi ya wananchi wa Isaka kwa ajili ya kushiriki katika huo mradi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kwa kuwa mradi huu unatoa fursa za kibiashara na ajira kwa wananchi waliowengi sana wa maeneo hayo. Je, ni maandalizi gani ya kijumla ambayo yamefanyika kwa ajili ya kuandaa wananchi hawa wa Isaka pamoja na Igusule ili waweze kushiriki katika kunufaika na mradi huo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana kwa namna ambavyo amekuwa akifuatilia mradi huu wa Bomba la Mafuta kutoka Hoima Uganda na namna gani wananchi wake hususan wa Jimbo la Msalala watakavyoweza kufaidika na maswali yake mazuri ya nyongeza na mara baada ya kukubali uamuzi wa wabia wa mradi huu wa eneo la kujenga kiwanda iwe Igusule.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa kuwa maswali yake ya nyongeza yamehusiana na miundombinu mingine ni kweli tafiti mbalimbali zimeendelea kufanyika kuhuisha miundombinu mbalimbali ikiwemo reli, ikiwemo ofisi mbalimbali za kiserikali itakavyotumika katika mradi huu na nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika eneo la Isaka hapo pia vitajengwa ofisi ya mradi huu ya *EACOP* na miundombinu mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia wananchi wake na ye ye mwenyewe anajua eneo la Igusule ni kama kilometra 5 tu kutoka Isaka. Kwa hiyo, ni wazi kabisa wananchi wa maeneo ya Isaka na maeneo mengine ya Mkao wa Shinyanga pamoja na Mkao wa Tabora watapata fursa mahususi kabisa katika mradi huu ikiwemo ajira na masuala mengine ya kibiashara na mpaka sasa mradi huu umeajiri takribani watanzania 229 kwa hizi hatua za awali lakini kuna makampuni nane yanatoa huduma mbalimbali katika mradi huu lakini pia faida zake mojawapo ni utoaji wa ajira utakapoanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikutaarifu tu kwa sasa mazungumzo yanaendelea na kwamba hatua ambayo imefikiwa sasa hivi ni tumefika mbali na tunatarajia mradi huu kuanza mwezi septemba 2019. Kwa hiyo, utakapoanza utaleta tija kubwa na faida kwa wananchi wa mikoa nane iliyopitiwa na bomba hili, wilaya 24, kata 134 na vijiji 280.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

MHE. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana yaliyosemwa na Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niwadhibitishie Waheshimiwa Wabunge Serikali kwa kutambua umuhimu wa mradi wa bomba hilo la mafuta na jinsi litakavyoweza kukuza ajira na uchumi wa Taifa letu, Ofisi ya Waziri Mkuu imeandaa programu maalum ya *local content* na tumeanza mafunzo maalum katika mikoa hiyo yote nane ili kuwahabarisha wananchi katika mikoa hiyo ni namna gani wanawenza wakatumia fursa mbalimbali ambazo zitapatikana katika mradi huo muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe wito kwa Wabunge wote ambao wanatoka katika mikoa ambayo inapitiwa na bomba hilo tuweze kuwasiliana ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu ili kuwaweka pamoja wananchi wao waweze kufaidika na mradi wa bomba la mafuta katika fursa mbalimbali zitakazopatikana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Ally Saleh swali la nyongeza.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante pamoja na majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Jenista na Mheshimiwa Naibu Waziri suala la *Local content* ni muhimu sana katika nchi yoyote ili uchumi ubakie ndani na sio utoke nje. Lakini inahitaji maandalizi kama alivyosema. Sasa hivi sasa tuna *sectoral individual locally content policies*. Je, Serikali iko tayari sasa kuja na sera kubwa na mabadiliko

ya sheria juu ya *local content* na pia sheria hiyo iwemo na vifungu ambavyo vinaweza kuwawzesha wananchi kifedha ili wafaidi *local content*?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu majibu.

MHE. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa swali la nyongeza liliolulizwa na Mheshimiwa Ally Saleh na Mheshimiwa Ally Saleh anafahamu kwenye Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria tumekuwa tukitoa taarifa hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshaanza hiyo kazi nzuri baadhi ya sheria ambazo zimekwisha kutungwa kwa mfano Sheria ya Mafuta na Gesi, hizo zote zimeshawekewa misingi ya kisera ya *local content* na imeshaanza kufanya kazi kwenye kanuni na sheria hizo. Lakini naomba nimhakikishie ili kufanya maandalizi hayo muhimu Ofisi ya Waziri Mkuu imeshatoa mwongozo wa *local content* katika miradi yote ya kimkakati ambayo inaendelea kwa sasa ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hii miradi yote ujenzi wa reli na miradi mingine yote mikubwa ya kimkakati sasa hivi mwongozo wa *local content* umekuwa ukitumika na sisi kama Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi tunasimamia kwa karibu sana kuhakikisha wazawa wanafaidika na miradi hii mikubwa ya kimkakati ndani ya Taifa letu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zedi.

MHE. SELEMANI J. ZEDI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, hili eneo la Sojo Kata ya Igusule ambako pameamliwa kujengwa kiwanda hiki liko jimboni kwangu na wananchi wametoa hekari 400 ili kupisha ujenzi wa kiwanda hichi muhimu. Na kwa kuwa majibu ya Mheshimiwa waziri

wamesema mwezi wa tisa ambayo ni miezi minne tu kutoka sasa mkandarasi anakabidhiwa eneo.

Je, nilitaka kujua kwamba Serikali inaweza kutoa commitment kwamba ndani ya kipindi hichi cha miezi minne kabla mkandarasi hajapewa hilo eneo wananchi wote waliotoa hekari 400 watakuwa wamelipwa fidia zao?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara Majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza na yeye pia nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia mradi huu mkubwa wa ujenzi wa bomba hili la mafuta na tija yake kwa wananchi wa maeneo yake hayo, kwa eneo ambalo limechaguliwa kujenga kiwanda cha kuunganisha mabomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimdhibitishie Mheshimiwa Mbunge moja ya kazi muhimu ambayo imefanyika ni kutambua mkuza ambako bomba litapita na tunatambua bomba hili ambalo litakuwa na urefu wa kilometra 1445 na zaidi ya kilometra hizo 1147 ziko upande wa Tanzania, Serikali yetu kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Makazi na *TPDC* imetambua ule mkuza na imeshafanya tathimini ya mali mbalimbali ambazo ziko katika huo mkuza ikiwemo eneo hilo la ujenzi wa kiwanda hichi cha *courtyard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimthhibitishie tathmini imekamilika na kwa kuwa tupo katika hatua nzuri ya mazungumzo ya *Host Government Agreement* baada ya hapo tutaenda Share Holders Agreement na kasha kufanya maamuzi ya *investment decision* na hatua zote hizi zipo katika mchakato wa miezi hii ambayo imesalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimthhibitishie tu Mheshimiwa Mbunge na kwa utashi wa viongozi wetu Marais wan chi mbili hizi, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli na Mheshimiwa Yoweri Kaguta Museveni wa Uganda kwamba mwezi wa tisa

utakapoanza mradi huu wananchi wote watakaopisha mkuza huu wa bomba watakuwa wamefidiwa kwa sababu tathmini ile imekamilika na sasa yapo tu mapitio ya mwisho ambayo yanafanywa baina ya Wizara ya Nishatu wataalamu, *TPDC*, Wizara ya Ardhi, Maendeleo Nyumba na Makazi na taasisi nyingine za Kiserikali. Nikushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunamalizia swalii letu la mwisho la Wizara ya Maji, Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki Mbunge wa Maswa Magharibi sasa aulize swalii lake.

Na. 209

**Mradi wa Maji Kutoka Ziwa Victoria Kutofika
Maswa Magharibi**

MHE. MASHIMBA M. NDAKI aliuliza:-

Usanifu wa Mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Miji ya Bisega, Bariadi, Itilima, Meatu na Maswa umekamilika kwa kiasi kikubwa lakini utanufaisha watu wa Maswa Mjini na baadhi ya vijiji katika Jimbo la Maswa Mashariki na kuliacha Jimbo la Maswa Magharibi bila ya maji ya uhakika:-

Je, kwa nini Serikali isichukue maji kutoka mji wa Algudu ambako tayari maji yameshafika na umbali ni mfupi ili Wananchi wa Kata za Malampaka, Mataba, Nyabubunza, Badi, Shishiyu, Masela, Sengwa, Jija, Kadoto, Mwanghondoli, Mwabayamla, Isanga, Busagi na Buchambi waweze kunufaika?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maji, majibu.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki Mbunge wa Maswa Mashariki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali natekeleza mradi wa maji safi kutoka Ziwa Victoria kwenye Miji ya Busenga, Bariadi, Itilima, Mwanhuzi na Maswa na vijiji vilivyo kilometra 12 kutoka bomba kuu la maji. Serikali pia inatekeleza mradi wa maji safi kutoka Ziwa Victoria kwenda katika Miji ya Ngudu na vijiji vilivyo ndani ya kilometra 12 kutoka bomba kuu. Vijiji hivyo ni Runele, Ngatuli, Nyang'onge, Damhi na Chibuji. Mradi huu ulihusu ulazaji wa bomba kilometra 25 na sehemu nyingine ya bomba kuu ilitumika bomba la zamani la mrai wa visima uliojengwa miaka ya 70. Bomba hilo ni lenye kipenyo cha nchi nane na kulingana na usanifu halitoshi kupanua zaidi kwenda Malampaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikal kuitia programu ya maendeleo ya sekta ya maji imetekeleza miradi ya maji ya Malampaka, Sayusayu, Mwasayi, Njiapanda na Sangamwalugesha ambayo miradi hii imekamilika na wananchi wanapata maji safi na salama. Serikali pia imekamilisha usanifu na uandaaji wa wa makabrasha ya zabuni kwa miradi ya maji ya Mwabulindi, Mwamanegé na Badi ambao utahudumia vijiji vitatu vya Muhiba Jihu na Badi yenyeze.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mashimba Ndaki swali la nyongeza.

MHE. MASHIMBA M. NDAKI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa muda niulize maswali mawili ya nyongeza. Nishukuru pia kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri lakini nilikuwa na ushauri mmoja na swali moja. Ushauri kwa kuwa Serikali imeamua kutoa maji kutoka kwenye maziwa makuu kama Ziwa Victoria na maziwa mengine ili kuwapa wananchi wake maji ya kutosheleza ingekuwa vizuri sasa inapobuni miradi hii ikafikiria kuwapa maji watu wanaohusika, lakini pia ikafikiria mbele uhitaji wa maji jinsi ulivyo mkubwa kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano Mradi wa Maji wa Ngudu kama ungebuniwa vizuri ungeweza kabisa kutoa maji

kwenye vijiji na kata nilizozitaja. Kwa hivyo inapobuni miradi ifikirie kupeleka mradi kwa watu wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali kwa kuwa pia nilishapeleka andiko kwaajili ya kupata maji ya Ziwa Victoria kutoka Wilaya Kishapu kwenda Kata ya Sengwa yenye vijiji vya Seng'wa, Mwanundi, Mandale, Mwabomba na Seng'wa yenyewe. Ni lini sasa wizara itaweka pesa kwenye mradi huu ili uweze kutekelezwa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maji majibu.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya ziada ya Mheshimiwa Ndaki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni ushauri tumeupokea ambapo na ni mipango ya Serikali kwamba tukianza kutengeneza miradi mikubwa lazima tuangalie maeneo ya mbali ili kuhakikisha wananchi wengi wanapata maji safi na salama na ndio maana sasa hivi miradi yote tunayojenga tunaochukua maji kutoka Ziwa Victoria tunatoa maoteo au tunapeleka maji mpaka kilometra 12 inapopita bomba kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili ni kweli tumepokea andiko lake na andiko hilo lina gharama takribani shilingi bilioni kwa ajili ya kutoa maji kwenye bomba kuu la Kashuasa na kupeleka maji kwenye vijiji vya Manawa, Sengwa, Mwabomba, Mandale na Mwanundi ambao tunalipitia sasa hivi na mara baada ya kulipitia tutafanya utaratibu wa manunuzi ili tuhakikishe kwamba wananchi wa maeneo hayo wanapata maji safi na salama kutoka Bomba kuu la *KASHUASA*.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na sasa nilete kwenu matangazo ya wageni tulionao Bungeni siku ya leo. Kwanza ni wageni walioko Jukwaa la Spika, wapo wageni ambao tulikwishawatangaza jana. Pia yupo mgeni wangu ambaye

ni Mkuu wa Kitengo cha Mafunzo, Sera, Utafiti na Maandalizi ya Makada Idara ya Itikadi kutoka Makao Makuu ya CCM Mkoa wa Dodoma Ndugu Mary Mwenisongole, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia Wageni wa Waheshimiwa Wabunge na wa kwanza ni wageni 40 wa Mheshimiwa Japhet Hasunga Waziri wa Kilimo amba ni wapiga kura wake kutoka Vwawa Mkoa wa Songwe wakiongozwa na Mchungaji Emmanuel Silungwe, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni 49 wa Mheshimiwa Agness Mathew Marwa amba ni madiwani, wenye viti na makatibu wa UWT kutoka Wilaya ya Serengeti Mkoani Mara wakiongozwa na Ndg. Maria Kisiri na Ndugu Esther Buruma karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao wageni 16 wa Mheshimiwa Joram Hongoli amba ni madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe wakiongozwa na Katibu wa CCM Wilaya Ndg. Valentino Hongoli, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia Wageni wawili wa Mheshimiwa Allan Kiula amba ni Mwenyekiti wa CCM Wilayani Mkalama Ndg. Jilala Mhela pamoja na jamaa yake Ndg. Alpha Shukia kutoka Mkalama Mkoani Singida, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni 47 wa Mheshimiwa Ritta Kabati amba ni wanafunzi 41 na walimu 6 kutoka Shule ya Sekondari Mlandege iliyopo Mkoa wa Iringa wakiongozwa na Ndg. Albert Mwilasi, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao wageni 10 wa Mheshimiwa Maria Kangoye amba ni wanafunzi kutoka Chuo cha Mipango cha Mjini Dodoma wakiongozwa na Mwenyekiti wa UVCCM Wilaya ya Butiama Ndugu Deus Wambura, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Rehema Migilla amba ni maafisa elimu kata kutoka Mkoa wa Tabora Ndugu Raphaeli Mageni na Ndugu Iddy Migila, karibuni sana.

Tunae pia mgeni wa Mheshimiwa Pauline Gekul ambaye ni mpiga kura wake kutoka Babati, Mkoa wa Manyara na huyu ni Ndugu Lambomba Bahati, karibu sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni waliopo Bungeni kwa ajili ya mafunzo wanachuo 100 kutoka Chuo cha Utumishi wa Umma Dar es Salaam Magogoni ambao wamelitembelea Bunge kujifunza jinsi linavyofanya kazi zake wakiongozwa na Ndugu Ezekiel Chipembe, karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge hao ndio wageni tulionao siku ya leo na tutaendelea na ratiba iliyo mbele yetu. Katibu!

NDG. RUTH MAKUNGU- KATIBU MEZANI:-

HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi,
Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020**

(Majadiliano Yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na majadiliano, lakini naona Mheshimiwa Khatib amesimama. Mheshimiwa Khatib.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. MOHAMMED JUMA KHATIB: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nimesimama kwa Kanuni ya 68(7) inayokwenda pamoja na ya 46 ambazo zinahusu maswali kujibiwa kwa ukamilifu na Mawaziri katika Bunge. Nilipouliza maswali mawili, Mheshimiwa Naibu Waziri alinijibu swali moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nilitaka kujua, pamoja na kwamba Katiba yetu inakataza Polisi kuwatesa watuhumiwa na kwamba kuna Mkataba ule wa Kimataifa, *International Convention Against Torture*, kwa nini Serikali haiuridhii huu? Maana mpaka leo haijauridhia. Kwa nini

hairidhii huu watu wanaoteswa wakapata fursa ya kushtaki katika Mahakama za Kimataifa pale wanapoteswa? Mheshimiwa Naibu Waziri akajibu yote mawili kwa pamoja wakati maswali haya yalikuwa yanajieleza yote, yanajitegemea, yeye akayachanganya kwa pamoja?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwa tunapoteza saa moja na nusu humu Bungeni kwa kipindi hiki cha Maswali na Majibu ili kuweka mwenendo wa masuala ya nchi sawa, lakini Mawaziri wanakuja wanatuvunga hapa, sijui inasimama vipi! Kwa hiyo, naomba mwongozo wako. Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Khatib alikuwa na swali leo ambalo liko chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na kwa maelezo aliyyoatao ni kana kwamba swali lake la nyongeza la pili halikujibiwa kikamilifu na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mujibu wa Kanuni yetu ya 46 ambayo inataka Waziri anayeulizwa swali ajibu kikamilifu. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, ili niweze kufahamu kama swali lilliyoulizwa na Mheshimiwa Naibu Waziri alivyojibu maswali yote mawili kwa pamoja halijajibiwa kikamilifu ni lazima nипитie Taarifa Rasmi za Bunge. Kwa hiyo, huu mwongozo nitautoa baadaye.

Hata hivyo niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge, maswali ya nyongeza kwa mujibu wa Kanuni zetu huwa yanataka uulize ufanuzi kwenye majibu yaliyotolewa. Maswali ya nyongeza kwa mujibu wa Kanuni zetu yanataka uwe unaomba ufanuzi kwenye majibu yaliyotolewa. Huo ni mwongozo wa jumla tu kuhusu maswali ya nyongeza, lakini mwongozo alionomba Mheshimiwa Khatib nitautoa baada ya kupitia Taarifa Rasmi za Bunge kuona maswali mawili ya nyongeza yaliulizwa vipi na Mheshimiwa Naibu Waziri alijibu vipi yote kwa pamoja?

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na wachangiaji wetu. Nimeshaletewa majina kwa mujibu wa Kanuni zetu. Tutaanza na mchangiaji wetu wa kwanza, Mheshimiwa Charles Kitwanga atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe na Mheshimiwa Riziki Lulida ajiandae.

HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi,
Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020**

(Majadiliano yanaendelea)

MHE. CHARLES M. KITWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze moja kwa moja kuchangia ajenda hii muhimu sana, lakini nitaiangalia kwa mapana yake zaidi ya badala ya ufinyu unaoangaliwa na baadhi ya watu wengi na nitaiangalia katika upande wa uchumi nikizingatia zaidi *balance of payment*. Nataka nizungumzie ATC na SGR na kama nitapata muda nitakwenda zaidi katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukianza na ATC, nizungumzie kimapana katika uchumi hasa tukiangalia *tourism*. Kwa mwaka 2017 *tourism* iliingiza shilingi bilioni 2.25 sawa sawa na asilimia 27 ya *total export* zote katika *goods and service* kwa nchi yetu. Kwa mwaka 2018 iliingiza Dola bilioni 2.45 sawa sawa na asilimia 29. Sasa tukiangalia ATC, nini mchango wake na utakuwa mchango wake katika *tourism?*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia sasa hivi, Kenya Airways inafanya safari tano kila siku kutoka Nairobi kuja Dar es Salaam na safari tatu kila siku kutoka Kenya kuja Zanzibar. Kwa nini wanafanya hivyo? Kwanini ATC isifanye hilo? Ni kwa sababu sisi tuliiicha ATC. Sasa tuone umuhimu wa ATC katika kuchangia *tourism* katika nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoangalia *ATC* kwa kusema kwamba watu wa Misungwi watapanda ndege, yaani nashindwa kuelewa, ni kufikiri kidogo sana. Tufikiri kiupana. Tukiangalia *ATC* pale itakapoanza kwenda katika *far East* kwamba iende India au China italeta watalii. Watalii watafika Dar es Salaam watachukuliwa watakwenda *KIA*, watakapofika *KIA* wale ndugu zangu wenye *Land Rover*, wale wenye *Pick-up* watawachukua watalii kufika karibu na Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, watakapofika Mlima Kilimanjaro wale wananchi wa kawaida kabisa kule Kilimanjaro watakuwa wapagazi, watabeba ile mizigo ya watalii kwenda kupanda Mlima Kilimanjaro. Umemgusa raia wa mwisho kabisa na pale hujazungumzia *ATC*. Uone umuhimu *ATC* itakaosaidia katika uchumi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuiangalie sasa *ATC* katika umuhimu wake *regionally*, halafu tutaangalia *intercontinental* inachangia vipi? Tutakapokuwa na *ATC* inaenda India ambayo ni shirika letu, maana yake sasa zile fedha ambazo zinachuliwa na mashirika ya nje kuleta watalii Tanzania zitakuwa zimeingia kwa *ATC* ambayo ni mali ya Watanzania na zitaongeza hilo pato kwenye *tourism* katika uchumi wetu. Watu hilo hatuwezi kuliangalia. (*Makofi*)

Mheshimiwa naibu Spika, siyo hivyo tu, tutakapokuwa tumetoka pale kwenye *ATC*, wale watalii watakapokuwa ni wengi zaidi wanakuja kwetu, pato la Taifa litakuwa limeongezeka zaidi. (*Makofi*)

Nawaomba ndugu zangu, badala ya kushambulia kununua ndege, tumpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu mwenye mawazo mapana. Anaona mbali zaidi, anaangalia kiupana zaidi lakini sisi tunaangalia kiufinyu kwa kuangalia ndege itabeba watu wa Misungwi. Hiyo siyo nia njema ya Rais wetu kuweza kuisaidia nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba Watanzania wote tumuunge mkono Mheshimiwa Rais wetu kwa kufanya

kazi na kufikiri zaidi katika maeneo yetu. Tusianze kufikiri kidogo kidogo. Watanzania na ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, niwaombe sasa tuone ni kwa namna gani tunaweza kuisaidia ATC badala ya kuibeba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi itaanza *intercontinental flights*, kwa maana itakwenda India na China kuleta watu zaidi, lakini biashara tunayoiangalia, tusiangalie utalii tu, tuangalie je, watu watakaotoka uwanja wa ndege watakuwa wametoka wapi? Sasa hivi kuna watu wanakuja pale Kariakoo kutoka Malawi, Zambia, Congo kufanya biashara. Sasa kama tutakuwa na ndege yetu ambayo itaifanya Kariakoo iwe ni Guangzhou ya Afrika, Guangzhou ya Afrika, maana yake ni nini? Maana yake utalii ambao unasababishwa na ATCutakuwa umeleta uchumi kukua zaidi katika nchi yetu. Kwa hiyo, tuangalie kwa mapana, tuache kuiangalia ATC kiufinyu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nishauri kwamba badala ya kuwa na hizi ndege chache ATC waangalia *regionally*, *wa-focus* zaidi sasa hivi, ndege hizi *Air Bus* ziwe ni za *regional*; ziende *South Africa*, Burundi, Rwanda, lakini wanunue tena ndege nyingine ambazo zitatusaidia sasa; hao watu wanaokuja kutoka kule watasambaaje katika nchi yetu? Kwa hiyo, waangalie uwezekano wa kununua ndege nyingine za aina hiyo kwa ajili ya *local*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *International* au *intercontinental* sasa hivi wameanza *ku-focus* kule *Far East* baadaye kwa mipango yao ya kati au ya jinsi wanavyoona waweze *ku-focus Europe*. Kwa hiyo, wanunue ndege nyingine kubwa zaidi ambazo ni sawa sawa na hizi *Dream Liner* ziweze kwenda *Europe* na sehemu nyingine. Vile vile, kwa baadaye zaidi tuweze *ku-focus market* ya Marekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisiishie hapo tu, kwa sababu ya muda niweze kuzungumzia umuhimu vilevile wa reli yetu katika *transit trade*. Again hii ni mawazo mapana ya Mheshimiwa Rais wetu. Mimi nampenda kwa sababu *he think big* na watu wengi tuna-*think low* halafu tuna-*think very*

narrow hatumwelewi. Sasa niwaombeni, mimi nina-*think big and I think wide*, ndio sababu leo naamua kutoa shule hii muweze kuelewa. (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *transit trade* tukiiangalia tuone ni kwa namna gani *ita-contribute* kwenye uchumi wetu. Tunaposema *transit trade* tunaangalia nchi zinazopakana nazo. Mimi nashangaa wakati mwengine hatuwazi namna gani tunaweza kuzitumia hizi nchi tunazopakana nazo kukuza uchumi wetu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiwa na reli ambayo itatoka Dar es Salaam kwenda Kigoma, Mwanza na pale Fela tukatengeneza *Economic Zone*, maana yake sasa mizigo itatoka moja kwa moja kwa haraka Dar es Salaam kwenda Mwanza. Ikisafika Mwanza pale, ndugu zetu wa Rwanda na Burundi watachukua ile mizigo kutoka pale Fela na kuweza kuisafirisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tutakuwa na *Economic Zones*, kwa mfano, tuwe na *Economic Zone* katikati ya Dar es Salaam na Dodoma ambapo tutakuwa na maeneo maalum ambayo biashara mbalimbali zitafanyika na tutaitumia hiyo reli sasa kusafirisha *products* zetu kwenda kuziuza. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakuwa na *Economic Zone* nyiningine, yaani *business centers* pale katika kwa mfano kati ya Dodoma na Tabora, maana maeneo yale sasa wakiwemo wafugaji, wakulima na wafanyabiashara wengi wakiwa na *productions* ambazo zinakwenda kwenye *centre* ambapo kuna *businesses* wanazozifanya, wasiwe na matatizo ya kuweza kusafirisha vifaa vyao au vitu vyao kwa ajili ya *raw material*/kuja kufanya *production*. Wawewe kupata usafiri wa rahisi na kitu kitakachowea kutusaidia ni reli yetu hii.

Kwa hiyo, Watanzania tuwaze na tuweze kufikiria namna gani hii *SGR* itatusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka reli... (*Makof*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kitwanga, muda wako umekwisha. Ahsante sana.

MHE. CHARLES M. KITWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Nina uhakika wale wanaojua upande gani nausema wamepata shule yangu. (*Makofi/ Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Tumefurahi sana kukuona Mheshimiwa Kitwanga.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimemwita Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe, atafuatiwa na Mheshimiwa Riziki Lulida, Mheshimiwa David Ernest Silinde ajiandae.

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi asubuhi hii nami niweze kuchangia katika Wizara hii ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda niishukuru Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kuititia Wizara hii imeweza kufanya mambo makubwa katika Sekta zote hizi za Uchukuzi, Mawasiliano na Ujenzi, hasa katika ununuzi wa ndege, upanuzi wa viwanja vyta ndege, ujenzi wa reli ya kisasa na mengineyo. Kwa ujumla naomba niwashukuru na niwapongeze viongozi wote wa Wizara kuanzia Waziri na Watendaji wake ambao siyo rahisi kuwataja mmoja mmoja, lakini kwa umoja wao wameweza kufanya kazi vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na suala la barabara ya Tabora mpaka Mpanda. Naiongelea hii barabara kwa sababu imeanza kusemwa toka mwaka 2005 mpaka leo hii. Nami nafahamu kwamba Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli akiwa Waziri wa Ujenzi,

alishaiombea fedha kupitia Benki ya Afrika. Sasa sielewi kunasuasua nini? Kwa sababu ukiangalia kila kipande kipande kina viasilimia; kuna asilimia 12 Kasinde - Mpanda, kuna asilimia 18; Urila kuna asilimia 15.9.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hizi asilimia hatujui tunazipimaje na hatuelewi hii barabara pamoja na kwamba ilishapata fedha, itakwisha lini ili iweze kuwasaidia wananchi wa Mkoa wa Katavi, Tabora, Rukwa, Mbeya na wote watakaopita ile njia pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Katavi, Jimbo la Kavuu, (samahani Jimbo la Katavi ni la Mheshimiwa Waziri), Jimbo la Kavuu na Wajimbo la Katavi wenye kuitia Inyonga ili waweze kuita kwenda mpaka Mwanza, mpaka Kahama waweze kufanya biashara zao? (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, naomba niongelee suala la Mfuko wa *USCAF*. Napenda niwashukuru mfuko huu wameweza kufanya kazi kwa uwazi na kwa namna ambavyo wananchi wameweza kuuelewa sasa, kwa sababu mwanzo walikuwa hawauelewi lakini leo wananchi wanaelewa chini ya Eng. Ulanga na wengineo wote wanaofanya nao kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kawaida yangu ndani ya Jimbo la Kavuu, lazima niombe masuala yote yanayohusu maendeleo. Kupitia Mfuko huu wa *USCAF* naomba Kata nzima ya Maji Moto na vitongoji vyake na vijiji vyake iweze kupata mawasiliano ya uhakika. Naomba Kijiji cha Mawiti, Kabunde, Mainda, Lunguya, Ikupa, Luchima, Kanindi, Minyoso, Kwamsisi, kote naomba niweze kupata mawasiliano. Ni vijiji ambavyo havina mawasiliano. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri Watendaji wako hapa na Mheshimiwa unapafahamu huko kote, naomba wananchi hawa wapate mawasiliano ili tuweze na sisi kwenda kisasa, tuweze kufanya biashara za kuitia mitandao. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudi kwenye suala la Shirika la Reli. kwenye suala la Shirika la Reli, mimi

toka nimeingia humu nimekuwa nikiongelea Shirika la Reli hasa kwa usafiri wa kutoka Mpanda – Tabora, Tabora – Dodoma, mpaka Dar es Salaam. Jamani, kuna kipindi alikuwa Mheshimiwa Waziri Mwakyembe, nikamwambia kule siyo mabehewa ya kukaa binadamu. Nilishaongea mwaka 2017 kwamba basi waangalie namna bora ya kubadilisha hata mabehewa, wananchi wale waweze kuingia kwenye mabehewa safi na salama. Mabehewa yale ni machafu, yemechoka. Kwa nini yaletwe Mpanda? Kama yamechoka, yakawekwe Morogoro, mtuletee mabehewa mazuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongee kuhusu mpango wa anuani za makazi wa *Post Card*; mpango huu ni mzuri sana. Tumetenga fedha nyingi sana. Nawaomba Watendaji tufanye vizuri. Leo ukitoka hapo nje ukienda Chuo cha *CBE*, ile tuliyoweka pale imeshang'oka. Sasa tuweke imara zaidi. Ni mpango mzuri unaoweza kutambulisha nchi yetu vizuri na ni kwa utaratibu wa maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niwaombe, hebu tuongeze ile *value for money* katika huu mradi kwa sababu hauna *impact*, hata ukitembea hapa kwenda hapo *stand Kimbinyiko*. Bado haijakaa vizuri. Kwa hiyo, naomba sana tuboreshe hili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudi katika barabara ya Kibaoni – Maji Moto – Inyonga, bado inafanyiwa upembuzi yakinifu na nini. Naomba Mheshimiwa Waziri aje na majibu. Hii pia ni ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kutoka Maji Moto mpaka Inyonga kwa kiwango cha lami, lakini pia kutoka Kibaoni; siyo Kibaoni tu mpaka Inyonga, mpaka Kansansa, Klyamatundu.

Mhesdhimiwa Naibu Spika, najua tumejenga daraja la Momba, Serikali yangu imefanya vizuri, nashukuru tunaipongeza, lakini hii barabara pia lazima tuifungue ili wananchi hawa wa Jimbo langu la Kavuu waweze kutoka Kansansa ama Maji Moto, ama Kibaoni mpaka waweze kufika Mbeya, Mbeya waweze kwenda Kalambo, Kalambo waweze kwenda Kasesha, Kasesha waweze kwenda

Mpulungu, waingie Zambia, waingie Mozambique waweze kufanya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila siku naliongea hili. Lazima tuangalie sasa ni namna gani tutatanua wigo wa kutoka Tunduma na wa kutoka Kalambo ili tuingie mpaka Mozambique. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudi niongelee sasa daraja langu la Msadya. Daraja hili naomba Waziri anisikilize vizuri, nimekwishapeleka maombi, najua linahudumiwa na Ofisi ya TAMISEMI kuititia *TARURA*, lakini *TARURA* hawa ni Wizara hii ndiyo wanawapatia pesa. Leo ni mwaka wa tatu wananchi wangu wa Kata ya Mbebe, Mwamapuli, Chamalendi mpaka wanaotoka Kibaoni hawawezi kufika Usevya ambako kuna kituo cha afya nilichosimamlia mwenyewe na Mkurugenzi wangu cha mfano! Pia Mheshimiwa Ummy alishafika pale akakiangalia, ni cha mfano, niwaombe sana wanitengee pesa kwa ajili ya hili daraja ili wananchi wangu waweze kupata huduma pale. Hawapati huduma mpaka sasa hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee suala la barabara ya Mpanda mpaka Kahama...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa, kengele ya pili imeshagonga. Ahsante sana.

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na naomba yote haya niliyoyaeleza yachukuliwe kwa umuhimu wake. Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Riziki Lulida atafuatiwa na Mheshimiwa David Silinde na Mheshimiwa Balozi Adadi Rajabu ajiandae.

MHE. RIZIKI S. LULIDA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru sana na niwashukuru Spika, Naibu Spika, Katibu wa Bunge, wafanyakazi wa Bunge na Wabunge wenzangu kwa kunisiaidia na kunitoa huzuni kipindi kigumu cha kupata msiba wa mtoto wangu ambaye alifariki. Nawe Naibu Spika ulikuwa mmoja wapo wa waliokuwepo mpaka tunasafirisha mwili wa marehemu kupeleka Dar es Salaam na tumezika, nashukuru *Alhamdulillah*. Mwenyezi Mungu awawezeshe na awalinde na Mwenyezi Mungu wote anasema *Inna lillah wainnailayhi rajiun* na kila nafsi itaonja umauti (*kullu nafsin dhaikatul-maut*).

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze Waislamu wote Tanzania na wasiokuwa Waislam kwa mwezi Mtukufu wa *Ramadhan*, nawatakia *Ramadhan Kareem* na Mwenyezi Mungu atujaalie katika Mwezi Mtukufu huu ailinde nchi yetu iingile katika amani, tusidhoofishwe na mabeberu ambao wanataka kutugawanisha na kutuweka katika mazingira magumu. Tanzania yenye amani inawezekana. Nashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, nitazungumzia suala la barabara, lakini hasa nataka nizungumze kwa dhati ya moyo wangu kuwa, kuna ubaguzi mkubwa unatendeka kwa kupitia Mawaziri wetu katika ugawaji wa barabara. Barabara haitakiwi kuonekana upande mmoja unapewa *priority* na upande mwingine unaachwa ukiendelea kulalamika kila mwaka. Hii haileti ufanisi na umoja tulikuwa nao katika Tanzania hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie Mkao wa Lindi katika mikoa nane ya ukoloni, tulikuwa katika mojawapo ya *province* nane za Tanzania, lakini leo kwenda Liwale, Liwale ni Wilaya ya zamani sana, inakuwa kama wako kisiwani. Watu wa Liwale wako Guantanamo. Leo mvua inanyesha inawachukua miezi mitatu mtu wa Liwale aweze kuja Dar es Salaam, akipata ugonjwa Liwale hawezi hata kwenda Lindi, jamani tufike mahali tusema basi tufunge ukurasa. tumelalamika barabara ya Liwale toka Waziri Mkuu wa Jimbo la Liwale alikuwa Rashid Mfaume Kawawa,

wanamuenzi vipi Kawawa katika Jimbo lake? Wanachofanya kipindi cha uchaguzi kutumia nguvu kubwa kutaka Jimbo, lakini je, wananchi wa Liwale wanawafanya nini? Kwenda Liwale ni kama adhabu na mfanyakazi wa Tanzania akitaka kuadhibiwa mpeleke Liwale. Mfanyakazi wakijiona hawamtaki wampeleke Liwale kwa maana Liwale ni Guantanamo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimezungumza kwa miaka, nimepeewa ahadi na Mawaziri kwa miaka, Mheshimiwa Mramba mpaka akasema mama mwaka huu ni wa mwisho nitakupelekea lami Liwale. Kwa masikitiko nataka niseme kitu kimoja kwamba, Bunge tutengue Kanuni ya kushika Msahafu au Biblia kwa kusema uongo humu ndani. Watu wanashika Biblia mwaka huu barabara itapatikana lisemwalo silo! Kwa nini tunashika *Quran*, kwa nini tunashika Biblia ikatuleta katika uongo, ina maana inatuingiza katika uongo na laana katika Bunge. Tutengue Kanuni, tutumie Katiba badala ya kutumia *Quran* maana *Quran* haitaki kusema uongo wala Biblia haitaki kusema uongo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais amezunguka Mtwara pamoja na mama Janeth, amesema kazi aliyoiona kwa barabara za kule kweli amehakikisha kwamba barabara ni mbovu, lakini kuna maeneo yanapata upendeleo, upendeleo kila mwaka, hii mpaka lini? Leo kwenda Liwale unaona Liwale mpaka Nachingwea barabara kubwa kiuchumi katika mikoa inayozalisha korosho, ni mikoa miwili ambayo na wa tatu ni Ruvuma. Wa kwanza ni Mtwara, wa pili Lindi na wa tatu ni Ruvuma. Asilimia 80 ya korosho ambayo ni uchumi mkubwa katika nchi hii inatoka sehemu hizo, lakini hakuna barabara. Wanalamika kuhusu *kangomba*, mtu yuko kijijiini, anaitoaje korosho yake kijijiini kupeleka katika magilio wakati hakuna barabara, sasa wale walangazi wanakwenda kuchukua kule kwa *ku-risk* na magari yao kutoka kule mpaka kufika mjini, leo wanawakamata watu kwa ajili ya *kangomba*, lakini je, wamewawekea barabara? Huwezi kumkata mtu bila kumwekea *alternative*, kunatakiwa kuwepo na *alternative*, barabara ziwepo vijijiini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo mikoa ambayo ina uchumi mkubwa sasa hivi tumeona *LNG* inaenda sasa hivi, miradi inakamilika kutaka kujenga *liquefied national gas industrial area* ambayo itawekwa Lindi, lakini hatuna *airport!* Ni kilometa 20 *only* kutoka *airport* kuja Kilikong'o, hakuna bajeti ya *airport*, je, hawa wafanyabiashara wakubwa wanaokuja kuwekeza katika mradi mkubwa wa matrillioni wataruka na ndege kutoka Mtwara. Mtwara mpaka Lindi wakati Lindi uwanja wa ndege kwa taarifa ya Bunge wa Lindi ni wa pili katika Afrika. Ndege ya kwanza ilikuwa inatoka London inatua Misri – Alexandria inakuja kutua Lindi inakwenda Afrika Kusini, tuko wapi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawafanya nini wananchi wa Mkoa wa Lindi? Kwa nini wanatudhalilisha wananchi wa Lindi? Tumefanya nini katika nchi yetu? Keki hili hili ya korosho na vitu vingine wengine wanafaidika zaidi kuliko kuyaangalia maeneo ambayo yana uchumi na uchumi bora katika nchi hili yametupwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Lindi, Mtwara na Ruvuma sasa hivi inabidi iwekewe *EPZA* yake ifanyiwe kazi kwa vile ndiyo mikoa ya kiuchumi, hakuna barabara. Utasikia barabara zinapeleka maeneo hata uchumi haupo na ubaguzi huu wa kupeleka *fund* nyingi katika maeneo mengine unauona kabisa. Tufike mahali bajeti isimame bila kuangalia pale paliposimama na maendeleo makubwa pasimame waende kwa maeneo ambayo watu ni maskini ili nao hawa wafaidike na sungura wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bandari ya Lindi ilikuwa ni bandari kubwa. Leo je, bidhaa zitaanza kupatikana kutoekana na miradi ya *LNG*, bandari iko wapi? Bandari iko Lindi, ukienda uani huwezi kuona utafikiri kichaka fulani tu, watu hata kuweka bajeti hamna, bajeti za kibaguzi, halafu wanakuja kutumia nguvu kubwa wakati wa uchaguzi maana yake ni nini? Haiwezekani! Wamefikia mahali wanawafanya watu wanakwazika kujiuliza na inakuwa ndiyo mahali pa watu kwenda kupiga vijembe, ninyi maskini, mikoa imetupwa, lakini ni kweli mikoa imetupwa. Nenda leo Liwale kuna nini, nenda

leo Milola kuna nini? Kutoka Lindi kwenda Milola hakuna barabara. Milola kwenda Nangaru na daraja limevunjika huu mwaka wa ngapi hakuna kinachosemekana. Nawaomba mpaka na Mawaziri kaangalieni mazingira, hakuna mtu anaye-*take action* nini maana yake? Basi tuamueni turudi Tanganyika yetu, tukakae na Tanganyika yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulifikia mahali tuliamua kuchanga kwa ajili ya kusaidia Lindi yetu tukasema haiwezekani, Lindi itachangiwa na Tanzania nzima, kuna nini Lindi? Barabara za Lindi ziko wapi? Nenda vijijini huko watu wanatembea kwa mguu, wanajitwika mitenga ndiyo maana hata wanakuwa wafupi kwa sababu kutwa mtu ana tenga kichwani. Hali hii ya umaskini wanayoipeleka Lindi inasababishwa na Serikali. Naomba barabara zikasimamiwe, nikitoka hapa nataka mguu kwa mguu na Waziri wa Ujenzi twende tukaangalie barabara Lindi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefika mahali tuseme wazi kuwa kuna maeneo mengine imetosha tupeleke mikoa ambayo iko maskini na mikoa ile barabara ipatikane, maji yapatikane, afya ipatikane, sio kwingine watu wanaburudika wame-leisure sisi wengine kwetu tunahangaika, tunatembea kilometra nyingi kwa miguu, kwa nini na wakatinchi hii ni yetu wote? Uchumi ni wetu wote, korosho yetu na mapato yapatikanayo kutokana na korosho ni ya Tanzania nzima, lakini sisi wenyewe tumewekwa nyuma tumekuwa kama boga, unasuka mkeka mwenyewe unalala chini. Hii haiwezekani na haikubaliki. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, gesi sasa hivi naona tayari mikataba inapita maana yake naona ninapoona, lakini cha kujiliza gesi ile maendeleo yake yako wapi, barabara zake za kuitisha vitu hivyo iko wapi? Inapita maporini humo hakuna kitu, hakuna barabara, mawasiliano yamekuwa magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nasema ahsante imetosha. Tunataka Lindi yetu yenye

barabara, Lindi yetu yenze afya, Lindi yetu yenze maji na hii inawezekana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa David Silinde, atafuatiwa na Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab na Mheshimiwa Abbas Hassan Mwinyi ajiandae.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kupata nafasi ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2019/20.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijazungumzia miradi ya kimkakati ya Kitaifa nitazungumzia mambo mawili madogo tu ya jimboni kwangu. Jambo la kwanza pamoja na shukrani ambazo zimetolewa za ujenzi wa Daraja la Momba ambalo limekamillka kwa karibu asillimla 97 na linatumika, sisi wananchi wa Momba tumefurahi sana, lakini tunaomba sasa ile barabara ya kutoka Mlowo – Kamsamba – Kiliamatundu ijengwe kwa kiwango cha lami kama ilivyo llani ya CCM ilivyoahidi, kama ilivyo ahadi ya Rais Mstaafu Mheshimiwa Jakaya Kikwete na Mheshimiwa Mkapa, wote waliahidi kujenga hiyo barabara lakini mpaka sasa hawajakamilisha. Barabara ya Kakozi – Kapele – Ilonga ambayo wameipandisha hadhi na hawajaifanyia kazi mpaka sasa, tunaomba ifanyiwe kazi haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nahitai kuzungumzia masuala ya Kitaifa ambayo kimsingi yanaweza yasieleweke vizuri na ndiyo maana unajikuta mara nyingi tumekuwa tukigongana. Mradi wa *SGR*, thamani ya mradi wote wa reli ya *SGR* ni dola za Kimarekani 7,000,000,000 na maamuzi yameshafanyika ya kujenga reli yetu kutoka Dar es Salaam - Morogoro mpaka Dodoma kwa awamu ya kwanza kabla ya kwenda kwa awamu ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tulishawaeleza Tanzania kwamba hatuna shida na reli inayojengwa, shida yetu ni namna mambo yanavyoteklezwa na nikasema hapa reli ambayo imejengwa, maamuzi ya awali yaliyofanyika chuma

chote kinatoka China – nje ya nchi. Chuma kidogo ambacho kimekuwa kikinunuliwa hapa ndani ya nchi wamekuja watu wenye viwanda kwetu, watu wa viwanda vya chuma wamepewa vile vitani kama vya kudanganyishia, tani 1,000 au 2,000 basi, lakini chuma chote kimetoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa haya tunasema ni makosa ambayo tumeshayafanya kabla hatujawaza mapema. Nimeamua kulizungumzia hili kwa sabbau najua awamu ya pili ya kutoka Makutupora kwenda mpaka Mwanza itafuatia, lakini kabla hatujaenda katika huo mradi tuna mradi wa Liganga na Mchuchuma. Liganga na Mchuchuma endapo tungewekeza kwenye kutengeneza chuma chetu maana yake hii fedha ambayo tunaitumia kwa ajili ya reli yetu hapa nchini tungekuwa tunanunua chuma ndani ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa juzi ulisikia ripoti ya *IMF*. Ripoti ya *IMF* imeshusha uchumi wa Tanzania kutoka kasi ya kukua ya asilimia saba mpaka asilimia nne na sababu walizozitoa nafikiri kila mmoja amejaribu kuzisoma na Serikali walituambia hapa tusiwhishe shughuli, tukakubaliana na hilo jambo, lakini Serikali wamekuwa wakitaja hizo *argument* zao huko mtaani kwamba mbona *IMF* hawaja-*include* miradi mikubwa kwa mfano reli ya *SGR* katika uchumi wetu pamoja na ndege.

TAARIFA

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpe Taarifa mzungumzaji. Mikononi mwangu nina barua ya *IMF* ambayo waliniandikia tarehe 18 April, 2019. Naomba niisome kwa sababu ni fupi sana. Inasema hivi:

"Dear Minister Mpango, This is to inform you that the IMF's communication department has been contacted by several leading news agencies today informing that they have copies of the staff report on the 2019 Article Four consultation and seeking comments on the report. In

accordance with the fund's transparency policy, our communications department has responded that the fund does not comment on leaked report. I would be grateful if we could discuss at your earliest convenience. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni Taarifa iliyovujishwa, sio Taarifa halali ya *IMF*. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tafadhali. Mheshimiwa Silinde, unaipokea Taarifa hiyo?

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba pamoja na kwamba tunapokea taarifa aliyopewa, lakini hicho kilichozungumzwa hakiondoi taarifa zilizokuwepo mle ndani, hakiondoi! *That's the fact!* Yaani bado ni asilimia nne, haiwezi kuondoa hiyo *fact!*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ambacho nilikuwa najenga, nafikiri Mheshimiwa Waziri ambacho alitakiwa anielewe ni kitu kimoja na hii ndiyo shida ya hili Taifa. Moja ya ambacho nilikuwa nakizungumza maelezo ambayo wamekuwa wakiyatoa kwamba kwa nini hiyo miradi mikubwa haiwi *included* kwenye ile Taarifa ni kwa sababu kumekuwa na *capital outflows* kubwa yaani tunatumia fedha ya ndani, tunanunua kila kitu nje ya nchi na ndiyo maana uchumi wetu unashuka kwa sababu hatu-*inject* fedha ndani ya uchumi wa Tanzania. Tumepata mradi lakini fedha kwenye *circulation* haipo! Hiyo ndiyo tofauti ya kwetu sisi na Kenya. Kenya...

NAIBU SPIKA: Sawa, sasa Mheshimiwa Silinde ngoja twende vizuri kwa sababu Taarifa uliyokuwa umezungumzia umesema ni ya *IMF* na barua tuliyosomewa ni ya *IMF*. Mimi naomba tuiji...

*(Hapa Mhe. Esther N. Matiko alikuwa akizungumza na
Mhe. David E. Silinde)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Esther muache asikilize Taarifa ninayompa mimi hapa ili aweze kufuata maelekezo,

ukimwongelesha atakuwa hanisikii, subiri mimi nimalize na wewe utazungumza.

Mheshimiwa Silinde kwa sababu Taarifa uliyokuwa unaizungumza umeanza kwa kusema Taarifa iliyotolewa na *IMF*imesema hivi. Taarifa aliyotoa Mheshimiwa Waziri inatoka huko huko *IMF* ikisema haijasema hivyo, kwa hiyo weka mchango wako vizuri ili taarifa zetu zikae sawasawa. Weka mchango wako vizuri Taarifa zetu zikae sawasawa.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Naibu Spika, naona hili jambo, labda kama nchi tuna-*complicate* sana kwa sababu ya *facts* ambacho kinaelezwa pale hawajakanusha kuhusu ukuaji wa uchumi wala hawaja-*comment* juu ya ile Taarifa na sisi hapa tunachojaribu kutaka *ku-rescue* hili Taifa hapa lilipo, ndicho ambacho tunachohitaji kukifanya. Sijui kama umenielewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningeweza kumwambia sijapokea, lakini ni taarifa kutoka *IMF*, ni barua ameandikiwa. Ukitosha ile taarifa yote utaona Maofisa wote wa Serikali wako pale. Sasa mimi najaribu kueleza kwamba tofauti ya kwa nini hawaja-*include* mradi yetu na ni kwa nini wenzetu Wakenya, mradi wao wao walikopa bilioni 5.5 *US dollar* wakaingiza kwenye mradi wao, kilichosababisha uchumi wao kukua kwa asilimia 1.5 kwa sababu fedha ilitoka nje ya nchi ikaingia ndani ya Kenya. Sisi Tanzania ni *vice versa*, fedha inatoka Tanzania, inakwenda nje ya nchi, hiyo ndiyo tofauti yetu sisi na watu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa hapa ambacho nataka nishauri, makosa yaliyofanyika awali kwenye kutoa fedha nyingi nje ya nchi, ndiyo nataka yasifanyike katika Mradi wa kutoka Makutupora kuelekea Mwanza kwa maana gani? Mradi wa Liganga na Mchuchuma gharama yake unahitaji kama dola bilioni tatu za Kimarekani, lakini ukishaukamilisha ule mradi kwenye mradi wa Liganga utapata chuma, utapata makaa ya mawe, utapata umeme na utachenjua madini mengine. Kwa hiyo tunapoanza kujenga mradi kutoka Dodoma kwenda Mwanza maana

yake chuma kitakuwa cha ndani ya nchi. Kwa hiyo hela yetu hii ya ndani itatumika hapa hapa, hatutaendelea kununua tena machuma kutoka huko China. Kwa hiyo hapo hata *IMF* watakavyokuja watakuambia kwa sababu fedha yote inabaki kwenye mzunguko, maana yake nchi yetu uchumi wetu utakua

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa unaweza ukajiuliza swalii dogo, kwa miaka minne mfululizo Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi mpaka sasa tumeiingizia shilingi trillioni 13.8. Mwaka huu wa fedha wanaomba shilingi trillioni 4.9, maana yake *in total* ni karibu shilingi trillioni 18.7, ndani ya miaka minne. Asilimia 40 ya fedha za miradi yote ya maendeleo ya Tanzania zipo Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sasa jiuлизе swalii, tume-*inject* fedha inakwenda kwenye shilingi trillioni 18 lakini matokeo ya kiuchumi yanakwenda *vise versa*. Badala ya uchumi kutoka asilimia 7 kwenda 8, matokeo yake inatoka 7 inakwenda 4, inakwenda *vise versa*. *That is the question* tunahitaji kupata majibu yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawashauri Serikali kwamba tumieni fedha ambayo inaingia ndani ya uchumi kwa ajili ya kubadilisha maisha ya Watanzania, hicho ndicho ambacho tunakitaka. Changamoto ambayo ipo watu wetu hawa hawapendi kusikiliza ukweli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *SGR* bado inaendeleoa, itatoka Dar es Salaam, itakuja Morogoro, *returning on investment* ni nini? Hili ni swalii ambalo tunapaswa kujuliza. Je, itabeba tu watu peke yake mpaka Morogoro? Jibu ni kwamba kubeba watu haiwezi kurudisha gharama ya fedha ambayo tumeiweka mle ndani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachotakiwa kufanya ni nini? Ndiyo maana nawashauri, sasa hivi wakati reli inakuja jengeni bandari kavu pale Morogoro. Ukishaweka bandari kavu pale Morogoro maana yake mizigo yote ambayo inakwenda nchi za *SADC*...

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

MHE. DAVID E. SILINDE: Pamoja na inayokwenda Mikoa ya Kusini reli ile itayopita pale itaibeba. Kwa sababu mradi wote...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Silinde, kuna taarifa.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Naibu Spika, nilindie muda wangu.

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpe taarifa mzungumzaji kwamba katika hali ya kawaida, unapofanya *investment* yoyote ile, hutegemei *return* ipatikane katika muda mfupi.

WABUNGE FULANI: Aaaaa.

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hata hiyo miradi tunategemea *investment* ipatikane baada ya miaka 5 au 10 ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Silinde, unaipokea taarifa hiyo?

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Naibu Spika, hamna taarifa hapa, hawataki kusikiliza ukweli tu. Sisi tunajaribu kuwashauri, shida mliyonayo Chama cha Mapinduzi mkishauriwa hamtaki, mkikosolewa hamtaki, mnataka nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ambacho najaribu kukieleza hapa ni kwamba kwa sasa mnatakiwa mjenje bandari ya nchi kavu Morogoro ambayo itasaidia kupeleka mizigo yote ya nchi za *SADC*, hicho ndicho kitu ambacho tunakihitaji kwa sasa. Nimesoma ile *package* ya kwanza ya mradi kutoka Dar es Salaam - Morogoro - Dodoma, nimeona

tuna lengo la kuweka bandari ya nchi kavu hapa Dodoma, sasa kabla hatujaanza hapo, kwa hii awamu ya kwanza tuweke bandari kavu pale Morogoro ili tuhakikishe kwamba *return on investment* iweze kujibu mapema kabla ya jambo lingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye jambo linguine maana kengele ya kwanza imeshalia ni barabara. Tanzania barabara ndiyo chanzo kikubwa cha ajali kuliko hata uzembe wa madereva, namba moja hiyo. Kwa sababu barabara zetu ni ndogo lakini hazirekebishwi kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuwe wakweli, Serikali haiwezi kufanya kila kitu kama ambavyo mmekuwa mkijiaminisha mbele za watu, haiwezekani! Kulikuwa na mradi hapa wa *Dar-Moro Express Way*, mradi ule ultakiwa tu uendeshwe kwa mfumo wa *PPP*ama kuropa *private sector*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niwaulize Serikali, unapomleta mtu akujengeta barabara, mkopo amekopa mwenyewe akajenga Dar es Salaam - Morogoro, barabara ile wanapita watu hata kwa kulipa fedha. Tunakwenda nchi za watu, tumekwenda South Africa, Ulaya na nchi zote, watu wanalipia gharama (*road toll*). Sasa mnasema kwa sababu ya reli, hatujengi *Dar-Moro Express Way* kwa sababu imekuwa *taken by event*, kwamba kwa sababu kuna reli basi hiyo barabara haiwezekani, yaani unaona ni *thinking* ya kurudi nyuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo yetu, ukijenga barabara kwa kutumia mfumo wa *PPP*, ukijenga madaraja kama Kigamboni, sifa inabaki kwa Serikali na haiendi kwa mtu mwagine tofauti. Tofauti yenu na sisi ninyi mnafikiri kwamba Serikali italeta maji, itajenga shule na kadhalika na ndiyo maana miaka yote, tangu mmekuwa madarakani kwa miaka 58 mambo yanakwenda polepole tofauti na kasi inayohitajika na mnataka pongezi kwa vitu ambavyo mnawiweza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri sasa watu wa *TISS* wafanye *vetting* ya watu wanaoweza kuongoza hii nchi ili kuhakikisha wanaipeleka mbele. Kuna watu wanafikiri kijamaa kuliko miradi inavyotaka kutekelezwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni *ATCL*. Hakuna mtu hata mmoja anayepinga *ATCL* lakini menejimenti lazima iwe huru, hiyo namba moja, wasiingiliwe wafanye kazi kibiashara. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakin pili, kuna vitu ambavyo sisi tutaendelea kuwakosoa kila siku hapa ndani. Wewe *Dreamliner* imekuja tangu Julai, 2018, karibu mwaka mzima imepaki pale, tunakaa tunaiangalia pale, ile ni hasara. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni sawa na mtu umenunua *coasteryako* kutoka Japan umeiweka nyumbani kwako unaiangalia, haiingizi kitu chochote. Kwa nini usisemwe, kwamba wewe unafikiri kibiashara au unafikiriaje? Hayo ndiyo tunayolalamikia kila siku. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia watu wa Rwanda, pamoja na kwamba wana Shirika la *Rwanda Air* lakin menejimenti ya Rwanda wamechukua watu wa Ethiopia, ndiyo wanao-run lile shirika halafu watu wa chini kule ndiyo watu wa Rwanda. Kwa sababu watu wa Ethiopia ndiyo wana uwezo mkubwa wa kuendesha mambo haya. Sasa na ninyi msione aibu kwenda kumchukua mtu Ethiopia, Rwanda akaja kuwasaidia. Hata *KQ*sasa hivi, miongoni mwa mabadiliko yao wamefanya hivyo. Msifanye maamuzi mkafikiri kwamba kila kitu kinawezekana. (*Makof!*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi hii. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab, atafuatiwa na Mheshimiwa Abbas Hassan Mwinyi na Mheshimiwa Boniface Mwitwa Getere ajilande.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kupata nafasi hii kuchangia hoja hii ambayo ni muhimu sana katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri Kamwelwe na Manaibu Mawaziri, Mheshimiwa Kwandikwa na Mheshimiwa Nditiye (Mzee wa Minara), Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote pamoja na Wakurugenzi wa ATCL, TTCL, TCRA, TANROADS na wengine wote. Nawashukuru sana kwa sababu Wizara hii kazi ambazo inazofanya ni nzuri sana na nafikiri kila mtu anaziona, katika sekta zote ambazo nimezitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii imebeba Wizara nyingi sana na imefukia mashimo ya Wizara nyingi kutokana na kazi zake nzuri ambazo wanazifanya. Siyo siri kwamba miradi hii mikubwa imeipa sifa sana nchi yetu na ni miradi ambayo itabdalilisha kabisa taswira ya Tanzania. Ni Wizara ambayo inatakiwa ipongezwe kwa sababu kwanza, Mawaziri na viongozi wake sasa hivi wanafanya kazi kubwa sana. Mawaziri hawa wametembea nchi nzima na wameona miradi ambayo iko kwenye mikoa yetu na wamejitahidi kwa kadri ya uwezo kutatua changamoto zilizopo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuzungumzia Jimboni hasahasa barabara yangu ya Amani - Muheza kilomita 36. Barabara hii imekuwa inatengewa fedha tangu mwaka juzi, shilingi bilioni 3, mwaka jana shilingi bilioni 5, mwaka huu karibu shilingi bilioni 2 lakini tatizo ambalo lipo ni la mkandarasi kutopatikana. Najua Meneja wa TANROADS Mr. Ndumbaro anafanya juu chini lakini kila ukimuuliza anakwambia hapana, bado kidogo, kuna mchakato wa mzabuni. Zabuni hii imetangazwa mara tatu, mara ya kwanza mkandarasi hakupatikana, mara ya pili mkandarasi hakupatikana na hii mara ya tatu ndiyo naambiya sijui kama

atapatikana na naambiwa mambo yote yako kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ndiyo uchumi wa Muheza. Muheza tunategemea barabara hii iwe kwenye kiwango cha lami ili iweze kuteremsha mazao kutoka Amani kwenda Mjini Muheza mpaka Dar es Salaam kwa ajili ya mauzo. Kwa hiyo, naomba uitolee maamuzi ili kabla mwaka huu wa fedha kuisha basi mkandarasi awe *site*. Nakumbuka Mheshimiwa Waziri nilikuona na nikakuomba kwamba fedha ambazo zimebekwa mwaka huu ni kidogo na ujaribu kuangalia namna ya kuweza kuziongeza. Nakushukuru sana kwa kupokea ombi hilo ambalo naamini utalishughililia. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na matatizo haya ya barabara ya Amani pia tuna matatizo ambayo tumeomba katika miaka hii miwili, mitatu iliyopita, kufanyiwa upembuzi yakinifu katikati ya barabara ya Pangani, *junction* ya Boza mpaka Muheza (kilomita 42) pamoja na Muheza – Maramba (kilomita 45) kwa matayarisho ya kuwekewa lami. Sikuona kwenye kitabu lakini naomba uangalie uwezekano ili ziweze kufanyiwa upembuzi yakinifu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni mawasiliano. Nimewasiliana sana na Mheshimiwa Nditiye, Naibu Waziri anayeshughulika na mawasiliano, kwa sababu mpaka wakati huu kiwango hiki tulichokifika kuwa na sehemu ambazo hakuna mawasiliano ni tatizo kubwa sana. Tarafa ya Amani mawasiliano ni tabu sana, ukiangalia Kata zote za Amani yenye, Mbomole, Zirai, Kwezitu, Misarai, Magoroto pamoja na sehemu za Kwebada mawasiliano ni mabovu sana. Jana tu nilikuwa naongea na wewe Mheshimiwa Naibu Waziri na ukanihakikishia kwamba utashughulikia. Napenda niliongelee hilo ulishughulikie ili na wananchi wa maeneo ya Amani waweze kusikia kwamba kweli suala hilo linashughulikiwa na mawasiliano hivi karibuni yatakuwa ni mazuri. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *SGR*, nimeona hapa kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri kwamba mpango wa

kuweka *SGR* kutoka Reli ya Tanga - Dar es Salaam - Arusha – Msoma upembuzi yakinifu ulishafanyika na sasa hivi mikakati inafanyika ya kumtafuta mkandarasi kwa njia ya *PPP*'ili na sisi reli ya Tanga tuweze kuwa na *SGR*. Suala hili ni la muhimu sana kwa sababu suala la *PPP* marekebisho yake tulishayafanya kipindi kilichopita na tunategemea kwamba suala hili lingeanza sasa hivi kutangazwa kwa sababu upembuzi yakinifu umeshafanyika ili tuweze kupata *SGR Tanga line*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwamba Bandari ya Tanga inaendelea kufanyiwa ukarabati. Kwa hiyo, suala hilo ni muhimu sana liendelee na liweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala la ndege kwenda Tanga - Pemba, tulisikia kwamba sasa hivi *bombardier* itatua Tanga na itakwenda Pemba na kurudi Dar es Salaam. Mpango huo mpaka sasa hivi naona kimya, ningeshukuru sana kama Mheshimiwa Waziri utakapokuja hapa ku-*wind up*, basi utuambie kwamba na sisi Mkoa wa Tanga hii ndege ya *bombardier* itaweza kutua kwenye uwanja wetu kwa sababu sasa hivi kiuchumi tunakwenda kwa kasi kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ambalo nataka kuongelea ni suala la *express way*, hili suala ni la msingi sana. Kila mwaka naongelea kwa nini hatuanzishi *road toll* kwenye barabara zetu. Ulimwengu mzima sasa hivi unakwenda na *road toll*, hakuna nchi ambayo utakwenda usikute imefungwa inatengenezewa *road toll* au kuna watu ambao wanalipa *road toll*. Hii ni njia mojawapo ya kuinua uchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi tulikuwa Kampala, tumeteremka *Entebbe* pale, *Entebbe* mpaka Mjini Kampala kuna *express way* wameshatengeneza wenzetu, mtu anachagua apite kwenye *express way* au aende kwenye barabara ya kawaida. Hivi vitu ni vya msingi na ni muhimu sana sijui kwa nini hii barabara ya Chalinze tusianzishe *express way*? Kama atapatikana mtu ambaye ana uwezo wa

kutengeneza, akaweka *road toll* yake, kwa nini tunakataa vitu kama hivi? Nashauri sasa hivi tuangalia umuhimu wa kuanzisha *road toll, express ways* ni muhimu sana kwa maendeleo ya miji yetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni suala la *SGR* ambalo mwenzangu Mheshimiwa Silinde hapa amelizungumzia lakini tunajua kwamba hawa watu wetu wenye viwanda vyuma, kweli hivi vyuma vilikuwa vinatoka nje lakini wewe mwenyewe Mheshimiwa Silinde utakubali kwamba wamekuja tangu juzi kwenye *Budget Committee* na wamekiri wameanza kupewa kazi hizo za kuweza ku-supply vyuma kwenye reli hii ya *SGR*. Hayo ni mafanikio kwamba sasa hivi wameanza na unajua kabisa kwamba Kamati ya Bajeti sasa hivi inashughulikia namna ya kufufua Mchuchuma-Liganga na jana tulikuwa na...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Abbas Hassan Mwinyi atafuatiwa na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere na Mheshimiwa Magdalena Sakaya ajandae.

MHE. CAPT. ABBAS ALI MWINYI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami nichangie katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema. Pia nichukue fursa hii kumpongeza Waziri Eng. Kamwelwe na Naibu wake wawili kwa kazi nzuri sana wanayoifanya ya

kutekeleza llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu kwa asubuhi ya leo nitajikita katika taasisi mbalimbali ambazo ziko chini ya Wizara hii. Nitaanza na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji ambacho kwa siku za karibuni tulipata fursa kwenda kukitembelea na Kamati. Tumeona hatua ya maendeleo iliyofikiwa na chuo hicho lakini tatizo kubwa ni kwamba kitendea kazi kikuu hakijapatikana ambacho ni ndege. Kwa heshima na taadhima naomba Waziri atakapokuja kufanya *wind-up*, aje kutueleza lini hasa fedha ambazo zimeahidiwa na Serikali za shilingi bilioni 4.2 zitatolewa kwa chuo hicho kwa lengo la kununua ndege *single engine* aina Cessna 172 ambapo mpaka dakika ndege hizo hazijapatikana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, tuna taarifa ya kwamba chuo hiki kitapata fedha kutoka Benki ya Dunia kiasi cha dola milioni 21.5. Fedha hizi pia zitatumika katika ununuzi wa ndege tatu, kwa hiyo, pamoja na zile mbili ambazo zimeahidiwa na Serikali zitafanya jumla kuwa tano. Mpaka ninavyozungumza hawana hata ndege moja katika kitengo hicho jambo ambalo kwa kweli linakifanya Kitengo hicho cha Usafiri wa Anga kudumaa, naomba Mheshimiwa Waziri aje kutueleza. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli wa hali halisi ilivyo sasa kuhusiana na uwiano wa marubani ambao wamepata leseni uko 60:40 yaani wageni wana asilimia 60 na wazawa wana asilimia 40 ya idadi ya marubani. Kwa hali hiyo basi, iwapo tutakisaidia chuo hiki, nafikiri uwiano huu utapungua kwa kiasi kikubwa. Itafika wakati sasa sisi kwa maana ya wazawa tutakuwa wengi zaidi kuliko idadi ya *foreigners* kama ilivyo sasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine nilikuwa nataka kugusia kuhusiana na Shirika letu pendwa la *Air Tanzania* ambapo kwa hali ilivyo hivi sasa linaendelea vizuri. Mengi ambayo nilikuwa nayakusudia kuyazungumza kwa siku ya leo wenzangu walionitangualia kama Mheshimiwa Kitwanga

ameyazungumzia, kwa hiyo, sasa hivi nitazungumzia vile vipande ambavyo ye ye haku vigusia. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli biashara ya ndege ni ngumu sana na gharama zake za uendeshaji hali hadhalika ni kubwa kupita kiasi. Napenda kukufahamisha tu kwamba, Rubani ye yote *validity* ya leseni yake ni miezi sita, ukimaliza miezi sita ina maana aidha ufanye *revalidation course* ambayo haifanyiki nchini bali ni nje ya nchi katika nchi za Canada, Uingereza au Ethiopia na watu gani wana-*incurred cost* hizo ni shirika lenyewe. Kwa hiyo, wameelemewa na mambo mengi sana, *cost* ya vipuri halikadhalika iko juu sana. Tairi tu lile la Dreamliner linaweza kufika hata dola 10,000, tairi tu moja. Kwa hiyo, mnaweza kuona gharama za vipuri zilivokuwa juu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda nishauri Serikali ni kwamba hatuwezi tukaendesha Shirika la Ndege kwa kutegemea fedha ambazo zinapatikana kutoka katika mauzo ya tiketi peke yake, haiwezekani lazima kuwe na mambo mengine, vyanzo vingine vya kupata mapato. Na vyanzo hivyo kwa upande wa Serikali wanaweza kutoa msahada hii *Air Tanzania* ikawa na *Ground Handling Company* yake yenewe hiyo itafanya wapate fedha mbadala inaweza alikadhalika ikapate ile *inflight catering service* zile na hiyo ni chanzo kingine cha fedha. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuwapatia sehemu ambayo kama godauni wale abiria ambao wanatoka nje ya nchi kuja kwetu wakija na mizigo yao na ile hasa ile ambayo iko *sensitive* kwa *temperature* inaweza ikahifadhiwa katika sehemu zile na baadaye sasa shirika likipata nafasi za kwenda kuzipeleka mizigo hiyo katika nchi za jirani kama Malawi na kadhalika na kadhalika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jana Mheshimiwa Shangazi alizungumza ya kwamba kuna haja ya kupata *Cargo Plane* nakubaliana naye kwa *hundred per cent*, isipokuwa ushauri wangu si lazima iwe *cargo plane hundred per cent per serve* lakini kuna ndege ambayo inaitwa Comb Q4100 ambayo

inachukua mizigo na abiria kwa wakati mmoja nafikiri aina hii ya ndege itakuwa inafaa zaidi kuliko kupata ile ambayo Mheshimiwa Shangazi ame-suggest. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nichukue tu fursa hii kumpongeza Mkurugenzi Mkuu na pamoja na Mwenyekiti wa Bodi kwa kazi nzuri sana ambayo wanaifanya na ninaomba nahisihii kwa kuwa shirika letu hili *Air Tanzania* halijaweza kusimama katika miguu yake miwili yenye we limefulufuwa tu majuzi bado lina mahitaji mengi tungeweza kusamehe baadhi ya tozo na hilo si geni *Ethiopia Airliner* kwa mfano hawalipi *landing fees*, hawalipi *parking fees*, wala hawalipi *navigation fees* na sisi tungewasamahe hawa kwa fees kama hizo kwa sababu kwa mwezi tu kwa aina hiyo kwa *calculation* zangu ina maana fees hiyo ni zaidi ya milioni 400.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni mzigzo sana hili shirika bado halijakua kiasi cha kutosha cha sisi kuanza sasa kuwanyonya. Kwa hiyo, kwa maana hiyo basi naomba Serikali iweze kufikiria jambo hili la kuweza kuwasamehe kodi za aina hiyo itapendeza sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nilitaka kulizungumzia leo ni kuhusiana na hifadhi ambayo ya Serengeti, asilimia yaani asilimia 90 ya hifadhi hii iko nchini kwetu Tanzania na asilimia 10 iko upande wa Kenya ambao wao wanaitwa Masai Mara. Sasa kwa ufupi katika sehemu Masai Mara peke yake wao wana *airfields* tatu za lami ambazo zina urefu zaidi wa kilometra 1.8, ambayo zinakuwa na uwezo sasa wa ndege aina ya *Bombardier Q4100*, kuweza kutua katika uwanja ule. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wanachokifanya watalii wanapofika katika uwanja wa kimataifa wa Nairobi ambao wanachukuliwa nchi tofauti huko nje ya nchi. Sasa Kenya Airways wanakuwa na kampuni tanzu, nafikiri *subsidiary company* ambayo inaitwa Jambo Jet, inachukua watalii inawapeleka moja kwa moja Masai Mara. Sasa pale wale watalii hawawi *inconvenient* hata kidogo, wanakuwa wanafurahia safari yao kwa sababu ni rahisi. Lakini kwa

mazingira hapa ya kwetu sehemu ambazo watalii wanaingia nchini ni Dar es Salaam, Kilimanjaro na Zanzibar, halafu wanakuja kwa makundi makubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa maana hiyo basi tungeweza kutengeza uwanja wetu wa ambaao uko katika sehemu ya Tanzania unaitwa Sereneira ambaao uwanja wenyewe una kilometra 2.2 ni mrefu kiasi cha kutosha, lakini unataka maboresho ili wale watalii ambaao wanatelemka Kilimanjaro au Zanzibar wapate fursa au waweze kuchukuliwa moja kwa moja na *Bombardier* ya *Air Tanzania* na kupeleka katika uwanja huu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufanya hivyo tutakuwa tumeusaidia uwanja wenyewe kupata mapato, lakini kwa Taifa kwa ujumla siyo watalii wote ambaao wanapenda kutelemka uwanja wa Kilimanjaro halafu wakachukua magari kuelekea katika sehemu husika, unakuwa unawasumbua kwa hali ya kutosha. Na hii ndiyo namna ambayo *Air Tanzania* ingeweza kushiriki moja kwa moja katika kukuza utalii kwa sababu unachukua watu unapeleka kule na wakimaliza shughuli zao wanapanda katika huo uwanja wa Sereneira wanarudi katika sehemu ya *Airport* kubwa ili waweze kuendelee na safari zao nchi ya nje. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ningeliomba hili sana upande wa Serikali uboreshwe uwanja ule na hautaki kazi kubwa, ni kuuweka tu *control tower* pale kwa sababu uwanja tayari upo mrefu ikiwa kama hali ya uchumi hairuhusu pengine si lazima lami kwa kipindi hichi unaweza ukaweka lami baadaYe ukauchonga katika namna ambayo ndege zinaweza kuteremka na kupaki kiurahisi. Hilo linawezekana kabisa nikuhakikishieni pato la Taifa litakuwa kabisa kwa kufanya hili jambo ambalo nail-suggest, halafu kingine... (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Muda wako umekwisha Mheshimiwa ahsante sana, Mheshimiwa Abbas umeongeza dakika tatu

za Mheshimiwa Mwita Getere, kwa hiyo, malizia hoja yako. (*Makof*)

MHE. CAPT. ABBAS ALI MWINYI: Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa la mwisho kuhusiana na hali ya *Air Tanzania* ambayo nilikuwa nataka kuizungumzia ni kwamba kwa ndege zetu, hazitumiki yani kuna *underutilization* na hizo hizo ndege hazitumiki ipasavyo naweza kusema kama vinatumika kama asilimia 60 *underutilization* ndiyo inavyofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hii inasababishwa na *factors* zingine kwa mfano viwanja vyetu vingi havina taa na kwa hali ya kawaida ndege haitakiwi kabisa isimame, wanaobadilishana ni Ma-crew lakini ndege inatakiwa ifanye wakati wote masaa 24 ikiwezekana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kutokana ukweli kwamba viwanja vyetu vichache tu vyenye huduma ya taa ndiyo maana sasa hatufikii ile kiwango cha matumizi ya ndege zilizokuwepo ya kutosha, lakin hii ni sababu moja. Nyingine ni sababu ya kibiashara ya kwanza unapowachukua watalii au watu wa nchi mbalimbali kwa maana ya wa hapa karibuni Malawi, au Lubumbashi kwa mfano ili kuwaleta Dar es Salaam lazima pengine wale wanabubiriwa sasa ndege nyingine ili waende nje, sasa kama hakuna ndege nyingine ambayo inawasubiri wale abiria ambao wanatoka katika nchi jirani inakuwa ni ngumu, hizo ndiyo sababu za kibiashara ndiyo maana ya kwanza tukawa asilimia 60 tu ya matumizi ya ile ndege ambayo tunayafanya ndiyo ambayo yanatokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja, ahsante. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Abbas Ally Mwinyi, Waheshimiwa Wabunge nadhani tunajifunza mambo mawili hapa, moja siyo lazima uchangia kwa kelele sana la pili ni kuchagua eneo moja ambalo unaweza ukachangia kikamilifu. Nimuite sasa Mhehsimiwa Boniphace Mwita Getere ambaye atachangia kwa dakika tano, atafuatiwa na

Mheshimiwa magdalena Sakaya dakika kumi, Mheshimiwa Oran Njeza ajiandae. (*Makofi*)

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia, nimpongeze Abbas alivyokuwa anachangia hapa vizuri zaidi amenikumbusha uwezo wa kawaida wa binadamu wa kufikiri ule unaitwa *argue* ni 100 na inaenda mpaka 150. Lakini wale wataalam wenye akili nyingi zaidi kama Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli wanaanza 170 mpaka 220 *argue*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tofauti yetu tulio wengi hapa Bungeni na Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli ni moja tu yeye *IQ* yake kwa kuwa ni kubwa anawaza Tanzania ya 2050 itakuwaje wakati huo huo sisi tunawaza lini tunakuja Bungeni kuendelea na maisha yetu ndiyo tofauti yetu. Kama unawaza kurudi Bungeni unaweza ukazungumza vitu rahisi rahisi vya kufurahisha watu ili uje Bungeni hapa kama unawaza nchi itakavyokuwa huko mbele maana yake ni kwamba unawaza mambo makubwa bila kujali itakuwaje, waanguke au usianguke, ndiyo Mheshimiw Rais Dkt. John Pombe Magufuli anafanya mambo kama hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshangaa kuna vitu vingine hapa vinakuwa kama mtu anakuja vibaya, au anakuja vizuri sasa tunaambiwa bwana nyie wa CCM sijui Wabunge tunawapa ushauri hamfuati, ushauri siyo agizo, ushauri kuna ushauri mzuri kuna *good advice* na kuna *bad advice*. Kwa hiyo, ushauri unaweza ukaufuata kama unaona kama unakufaa au haukuifai, ndiyo maana unaitwa ushauri. Tungefuata ushauri huo basi kulikuwa na lugha hapa mnajenga ndege za nini mnajenga reli za nini bandari sijui yameenda, lakini leo tunashauriwa leo nimeona hapa Mheshimiwa Silinde anashauri juu ya kuendeleza mapato ya ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ina maana amekubali ndege ni sahihi kuletwa hapa nchini. Kwa hiyo, tunakubaliana, leo tumeona watu wanashauri kujenga

bandari kavu, ambayo bandari kavu kujenga ni miezi mitatu, lakini kujenga reli ni zaidi ya mwaka mmoja miaka miwili. Kwa hiyo, tumeanza kile kikubwa tunakuja kwenye kile kidogo ili tuweze kwenda vizuri kwenye mambo yetu tunayoenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye barabara za Jimbo la Bunda na kwenye barabara za Mkoa wa Mara. Kuna barabara ya kutoka Nyamswa kwenda Bunda, Bunda kwenda Buramba, Buramba kwenda Kisolia, kuna barabara hiyo ipo toka mwaka 2000 mpaka leo haijajengwa amekuja Mheshimiwa Rais tarehe 4 alikuwa Kibara mwezi wa 9 tarehe 6 alikuwa kwenye Jimbo la Bunda ameagiza amefungua ujenzi wa hiyo barabara akaagiza nikitoka hapa kasi ya barabara hii iendeleee.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa ni miezi 9 sasa barabara hii haiendi, barabara ya Buramba kwenda Kisolia haiendi, barabara ya Nyamswa kuja Bunda haijatangwaza hata mkandarasi hajapitiaka, barabara ya makutano kule Sanzati bado inasua haiku vizuri, barabara ya kutoka Sangati kwenda Natamgumu bado iko vibaya. Sasa najiuliza sasa Wizara hii ya ujenzi na miundombinu kama kuna mtu alioa Mara halafu mke akamkimbia aje tumrudishie sasa shida iko wapi? Mbona sisi tunapata shida? Ukienda kwenye uwanja wa ndege tumeahidiwa mpaka leo haupo ukienda kwenye bandari haipo sasa ni nini kinatokea sasa kwenye Mkoa wa Mara kitu gani kinakuwepo? Tuna hasira sasa na mambo kama haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sasa Wizara ianze kuona Mheshimiwa Rais ametoa agizo la kujenga barabara hizo na kutangaza wakandarasi shida yetu iko wapi. Kweli tukafikiri kwamba watu waweze kujenga ili tuweze kuona kazi inaenda. Lakini vinginevyo uwanja wa ndege wa Musoma umepewa bilioni 10 na hautatolewa mpaka leo haujatolewa, Wizara hii ya Ujenzi kusema kweli nchi ni kubwa na wanafanya kazi nzuri niwapongeze kusema kweli, Mheshimiwa *Engineer Kamwelwe* naomba sasa naomba sasa ujitalidi ufanye kazi vizuri, Mheshimiwa *Engineer Nditiye*

umsaidie Mheshimiwa Kwandika nawe umsaidie na watendaji wote wa Wizara hii msaidiane nchi ni kubwa tusipoangalia sasa namna ya kupanga hivi vipande vyetu na keki yetu maeneo mengine yatakuwa, yataendelea kupata shida sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tuangalie kuangalia Mkoa wa Mara muuangalie, Mheshimiwa Rais ameusemea sana alipokuwa kule ndani na mwaka huu tuna maazimisho ya Mwalimu mwezi wa 10 tunataka zile barabara zipitike ili wageni watakavyokuja pale kutoka *South Africa* wawepo.

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Muda wako umeesha Mheshimiwa, kengele imeshagonga, ahsante sana.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika, dakika tatu hamna? (*Vicheko*)

NAIBU SPIKA: Hapana ameongezewa tu Mheshimiwa Abbas, wengine wanachangia kwa muda wao, Mheshimiwa Magdalena Sakaya atafuatiwa na Mheshimiwa Oran Njeza, Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete ajiandae.

MBUNGE FULANI: Haya kelele inakuja hiyo sasa.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ambayo iko mbele yetu. Pia nimshukuru Mungu pia kunipa kibali kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kwa ajili ya kuendelea kuwatumikia wananchi na kutumikia taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeweeka sera ya kuwasaidia kujenga uwezo kwa makandarasi wa ndani kwa maana ya kwamba zile barabara ambazo ziko chini ya

kilometra 30 wanapewa wakandarasi wa ndani ili kujenga uwezo wao, pia kuendelea kuenzi kazi zao za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa na tatizo kubwa sana la udhaifu mkubwa sana la utekelezaji wa kazi zinazofanywa na wakandarasi wa ndani. Na hapa ninasema kwamba hatuwachukuii wakandarasi wa ndani tunawapenda, lakini tunaangalia matatizo tuliyokuwa nayo pia miradi ambayo inapangwa iende kwa muda na kazi iende kwa muda unaotakiwa. Leo kazi ya mwaka mmoja inafanyika kwa miaka mitatu, wapo wakandarasi ambao kiukweli ni dhaifu uwezo ni mdogo na unapoambiwa kwamba washirikiane na wenzao pia wanakuwa ni wagumu, ninaomba Serikali ituambie tutaendelea kuwabeba wakandarasi wa aina hii mpaka lini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wantanzania wanapata shida mfano mmoja ni barabara Kaliua Urambo, kilometra 28 tu wamepewa wakandarasi wamepewa mwezi wa 4 mwaka 2017 ilikuwa ni kazi ya mwaka mmoja, leo ninapoongea na wewe na hapa Bungeni hata robo haijafika na wako *site*, na visingizio kila siku mara mvua, mara jua mara hiki ukienda pale kazi inayofanyika haieleweki, lakini wakati huo huo wenzao wa nje, wenzao wa *CHICO* walipewa kandarasi pamoja wamejenga barabara ya Neuya hapa kwenda Tabora kila siku wako kazini na kazi yao ni nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ituambie tutaendelea kuwabeba hawa wa ndani mpaka lini? Kama lengo ni kuwasaidia tunawatesa wananchi, tunawaonea wanachi. Kaliua ni Wilaya yenye uzalishaji kubwa sana asilimia 60 ya tumbaku yote Tanzania inatoka Kaliua mazao mengi mpunga, mahindi, karanga, lakini ukiona barabara ambavyo magari yanapita unaona huruma, pia Kaliua sasa hivi hatuna hospitali ya Wilaya, ukiona mtu akipewa rufaa akienda Tabora unamuonea huruma ile barabara jinsi ambavyo ni mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ituambie sasa baada ya mkandarasi wa pale barabara ya Kaliua

Urambo kuongezewa muda tena karibu mwaka mzima ni lini ile barabara itakamilika kwa kiwango kinachotakiwa? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara nyine ni barabara inayoungasha Mkoa wa Tabora, na Katavi pamoja Shinyanga, barabara inayoanzia Katavi inakuja Kaliua inakwenda Uliyankulu inakwenda mpaka Kahama, barabara hii ni barabara muhimu sana kwa uchumi na pia ni barabara kuu ni barabara ambayo iko kwenye *TANROADS*, lakini kuna kilometra 60 kutoka Kangeme kwenda mpaka kilometra 120 kwa maana ya mpakani haijaguswa wala kufunguliwa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atuambie ni lini sasa kile kipande cha kilometra 60 kutoka Kangeme, kwenda mpaka pale mpakani mwa Katavi itafunguliwa? Kilometra 60 zingine zimefunguliwa, lakini barabara hii ni lini sasa itatengezwa kwa kiwango cha lami sababu ni barabara ya uchumi, barabara kuu, barabara ya Mkoa kati ya Mkoa na Mkoa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la barabara zilizopo pale Kaliua Mjini ahadi Mheshimiwa Rais ambaye alituahidi wakati uchaguzi, pia ameahidi 2017 alifanya ziara Kaliua kwamba kilometra saba za pale Mjini zijengwe na aliagiza kwa haraka mpaka leo barabara hizo bado hazijajengwa.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa waziri atakapokuja ku-*windup* atuambie barabara za pale kilometra saba za pale Mjini zitajengwa lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala la mitando, maeneo mengi ya Kaliua tena maeneo ambayo yana uchumi mkubwa wa kilimo hayana mawasiliano ya simu hivi tunayoongea kuna watu wanapanda kwenye mti ili aongee hata aseme shida yake apande juu ya mti aongee ndiyo Mhehimiwa Mbunge aweze kupata shida yake. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuambiwe maeneo mbalimbali ya Kaliua yatapata mitandao ya simu lini? Mheshimiwa Waziri nimezungumza sana kwa habari ya maeneo haya, maeneo ya Pandamloka ambapo mchele mwiningi unaolimwa Kahama unapatikana Pandamloka, hakuna mawasiliano ya simu, Pandamloka, Mwahalaja, Kombe, Shela, Maboha, Luenjomtoni, Usinga, Ukumbi Kakonko, Mkuyuni, Mpilipili, Igombe maeneo yote haya ni muhimu kwa uchumi, yanalima sana lakini kwa miaka yote kiukweli wanateseka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana maeneo haya yaingie kwenye bajeti. Naomba tuambiwe sasa ni lini minara itajengwa maeneo yale ili wananchi wa Kaliua ambao wanalima sana, wanachi wa maeneo mengi ya nchi hili waweze kupata mawasiliano na waweze kuwa na huduma nyingine kama wananchi wengine? (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii. Ahsante sana. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Oran Njeza atafuatiwa na Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete na Mheshimiwa Deo Ngala wa ajiandae.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kupata hii nafasi ya kucahngia hii Wizara muhimu ya miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Eng. Kamwelwe, Manaibu Waziri, *Engineer Nditiye* na Naibu wake, *CPA* Kwandikwa kwa kazi nzuri walioyoifanya pamoja na Makatibu wao Wakuu. Kwa kweli wanafanya kazi nzuri, hata ukiangalia hii bajeti waliyopewa nafikiri wanastahili, nasi wachukue maoni yetu waweze kuboresha zaidi sekta hii ambayo ni mtambuka ambayo kwa kiasi kikubwa itatusaidia hata kuboresha kilimo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru vilevile kwa ziara aliyoifanya Mheshimiwa Rais katika Mkoa wetu wa Mbeya na mengi aliyoayazungumzia ni pamoja na miundombinu ya barabara. Napenda kumkumbusha Mheshimiwa Waziri kuwa katika ahadi aliyoifanya siku ile, siku ya mwisho ilikuwa ni ujenzi wa barabara ya Mbalizi - Shigamba mpaka Isongole. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii barabara ni muhimu sana kwa vile inapitia kwenye maeneo ambayo ni ya kilimo cha mazao yanayotuletea pesa za kigeni; kahawa, pareto, viazi na pia kwenye mazao ya mbao. Vile vile hii barabara inatuunganisha na wenzetu wa Malawi na vilevile inapita kwenye bonde la Mto Songwe ambao ni ubia wa Serikali yetu ya Tanzania na Serikali ya Malawi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri aangalle kwani wananchi wanasubiri sana hii ahadi yake ikiwa ni pamoja na barabara ya Isonje - Kikondo na barabara ya Mbalizi - Chang'ombe kwenda Makongorosi. Hizi ni barabara muhimu sana. Kwa hiyo, nilipenda niliweke hili mwanzoni ili wasije wakajisahau kwa vile hizi ni ahadi za Marais waliotangulia na Rais wetu kasisitiza kwamba hii barabara ijengwe kwa kiwango cha lami. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda vilevile nichangie reli yetu ya TAZARA. Tunapoangalia ujenzi wa kuimarishe miundombinu ya reli ya nchi hii, naomba Wizara isije ikasahau miundombinu ya TAZARA. Reli ya TAZARA uwezo wake ni wa kubeba mizigo isiyopungua *metric tonnes* milioni tano, lakini mpaka leo hii nilikuwa naangalia *reportya* Mheshimiwa Waziri hapa, kwa mwaka 2018 na mwaka 2017 ni wastani wa *metric tonnes* 150,000 tu. Sasa hii ni chini ya asilimia tatu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia uwezo wa TAZARA; na hii reli ni ya kimkakati, bila hii reli, mizigo mingi ambayo inakwenda kwenye nchi za Zambia, DRC, Malawi na kwa kiasi fulani nchi ya Zimbabwe, hatutakuwa katika ushindani mzuri. Sasa hivi ushindani mkubwa wa Bandari yetu

ya Dar es Salaam ni Bandari za Msumbiji, Bandari za Angola na Bandari za *South Africa*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naangalia Bandari moja tu ya Msumbiji inaitwa Nakal ambayo wakilinganisha na gharama yake na Bandari yetu ya Dar es Salaam wao wako chini kwa asilimia 40. Sasa bila kuiboresha *TAZARA* na tukategemea hii mizigo iendelee kupitia kwenye barabara, sisi tutaondoka kwenye hiyo biashata na tutajikuta badala ya ku-*create value* ya bandari yetu lakini kwa kupitia *TAZARA*, tutakuwa tunafanya *value evaporation*. (*Makof*)

MBUNGE FULANI: Hongera sana.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vilevile kwa sababu hii reli ni ya ubia kati ya Zambia na Tanzania, inaelekea wenzetu wa Zambia hawana tena umuhimu na hii reli. Nguvu wamezipeleka kwenye hizo nchi nyingine nilizozitaja na wanaona kuna manufaa zaidi ya kutumia hizo bandari nyingine kuliko hii reli yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri Wizara na Serikali iangalie ni namna gani kuangalia upya huo mkataba tulionao kwa sababu hadi leo tunashindwa hata kuchukua pesa ambazo Serikali ya China iko tayari kutukopesha. Kwenye Itifaki Na. 16 nimeona kwenye *report* hapa bado tunaendelea, tunaangalia namna ya kuharakisha lakini miaka inaenda, hata kukopa tu hizi pesa nayo bado imekuwa kwenye mkakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nimeona kwenye *report* ya Kamati, deni la wafanyakazi ni shilingi bilioni 434, hizo ni pesa nyingi sana. Siamini kama kweli hili deni kubwa namna hii kama ni la wafanyakazi tu na zimehakikiwa na hazijalipwa.

Je, hii *TAZARA* itakuwa hai au imefilisika? Kwa sababu kama deni halijalipwa shilingi bilioni 434 ni la wafanyakazi, limehakikiwa toka 2016, leo 2019 hazijalipwa na ninaamini kwamba wafanyakazi wengi wa *TAZARA* wako katika umri

wa kustaafu. Je, mkakati gani ambao unachukuliwa kuhakikisha kuwa tunaajiri wafanyakazi wapya wa reli hii? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na reli hii, ili ifanye kazi vizuri tunahitaji tuwe na Bandari Kavu pale Mbeya na vilevile tuwe na reli ya kutoka Mbeya -Inyala kwenda Kyela ili iwe kiungo cha Nchi ya Malawi, Msumbiji pamoja Zimbabwe na tuweze kutumia vizuri zile meli zetu tatu ambazo ziko kwenye Ziwa Nyasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni muhimu sana. Hata ukiangalia katika maandiko ya nchi majirani na maandiko ya Kimataifa, zinaonyesha ni kiasi gani tutapoteza biashara ya *TAZARA* kwa nchi majirani kwa sababu reli ya *TAZARA* ilikuwa muhimu wakati ule wa ukombozi. Leo nchi zile zimeshakombolewa, nazo ndiyo zinafanya mikakati ya kuhakikisha kuwa watatunyang'anya biashara zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na *TAZARA*, lakini vilevile napenda kuongelea kwa kifupi sana barabara zetu nyingine za Mkoa wa Mbeya ikiwemo barabara ya *bypass* na upanuzi wa barabara ya kutoka Tunduma kuja mpaka Igawa. Hizi barabara ni muhimu sana kwa ajili ya uchumi wetu. Gharama kubwa za kilimo zinachukuliwa na gharama za usafirishaji ikiwemo usafirishaji wa mbolea na usafirishaji wa mazao yetu.

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Muda umekwisha Mheshimiwa. Kengele ya pili imeshagonga.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Ngalawa na Mheshimiwa Zitto Zuberi Kabwe ajiandae.

MHE. FREDY A. MWAKIBETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa nami niweze kuchangia katika Wizara hii ya Ujenzi, Uchukizi na Mawasiliano. Kabla sijachangia, napenda kwanza nimshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingsi wa rehema ambaye ametupa uzima hata kuwepo siku hii ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano katika nchi nyingine na hata nchi yetu ya Tanzania ni muhimu sana kwa uchumi wetu wa Tanzania. Pia nianze kwa kumpongeza na kuwashukuru sana Mawaziri, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu pamoja na Manaibu Katibu Wakuu wote katika Wizara hii ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze mchango wangu kwanza kwa kuzungumzia suala la barabara ambayo nimekuwa nikizungumza humu Bungeni kwa muda mrefu, barabara ya Katumba – Lwangwa – Mbambo yenye urefu wa kilometra 83 na hii barabara ni mkombozi mkubwa sana kwa Jimbo langu la Busokelo pamoja na Majimbo jirani ikiwemo Kyela pamoja na Rungwe. Ni barabara pekee ambayo imeandikwa kwenye Ilani ya Chama chetu cha Mapinduzi kwa zaidi ya vitabu vitatu. Iliandikwa 2005, ikaandikwa 2010, iliandikwa 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana kipekee Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hivi karibuni tarehe 29 mwezi huu wa Tano alitembelea Halmashauri yetu ya Busokelo na kuahidi tena; na kuagiza Wizara kwamba sasa hii barabara itengenezwe kwa kiwango cha lami kwa kilomita zote 81.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Busokelo tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais na wewe Mheshimiwa Naibu Spika ulikuwepo, ulishuhudia hali ya hewa ilivyokuwa, mvua zilikuwa ni nyingi na umuhimu wa barabara hii, kwa maana wananchi wote wanategemea barabara hii kwa sababu kule tuna viwanda vya chai, tuna viwanda mbalimbali ikiwemo gesi asilia (*carbondioxide*) lakini

tunazalisha mazao ya kila aina, kwa sababu msimu wa mvua ni zaidi ya milimita 2000 kwa mwaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na barabara hiyo, kuna barabara nyingine ambayo inaunganisha Jimbo langu la Busokelo na Mkoa wa Njombe kuititia Makete na barabara hii nakumbuka mwaka 2018 Mheshimiwa Naibu Waziri, Eng. Kwandikwa alikuwa amekubali kwamba ataunga juhudhi za wananchi wale kulima kwa jembe la mkono, lakini kwa bahati mbaya naona hakupata fursa hiyo. Naamini alikubali ili aiweke kwenye Bajeti ya Serikali ili sasa iweze nayo kuwa katika mpango mzima wa Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, cha ajabu, bado sijaiona kwenye kitabu chetu hiki na ninaamini atakapokuja ku-*wind up* basi atakumbuka ile ahadi lakini na namna ambavyo wananchi wale walimwomba alivyokuja kutembelea ile barabara ya Mwakaleli mpaka kule Kandete. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na suala la barabara kuna jambo zima la miundombinu hasa upande wa uwanja wa Songwe wa Kimataifa. Uwanja huu shida kubwa na changamoto kubwa iliyopo pale ni suala la taa za kuongozea ndege. Nimeona kwenye kitabu hiki wameweka shilingi bilioni tatu kwa ajili ya kumalizia jengo la abiria pamoja na kuweka taa za kuongozea ndege wakati wa usiku na wakati wa mchana hasa wakati wa ukungu kipindi kama hiki, kwamba Mkoa wetu wa Mbeya mara nyingi unakuwa na shida ya ukungu muda mrefu. Kwa hiyo, ndege zinapata wakati mgumu kutua kipindi kama hiki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka mwaka 2018 pia mliweka kwenye bajeti haikutekelezeka, mwaka juzi iliwekwa haikutekelezeka. Naomba sana, hii shilingi bilioni 3.6 ambayo imewekwa sasa iweze kutekelezeka katika kipindi hiki. Nakumbuka mwaka huu alipokuja Mheshimiwa Rais kuzindua Kiwanda cha Maparachichi (*Avocado Company*) ambacho ni mkombozi mkubwa sana kwa wakulima wa Mkoa wa Mbeya pamoja na Wilaya ya Rungwe kwa ujumla, lakini maparachichi yale yanasa firishwa kwa njia ya malori

mpaka Dar es Salaam ili yaweze kusafirishwa kwenda nje ya nchi. Siyo hivyo tu, yanasaferishwa mpaka Mombasa kwa sababu uwanja wetu wa Kimataifa wa Songwe hauna vigezo vyta kufanya ndege za mizigo ziweze kutua pale. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kukamilika kwa kiwanja hiki cha Songwe kitafungua malango mengi sana ya fursa za kiuchumi kwa Mikoa ya Nyanda za juu Kusini lakini pamoja na Nchi za SADC kwa maana ya zilizo chini ya jangwa la Sahara na nchi jirani. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna suala zima la hizi hizi ndege ambazo sasa hivi tunapanda, wenzetu wanasesma pengine hazina faida kwa sasa, lakini kawaida sekta moja inaweza ikawa na *multiplier effect* kwa sekta nyingine. Kwa hiyo, uchumi hauwezi kubadilika kwa sasa mara moja, pengine baada ya miaka mitano, 10, 20, 30 ndipo tutakapoona umuhimu wa hizi ndege. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara kwamba ikifungua malango kwa kufungua njia nyingine mpya za *route* kutoka hapa Dodoma kwenda Mbeya pamoja na Nyanda nyingine za juu Kusini ili mtu atoke Mbeya moja kwa moja kuja Dodoma na atoke Dodoma aende Dar es Salaam na maeneo mengine, lakini sasa hivi maana yake inakulazimu uende Dar es Salaam, uende Iringa *then* uende Mbeya ama utoke Dodoma uende Dar es Salaam *then* uende Mbeya moja kwa moja. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka nizungumzie ni...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Muda wako umekwisha Mheshimiwa. Ahsante sana.

MHE. FREDY A. MWAKIBETE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante Sana. Mheshimiwa Deo Ngalawa atafuatiwa na Mheshimiwa Zitto Kabwe na Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah ajilanda.

MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuongea na kuchangia hotuba. Kwanza naipongeza Serikali kwa kazi nzuri ambazo inazifanya hususan maeneo yetu ambako tunatoka. Kwa hiyo, nashukuru. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuishukuru Serikali hasa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Eng. Kamwelwe, Waziri wetu na Manaibu wake pia Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara nzima, nianze kuiongelea barabara ya Itoni – Njombe – Ludewa – Manda. Barabara hii imewekwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi na barabara hii kwa kweli ina urefu wa kilometra 211.6 mpaka kufika kule Manda. Itajengwa katika *lots nne* na kwa sasa imeanza ujenzi wa *lot* Na. 2, Lusitu - Mawengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii, hivi tunavyoongea toka ilipoanza kujengwa ilipaswa iwe imeisha lakini mpaka sasa barabara hii haijaisha. Kwa hiyo, naiomba Serikali sasa ijaribu kufanya jitihada za haraka ili kipande hiki korofii kiishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna eneo la Lusitu kwenda pale Itoni, *lot* Na. 1, kwa kweli kipande hiki kinasumbua sana. Hivi ninavyozungumza, malori mengi sana yamekwama kwenye maeneo ya Njombole kule, maeneo ya Luponde na kusababisha adha kubwa ya usafiri mpaka ikapelekea wiki iliyopita baadhi ya wenye magari kutokupeleka magari Ludewa kwa sababu ya adha hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba sasa Serikali angalau itufikirie kwa kipande cha kutoka Itoni kwenda Lusitu na wakati huo huo ile barabara ya Mawengi - Lusitu ikifanyiwa jitihada kubwa. Kwa sababu nakumbuka Mheshimiwa Waziri alikuja mwezi wa Nane akaona na akatoa

maagizo, lakini inaonekana kama yale maagizo hayakufanyiwa kazi kabisa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuipongeza Serikali kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya kutoka Mkiu – Liganga – Madaba na ule wa kutoka Mchuchuma kwenda Liganga. Kwa kweli barabara hizi ni muhimu, upembuzi umefanyika. Sasa naiomba Serikali iweke jitihada kubwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa lami ya barabara hizi kwa sababu barabara hizi ndiyo zinakwenda kwenye ile miradi ambayo tunaita ni *flagship projects* ya Liganga na Mchuchuma. Kwa hiyo, naiomba Serikali ifanye jitihada za haraka kwa sababu ya umuhimu wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naishukuru Serikali kwa kuiweka kwenye mpango wake wa Bajeti wa kuifungua barabara inayopita kando kando ya Ziwa Nyasa; barabara kutoka Lupingu – Makonde - Lumbila mpaka Matema. Kwa hiyo, naiomba Serikali sasa iweke misisitizo mkubwa kwa sababu eneo hili la Ziwa Nyasa ni eneo la Kitalii na pia ni eneo la kiulinzi na usalama. Kwa hiyo, ninaamini kwamba kazi hii mtaifanya na mtaifanya kwa kutumia nguvu kubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie daraja la Mto Ruhuhu. Daraja la Mto Ruhuhu lilipaswa liishe toka mwaka 2017, lakini mpaka leo hii daraja hili halijaisha na daraja hili lipo kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, tunaomba basi mwaka huu hili daraja likamilike ili lipitishe wananchi ambao wanatoka Ludewa kuelekea kule Nyasa, kwa sababu kwa mwaka 2018 tu, tayari wananchi zaidi ya watano wameliwa na mamba kwenye mto huu huu kwa sababu ya kutokuwepo kwa daraja pale. watu wanapita kwa mitumbwi na wakati mwingine hata ile Panton iliyopo pale inakuwa haifanyi kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali na kusisitizia kwamba ikiwezekana hili daraja liishe mwaka huu kama ambavyo Mheshimiwa Waziri ameniahidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuipongeza Mamlaka ya Bandari Tanzania kwa kazi inayofanya kule Ziwa Nyasa. Tumeona Mheshimiwa Nditiye akiwepo pale na bahati nzuri na Mkurugenzi Mkuu wa Bandari tumekuwa tukiwasiliana mara kwa mara. Kwa hiyo, nashukuru kwa kunipa tu vile vituo vyta kupakia na kupakua abiria na mizigo ili kuweza kuwarahisishia wale wananchi wanaoishi Kanda ile, usafiri wa kutoka eneo moja kwenda eneo lingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kushukuru Wizara kwa ajili ya minara ya mawasiliano ya simu. Minara hii tayari imeshajengwa na iliweza kuwaka kwa siku tatu tu lakini mpaka sasa hivi imezima. (*Makofi*)

Kwa hiyo naomba sasa Wizara kuptitia mawasiliano kwa wote, kazi waliyoifanya ni kubwa na kazi waliyoifanya ni nzuri, niwapongeze na nimpongeze Mheshimiwa *Engineer Ulanga* na timu yake yote na nimpongeze Mheshimiwa *Waziri*, kazi hii ni njema lakini wale watu wanasubiri kwa kiasi kikubwa mawasiliano kwa sababu mawasiliano yamekuwa ni tatizo kubwa kwao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niongelee kidogo *7TCL* ni Shirika letu, Shirika la nchi na la umma, kuna haja ya kuweka utaratibu mzuri ili iweze kushindana na taasisi nyininge hasa kwenye eneo la manunuzi. Manunuzi inavyoonesha kwamba inachukua muda mrefu kiasi ambacho hawawezi ku-compete na wenzao. Wenzao wao *private sectors* wao wanafanya mambo yao kiurahisi, kwa hiyo kuna haja ya Serikali sasa kuipa uwezo wa kuijendesha yenywewe na hizi sheria za manunuzi tuweze kuzirekebisha ili hilli shirika liweze kuijendesha vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Zitto Kabwe atafuatiwa na Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah na Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula ajiandae.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii. Nina mambo mawili tu ya kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ni mambo ya jimboni; napenda nitoe shukrani za dhati kwa Mamlaka ya Bandari Tanzania kwa miradi ambayo imeanza kuifanya katika Mkoa wa Kigoma katika Manispaa ya Kigoma Ujiji, Bandari ya Ujiji, Bandari ya Kibirizi na Bandari ya Nchi Kavu ya Katosho. Bandari ya Nchi Kavu ya Katosho umuhimu wake ni kuhakikisha kwamba Kigoma inakuwa ni kituo cha biashara kama ambavyo imekuwa siku zote kwamba eneo la Ujiji na Kigoma ni eneo la biashara la Maziwa Makuu na hivyo kuwezesha mizigo ambayo inatoka Bandari ya Dar es Salaam kwenda Burundi au kwenda Mashariki ya Congo upande wa Kaskazini ya Mashariki ya Congo watu waweze kuichukua pale Kigoma, kuifanya Kigoma ni *plot of destination. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Mamlaka ya Bandari kwa kazi hizi ambazo wanaendelea kuzifanya na maeneo mengine nimeona bajeti wamepanga ya shilingi bilioni 548 kwa ajili ya miradi mbalimbali ya Mamlaka ya Bandari nchi nzima, ni kazi ambayo ni nzuri kwa sababu maendeleo yake yanaendana na maendeleo ya jumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, niombe Wizara itupatie majibu ni kwa nini kama jinsi alivyoongea Mheshimiwa Nsanzugwanko jana, ni kwa nini Mradi wa Uwanja wa Ndege wa Kigoma unazidi kucheleshwa? Tunafahamu kwamba manunuzi yameshakamilika toka mwezi Januari, 2018, sasa hivi ni mwezi Mei, 2019, hatujaona chochote ambacho kinafanyika katika Uwanja wa Ndege wa Kigoma, viwanja vingine tunaona vikijengwa, vingine vipya havikuwepo kabisa vinajengwa, kwa nini mradi ambaao tayari una fedha kutoka *European Investment Bank* unaendelea kucheleweshwa mpaka sasa hivi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, tuna mradi mkubwa sana wa takribani dola milioni 40 wa upanuzi wa Bandari ya

Kigoma ambao unafadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Japan (*JICA*). Juzi niliona Mheshimiwa Waziri wa Fedha akiwa amezungumza na watu wa *JICA* alivyokuwa kule Washington, lakini mpaka sasa hatujaona taarifa yoyote ile kuhusiana na mradi huu wa Kigoma. Nilivyo fuatilia niliambiwa kwamba kuna masuala ya kikodi na kadhalika, nadhani kuna haja ya Serikali kuweza kuona vitu ambavyo msaada huu kutoka Japan wanaomba viingie bila kulipia kodi kama faida yake ni kubwa kuliko mradi wenyewe kwa ujumla wake, kwa sababu kuingiza dola milioni 40 katika Mji wa Kigoma kwa ajili ya ujenzi wa Bandari ya Kigoma nadhani una faida kubwa zaidi kuliko *VAT* ambayo wanaomba iwe *exempted* kwa ajili ya kuingiza vifaa vyao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naamini kabisa kwamba Wizara na hasa Wizara ya Fedha na Mheshimiwa Waziri Mpango yupo hapa, watahakikisha jambo hili linakamilika sababu mwezi huu Mei ultakiwa mradi uwe umeanza, mpaka sasa Wizara ya Fedha bado haijasaini mkataba na *JICA* kwa ajili ya mradi huu, zabuni zitangazwe ili uweze kuanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa lingine ni suala la kinchi la kiujumla. Mheshimiwa Silinde amezungumza hapa, toka tumeanza Awamu ya Tano fedha ambazo tumeziingiza Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ni asilimia 46 ya bajeti yote ya maendeleo ya nchi yetu. Jumla ya fedha ambazo tumeziingiza Wizara hii ni trilioni 18.7 na fedha ambazo za ujumla za bajeti ya maendeleo ya nchi ni trilioni 40.6. Kwa hiyo *46 percent* ya bajeti ya maendeleo anaishika Mheshimiwa Kamwelwe na Manaibu wake wawili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wana haki ya kuuliza kiasi hiki cha fedha ambacho tumekiingiza mpaka sasa kimezalisha viwanda vingapi? Kwa sababu tunazungumza kuhusu *forward and backward linkages*, tunazungumza kuhusu namna gani ambavyo fedha tunazoingiza kwenye miradi kama reli, miradi kama ndege ni namna gani ambazo zinachochea sekta nyingine za uchumi. Kwa hiyo, tungepata maelezo ya Serikali hapa

kwamba tumeingiza triliuni 18.7, nini *multiplier effect* ya hili na Mheshimiwa Waziri Mpango analijua vizuri sana. Moja ya seka ambayo ina-*multiplier effect* kubwa ni *construction* seka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini sisi ambao tunaingiza fedha nyingi namna hii bado kasi ya ukuaji wa uchumi iwe ni ndogo, leo hii tunabishania makisio ambayo haya *IMF* wameyatoa ya *four percent* na kadhalika, *IMF* Mheshimiwa Waziri Mpango hawajakanusha kuhusu makisio hayo, wamekanusha *ripped report* lakini makisio ni yale yale, lakini hata usipochukua makisio ya *IMF* chukua makisio ya Serikali ya *six percent before* Serikali ya Awamu ya Tano kuingia madarakani *economy* yetu ilikuwa inakua kwa *seven percent for 10 years*. Serikali ya Awamu ya Tano imeingia madarakani 18 *trillion shillings* zimeingizwa kwenye *construction sector, growth rate* iko chini kwa nini? Haya ndio masuala ambayo Wabunge tunapaswa kuiuliza Serikali, (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kenya wamejenga ile *SGR* ya mkopo wenyewe ghari sana na wote tunajua, lakini mchango wa ujenzi *building construction* kwenye *growth rate* ilikuwa *1.5 percent*, iweje sisi warithi *growth rate* ya *seven percent* halafu ndani ya miaka mitatu baada ya *ku-inject all the money* tushuke, nimesema waachane na *four percent* ya *IMF*, waende na *six percent* ya Serikali, *why?* Ni kwa sababu utekelezaji wetu wa mipango ya maendeleo ya miundombinu ni utekelezaji unaotoa fedha kwenda nje, hauingizi ndani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana mzunguko wa fedha ni mdogo sana kwa sababu wamewapa kazi wakandarasi wa nje, wanaagiza *raw materials* kutoka nje, *every single cent amount* ya nchi yetu inapelekwa nje, wanakusanya kodi kwa muuza nyanya, wanaenda kumlipa Mturuki anapeleka Uturuki, ndio maana uchumi haukui. Hata wajenge *argument* namna gani. Nimeona *argument* ya Serikali kwenda *IMF* kusema makisio haya ni makosa kwa sababu tuna miradi mikubwa, tuna *Stiegler's*

Gorge, argumentile haina maana kwa sababu all the money zinaenda nje na debt service yetu, huduma yetu ya Deni la Taifa ni kubwa... (Makof)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zitto kuna taarifa hapo, Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

TAARIFA

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Zitto, hapa nimeshika takwimu rasmi za Pato la Taifa na ukuaji wake kwa mwaka 2018 ambayo ipo bayana. *Growth rate* mwaka 2013 ilikuwa asilimia 6.8; mwaka 2014 ilikuwa asilimia 6.7; mwaka 2015 ilikuwa asilimia 6.2; mwaka 2016 asilimia 6.9; mwaka 2017 asilimia 6.8; na mwaka 2018 asilimia 6.9. Mheshimiwa Zitto hiyo *growth rate* iliyoteremka ni ipi? Kwa nini wanatumia taarifa za IMF ambazo hazina ukweli na bado niliwaambia katika Bunge hili kwamba bado tunazungumza, *African Development Bank* wana *project* uchumi wa Tanzania mwaka 2019 utakuwa asilimia 6.8, *estimate* ya *World Bank* asilimia 6.6, sasa hiyo *growth rate* iliyoteremka ndugu yangu ni ipi? Pokea taarifa. (Makof)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zitto, unaipokea taarifa ya Mheshimiwa Mpango?

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea taarifa ya Mheshimiwa Waziri Mpango. Ninachotaka kumwambia Mheshimiwa Waziri Mpango kwanza anajua kwamba mamlaka ya *economic surveillance* ya dunia ni moja, ni IMF na anafahamu kwa sababu amefanya kazi huko, Benki ya Dunia, *African Development Bank* na hata Wizara yetu ya Fedha makisio wanayoyatumia ni makisio ya IMF, sio makisio mengine yoyote na anafahamu, labda atakataa kwa sababu lazima a-defend Serikali hapa, lakini najua anafahamu hivyo. Hata hivyo, *point* yangu ni kwamba, wastani wa over a decade thus why tulikuwa sisi ni the fastest growing economy, wastani wa over a decade ni seven percent, sawa we can debate about that... (Makof)

NAIBU SPIKA: Nashauri Waheshimiwa Wabunge ongeeni huku ili iwarahisishie kwenda na mazungumzo mnayotaka kuzungumza, mkianza kutazama wenyewe huko ndio hayo mnaanza kujibizana wenyewe, zungumza na mimi huku ili usipate wakati mgumu kuona mtu amekataa jambo lako.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Naomba nichukue takwimu za Mheshimiwa Waziri Mpango, ye ye ni mchumi anajua, panapokuwa na *depression*, panapokuwa na m dororo wote wa uchumi kwa kutumia *fiscal Policy* Serikali ina-pump in money kwa ajili ya kuchochaea uchumi, over the last three years, tume-pump 18.7 trillion kwenye construction. Naomba nijibiwe, hii fedha ambayo tumei-pump tumezalisha viwanda vingapi, tumezalisha ajira za kudumu ngapi, sekta ya kilimo imechochewa namna gani, ndio maana ya *multiplier effect* na ndio swalilangu hili na wakati mwingine tunapozungumza wala hatuna nia mbaya, nia yetu ni kuhakikisha kwamba tunakwenda pamoja as a country, hakuna mtu ambaye hataki nchi yake iendelee, so there is no haja ya kuwa defensive. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba utekelezaji wa sera za kiuchumi wa nchi yetu over the last four years ni utekelezaji mbovu, ni utekelezaji fyongo, ndio maana pumping in of money, 20 percent ya development budget tunayoiingiza, haichochei uchumi inavyotakiwa.

TAARIFA

NAIBU SPIKA: Kuna taarifa nyingine Mheshimiwa Zitto kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Ashatu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Zitto, naamini na ye ye ni Mchumi aliyeiva kama Mheshimiwa Waziri wa Fedha na anafahamu unapopeleka fedha kwenye sekta hii ya ujenzi athari yake sio ya muda mfupi, hilo la kwanza atambue. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sekta zilizochangia ukuaji wa uchumi aliousema Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa mwaka 2018, sekta ya ujenzi ni sekta ya pili iliyochangia ukuaji wa uchumi wa 6.9. Kwa hiyo aache kuwapotosha Watanzania mchango wa sekta ya ujenzi unaonekana na ni asilimia 12.9 sekta ya ujenzi imechangia kwenye ukuaji wa uchumi kwa mwaka 2018. Kwa hiyo, Mheshimiwa Zitto alitambue hilo. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zitto, unapokea taarifa hiyo?

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, sipokei taarifa ya dada yangu na namtakia mfungo mwema wa mwezi wa Ramadhani na ajiepusha sana kutumia maneno kupotosha kwa sababu mimi siwezi kutumia hayo dhidi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tofauti kubwa sana kati ya kasi ya ukuaji wa uchumi na uchumi. Sekta ya ujenzi ni ya pili kwenye kasi ya ukuaji, sio ya pili kwenye uchangiaji wa uchumi. Sekta ya ujenzi inachangia kidogo sana kwenye uchumi, ni ya pili kwenye ukuaji, *we have to pump in all this money*, lakini huo wa pili wake hauonekani kwenye uchumi wa ujumla wake na ndio *argument* yangu, kwamba *almost halfmama ya development budget.* (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ongea na kiti mwache Mheshimiwa Dkt. Ashatu.

MHE KABWE. Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, nusu ya fedha zako za maendeleo unaziingiza kwenye sekta moja, Wizara moja unapaswa uone namna ambavyo sekta zingine zimeinuliwa na ndio maana maswali hapa nimeuliza. Serikali ije kutujibu hii *investment* ambayo tumefanya imezalisha viwanda vingapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, *construction sector impact* yake sio *long term* inaanza na *short term*, mfano mzuri, anaweza akawa ni kijana anatengeneza screw za ujenzi wa

reli, akapata kazi, *screw* tu ni moja ya kiwanda ambacho kinaweza kikatengeneza wakati huo na akiendelea maana yake wawe wamefanya *transfer of technology*, wameajiri, wame-train ataendelea na ile kazi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachokiomba, muundo wetu wa mipango ya kiuchumi na utekelezaji wa miradi yetu iangalie *backward and forwarding linkages* ili fedha ambayo tunaiingiza *public investment* ambayo tunaifanya iweze kuwa na faida zaidi kwa nchi yetu kwa ujumla wake. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie mambo mawili...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Kengele ilishagonga, ahsante sana.

Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, lakini kabla ajaanza kuzungumza Mheshimiwa Munde ili taarifa zikae vizuri na waandishi wazipate vizuri maana ndio yale tena yanaanza taarifa zinatoka sio sawasawa. *IMF* iliyokataa na hiyo barua maana yake imeikataa na taarifa iliyotoka kabla haijatoka taarifa rasmi. Kwa hiyo, ni lazima hata waandishi wetu waelewe wanapopeleka taarifa hiyo nje, wamekataa taarifa iliyotoka ambayo siyo rasmi ikiwa ni pamoja na hiyo asilimia.

Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah atafutiwa na Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula na Mheshimiwa Shaban Shekilindi ajiandae. (*Makof!*)

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia Wizara ya Miundombinu. Umesema leo tujifunze kwa Mheshimiwa Abbas kutokupiga kelele, tunasikika tu, ngoja nianze kujaribu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe pongezi zangu za dhati kwa Serikali na Wizara nzima ya Ujenzi pamoja na miundombinu, Mheshimiwa Waziri, Manaibu Waziri,

Mheshimiwa Nditiye na kaka yangu Mheshimiwa Kwandikwa, tunawapongeza sana kwa kazi nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizipongeze pia taasisi zote zilizo chini ya Wizara hii *TPA, SUMATRA, TCRA, RAILWAY, TANROADS, TCAA, TASAC, CATCO, ATCL, UCSAF* na zingine zote, kwa kweli wanafanya kazi vizuri sana. Nimeingia kwenye Kamati hii ya Miundombinu muda mfupi tu, nimeona kwa kweli kazi inayofanyika ni nzuri na ni kubwa, tunawapongeza sana na tunataka waendelee kumuungu mkono Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuchangia naomba niongee kidogo kuhusu mdogo wangu Mheshimiwa Makamba, jana alichangia akasema kwa nini Serikali imehamisha kitengo cha Wizara kinachohusika na ununuzi wa ndege na kukipeleka Ikulu, wanaficha nini. Naomba tu nimwambie hayupo lakini najua taarifa atazipata kwamba Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kikatiba anayo mamlaka ya kuhamisha Wizara yoyote, kuhamisha Taasisi yoyote ya Serikali, kuipeleka popote anapotaka yeye. Anayo mamlaka ya kuanzisha leo mkoa mpya na kesho kuuvunja, anayo Mamlaka ya kumteua Waziri na kesho kumtumbua na anayo Mamlaka ya kuteuza Katibu Mkuu na kesho kuondoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kama wanaona kwamba Mheshimiwa Rais alihamisha ile taasisi kwa kuficha kitu sidhani kama wanawaza vizuri, nadhani saa nydingine wanaropoka au wamechanganyikiwa, wakijua kabisa kama Mheshimiwa Makamba anajua kabisa Katiba ya Jamhuri ya Muungano inampa uwezo huo Mheshimiwa Rais. Mfano tulikuwa na Wizara ya Nishati na Madini akazitenganisha, anaaficha kitu gani yote hiyo ni kutaka *efficiency*, kazi zake ziende vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, TAMISEMI ilikuwa chini ya Waziri Mkuu ameihamishia Ikulu anaaficha nini? Yote hiyo ni kutaka kazi zisimamiwe vizuri. Kwa hiyo, sisi tunaendelea

kumpongeza Rais na tunamwambia aendeleee kufanya kazi kadiri atakavyoona mafanikio yatakuwa makubwa na ni mazuri. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wanasema Shirika la Ndege halina faida wala maana yoyote. Nimeshukuru kaka yangu Mheshimiwa Abbas ameелееа vizuri faida zake, lakini shirika hili la ndege ni *identity*, ni utambulisho wetu Watanzania na lina faida kubwa sana. Faida yake si tiketi tu, *Emirates, Ethiopia Airline, Qatar* hawajawahi kupata faida kwenye tiketi wanapata faida kwenye mambo mengine, kwenye mzunguko kama alivyosema kaka yangu Mheshimiwa Abbas, siwezi kurudia, ndivyo faida inavyopatikana.

Kwa hiyo, mambo haya ya kusema ndege hazina maana, ndege zina maana kubwa, naipongeza Serikali yangu imeweka bajeti ya kuongeza ndege nyingine, naomba iongeze ili tuendelee kufanya vizuri jambo ambalo wao hawakutegemea. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kelele zilizopigwa nchi hii ni shirika la *ATCL* kufa. Leo Mheshimiwa Rais amejitokeza kulirejesha shirika hili ni lazima alisimamie kikamilifu ili isije tena ikajitokeza hali ile kama ilivyokuwa mwanzo. Kwa hiyo, mimi naungana naye mkono kuhamisha kitengo hicho kukiweka lkulu ili usimamizi wake uwe wa karibu zaidi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika *legacy* atakazoziacha Mheshimiwa Rais wetu ni pamoja na Shirika la Ndege na reli. Leo reli ya Dar-es-Salaam – Morogoro ya *Standard Gauge* inayojengwa imeshafika asilimia 50, lakini pia kuna *Phase II* inayojengwa na yenyewe inaendelea vizuri na tunaomba Mungu iendelee vizuri na iishe ili na sisi Tabora tuingie sasa *Phase III*. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Uwanja wa *KIA* kuna *hangar* ilijengwa muda mrefu, njiombe Serikali iboreshe *hangar* hiyo ili ndege zetu sasa ziweze kutengenezwa Tanzania. Tuna *hangar* kubwa mpaka *dreamliner* inaingia. Kwa hiyo, sioni

tena sababu ya kuchukua ndege kuzipeleka nchi za nje kwenda kutengenezwa, tuna ma-*engineerzaidi* ya 60 ambao wana uwezo wa kutengeneza ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimwombe Waziri na Serikali kwa ujumla ihakikishe imeboresha *hangarile* ndege zetu sasa zifanyiwe ukarabati ndani ya nchi yetu na sio kupeleka nje. Hiyo iambatane pia na Uwanja wa Ndege wa KIA uendelee kukarabatiwa, uongezwe *parking* na mambo mengine kwa sababu uwanja ule sasa umeshakuwa mkubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jana pia waliongelea kuhusu bandari. Mimi niipongeze Mamlaka ya Bandari, kazi ni nzuri, sasa mizigo inatoka haraka siyo kama ilivyokuwa mwanzo, kwa kweli wanajitahidi kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nimesikia Mkurugenzi wa Bandari amelaumiwa kwa kuwafanyisha watumishi kazi mpaka saa 7.00 za usiku; mimi niipongeze sana, dunia nzima watu wanafanya kazi saa 24 sehemu kubwa kama zile. Yeye ni kupanga *shift* zao kwamba nani ataingia mpaka saa 10.00, nani ataingia mpaka saa 5.00 ya usiku na nani ataingia mpaka alfajiri ili kuweka mambo sawa na ili bandari yetu iende na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi kubwa inayofanywa ya kupanua hizi bandari inabidi ziende na wakati. Kwa hiyo, kitu cha muhimu ni kupanga *shift* na nawapongeza sana. Yule aliyekuwa analaumu kwa nini wanafanya kazi mpaka saa 7.00 ya usiku nadhani hajatembea, atembee duniani, dunia nzima watu wanafanya kazi saa 24. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naongea kuhusu *SUMATRA*. *SUMATRA* kuna kitengo kimeanzishwa kinaitwa *VTS (Vehicle Tracking System)* ambapo sasa hivi mabasi yetu yamefungwa kifaa hiki akitembea mbio au akifanya nini anaonekana moja kwa moja kule Dar es Salaam. Haya ni maendeleo makubwa sana ya Serikali ya Awamu ya Tano, tunaipongeza Wizara ya

Ujenzi na Mawaziri na Manaibu wote kwa kazi hii nzuri.
(Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Muda wako umeisha Mheshimiwa, kengele imeshagonga. Ahsante sana.

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, ahsante, naunga mkono hoja. *(Makof)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilikuwa nimemuita Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, atafuatiwa na Mheshimiwa Shaabani Shekilindi na Mheshimiwa Susan Kiwanga ajiandae.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mungu kwa kutupa uhai na uzima na kwamba tunaendelea kuwatumikia Watanzania. Niendelee kuwashukuru ndugu zangu wa Mkkinga kwa jinsi ambavyo wanaendelea kuniunga mkono ninapotimiza majukumu yangu ya kuwatumikia. *(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze vilevile kwa kuishukuru Serikali kwa jitihada inazofanya katika kuwezesha miundombinu ya nchi yetu, hususan Bandari ya Tanga tunaiona kazi inayofanyika ya kupanua na kuongeza kina cha bandari ile, tunawashukuru. Tunawashukuru vilevile kwa Barabara ya Tanga – Pangani – Bagamoyo ambayo tunaambiwa muda si mrefu itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami, tunaishukuru Serikali kwa jitihada hizo. *(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nikitoa pongezi hizo, nieleze masikitiko yangu katika maeneo mawili. Kwa muda

mrefu sasa tumekuwa tukipigia kelele barabara ya kutoka Mabokweni – Maramba – Bombo Mtoni – Umbo Junction – Mkomazi – Same. Barabara hii ni muhimu sana kwa uchumi wa Mkoa wa Tanga na ni muhimu sana kwa watu wa Maramba, Mkinga, Korogwe, Lushoto na Same. Ni barabara inayounganisha Mkoa wa Tanga na Mkoa wa Kilimanjaro lakini vilevile na nchi jirani ya Kenya. Ni barabara ya kiusalama kwa sababu ipo kwenye ukanda wa mpakani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni barabara ya kiuchumi kwa sababu inaunganisha maeneo ya kiutalii. Unapozungumzia utalii unaofanyika Zanzibar fursa hiyo vilevile inakuja kwa upande wa Tanga, unaiunganisha na eneo lile la Bagamoyo lakini vilevile unaunganisha na Mbuga ya Mkomazi ambayo inaanzia upande huu wa Mkinga eneo la Mwakijembe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni barabara muhimu sana kwa uchumi wa kiutalii lakini uchumi wa kusafirisha mazao, kama walivyosema wenzangu, bidhaa za mazao ya matunda, mbogamboga, karafuu kutoka kule Kigongoi na mazao ya viungo kutoka Muheza na kule Bosha. Kwa hiyo, ni barabara ambayo tukiona kunakuwa na kigugumizi cha kuishughulikia tunapata shida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba Serikali ihakikishe barabara hii sasa inawekewa fedha ili iweze kufanyiwa usanifu. Barabara hii kwa upande wa Kilimanjaro tayari usanifu umekwishafanyika, tunashangaa kwa nini upande huu wa pili barabara hii haifayiwi usanifu? Tunaomba suala hili liweze kushughulikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kuna matengenezo yanayoendelea katika barabara hiyo lakini kuna maeneo korofi. Eneo la kwa Mukamba, pale tunahitaji kifereji na kuweka kifusi cha changarawe ili barabara ile iweze kupitika wakati wote. Eneo la Majumba Matatu na lenyewe ni korofi, najua kuna mifereji inaanza kujengwa pale lakini ikamilishwe kwa wakati na iongozewe eneo refu zaidi ili barabara ile iweze kupitika kwa wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ni bandari. Mwaka 2014 Kampuni ya Kichina inayojulikana kama Hengia ilionesa nia ya kuja kuwekeza katika nchi yetu kiwanda cha kuzalisha tani milioni 7 kwa mwaka, uwekezaji wa dola bilioni 3, lakini vilevile walisema wataanza na uwekezaji wa bilioni 1, hapa unazungumzia trillioni 2.3 hivi zingeweza kuwekezwa katika kujenga kiwanda kikubwa katika Ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara. Hata hivyo, pamoja na jitihada zao za kuomba vivutio mbalimbali vyta uwekezaji bado tangu mwaka 2014 mpaka leo kiwanda hiki kimekwama kupata vibali kianze kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu hawa walitaka sambamba na kujenga kiwanda cha kuzalisha simenti vilevile waweze kupata fursa ya kujenga *jet*. Tumekuwa na kigugumizi cha kuwapa ruksa ya kujenga *jet* kwa sababu za kiusalama. Nijambo ambalo unaweza kulielewa ukielezwa lakini maswalli tunayojuliza hivi sisi tumeshindwa kuvi-*engage* vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vikasimamia *jet* ile hata kama wameijenga wao? Tukawaweka watu wetu wa *TRA* wakasimamia mapato yetu? Tukawaweka vyombo vingine vya bandari vika-*manage* *jet* ile ili uwekezaji hu mkubwa tusiweze kuupoteza? Watu wa Mkinga tunahitaji kupata majibu ni lini kitendawili hiki kitateguliwa? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapata hofu kwamba tunaenda kupoteza uwekezaji mkubwa huu wa trillioni 6.5 ambazo zingeingia kwenye uchumi wetu. Tunaiomba Serikali ifanye maamuzi ili watu hawa waweze kuanza ujenzi na kuzalisha simenti. Kama tunadhani hatuwezi kuwaruhusu wao kujenga basi twendeni tukajenje sisi *jet* ile ili uwekezaji huu usiweze kupotea. Naiomba Serikali ifanye maamuzi ya haraka ili jambo hili liweze kufanikiwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Shaabani Shekililindi, atafuatiwa na Mheshimiwa Susan Kiwanga, Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha ajiandae. Mheshimiwa Susan Kiwanga atachangia kwa dakika saba.

MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii niweze kuchangia Wizara hii ya Miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingu wa rehema kunipa afya na nguvu ya kuweza kuchangia katika Wizara hii. Niwapongeze Waziri, Mheshimiwa Eng. Kamwelwe, Naibu Waziri Mheshimiwa Nditiye na Naibu Waziri Mheshimiwa Kwandikwa kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuishukuru Wizara hii kwa kunitengenea fedha za kujenga kilometa 1 kila mwaka ambapo zinajengwa katika barabara ya kutoka Magamba - Mlalo na Magamba - Mlola. Nashukuru Serikali kwa kilometa 1 waliyotutengea lakini ni chache sana ambapo sasa hatuendi na ile kasi ya kujenga viwanda na kwenda kwenye uchumi wa kati. Niucombe Waziri aweze kututengea hata kilometa 4 ili pande zote mbili ziende kilometa 2, Mlalo kilometa 2 na Mlola kilometa 2. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hayo pia kuna barabara ambayo kila siku nilikuwa naionglea, inaanza Mlalo - Ngwelo - Mlola - Makanya - Milingano - Mashewa. Barabara hii inaenda mpaka kwa Mheshimiwa Kitandula Mkinga kule, inaenda mpaka Chongoleani, kwa hiyo, barabara hii ni ya kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini barabara hii nimeiongelea sana na hii ni bajeti ya nne. Niucombe Mheshimiwa Waziri kwamba, itoshe sasa, mimi siyo mtoto wa kufikia, mimi ni mtoto wako kabisa, sijawahi kushika shilingi, sijawahi hata kukataa bajeti, ifikie hatua sasa Mheshimiwa Waziri hebu barabara hii uichukue ili tuweze kunusuru watu wa Makanya na maeneo mengine niliyyataja. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo Mheshimiwa Waziri anafahamu fika kwamba barabara ile ni ya kiuchumi. Barabara ile kuanzia Makanya au Mlola kwenda maeneo niliyyataja hakika tutakuwa tumekuza uchumi. Kwa

hiyo, nikuombe sana itoshe, kwa kweli sijui niingie kwa *style* gani au nije kwa *style* gani ili uweze kunielewa barabara ile iweze kupandishwa hadhi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kuna barabara nydingine ya kutoka Duchi – Ngulwi - Mombo ambayo ni kilometra 16. Barabara ile Mheshimiwa Waziri niliripoti kwako 2017 wakati barabara ile inapata mafuriko. Kwa hiyo, nikuombe nayo barabara hii Mheshimiwa Waziri hebu iingize sasa iweze kutengenezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii walisema kwamba *TARURA* inaweza lakini *TARURA* haina fedha za kutosha kila mwaka inatengewa kilometra 1 au 2, kwa hiyo, ni kama vile barabara hii imetelekezwa. Mheshimiwa Kwandikwa ni shahidi amefika mpaka pale kwa wananchi wa Ngulwi ameongea nao akawaambia kwamba barabara hii sasa itatengenezwa lakini mpaka leo hii barabara ile hajatengenezwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ile pia ni ya kiuchumi. Halafu ni barabara ya mchepuko, kama unavyofahamu Lushoto kuna barabara moja tu kubwa ambayo ni ya Mombo – Soni - Lushoto kilometra 32. Kwa hiyo, kukitokea matatizo kama yalivyotokea 2017 na kuziba barabara ile ya Soni – Mombo basi Wilaya ya Lushoto tunakosa huduma kabisa. Kwa hiyo, niombe sasa barabara hii iwe barabara mbadala na inawezekana hata barabara hii sasa ikawa ni barabara kwa ajili ya kushuka tu magari na hii ya Soni - Mombo kwa ajili ya kupandisha magari. Hiyo, naamini kwa kweli ukiipanga vizuri Mheshimiwa Waziri inawezekana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja sasa kwenye minara (mawasiliano). Mheshimiwa Nditiye wewe ni shahidi nimekuja mara kadhaa kwako kwa ajili ya kukuomba minara. Mfano maeneo yangu mengi ya Wilaya ya Lushoto hayana mawasiliano, mfano, Ubiri, Mazumbai, Magului, Makanya, Kireti, Kigumbe na maeneo ya Mlalo ya Makose, Longoi, Mavumo na Kikumbi. Nikuombe chondechonde kaka

yangu hebu sasa peleka mawasiliano katika maeneo haya ili wananchi wetu waende na wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende sasa kwenye Uwanja wa Ndege Tanga, wenzangu wameongea sana kuhusu uwanja huu. Uwanja ule wa Ndege kweli tumeona tumetengewa mashine zile lakini ziende sambamba sasa na kuongeza uwanja ule. Mwaka jana Mheshimiwa Waziri ni shahidi wakati wa bajeti wakati ana-*wind-up* alisema kabisa kwamba uwanja ule utaletewa *bombardier* lakini mpaka leo hii *bombardier* hatuioni, Tanga kumekucha, Tanga kuchele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu sasa Tanga ionekane, safari hii tuweze kupata *bombardier* inayotoka Dar-es-Salaam kuja Tanga mpaka Pemba ikiwezekana hata iende mpaka Mombasa. Hili naomba sasa nalo ulichukue wakati wa ku-*wind-up* naamini kabisa uthaliseMEA na ukizingatia Tanga tayari tunaongeza kina cha bahari, Serikali imetuona, tuna viwanda pia kama unavyoja.

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Naibu Spika, naona muda umeisha. Naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia 100, ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Susan Kiwanga atachangia dakika saba, atafuatiwa na Mheshimiwa Ignas Malocha, kama muda utakuwa bado upo atafuata Mheshimiwa Ngeleja.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa sana hapa nilipo nalia. Silii kwa kupenda, nimetuma kwenye ma-*group* ya Wabunge, nimemtumia Waziri, kama kijiko kimezama barabara ya kutoka Ifakara - Mlimba hivi akina mama kutoka Mlimba wataendaje Hospitali ya Ifakara kwenda kujifungua?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kijiko kimezama (*excavator*) na yule mtoto anayesimamia pale kijiko kile alichokodisha cha baba yake amelazwa hospitali. Barabara hii imeshafanyiwa upembuzi yakinifu, imeisha mwaka 2017 lakini mpaka leo barabara hii hajengwi kwa kiwango cha lami. Chondechonde, hivi Watanzania wanaoishi Mlimba mnawahesabu wapo katika kundi gani nchi hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ni mbaya. Kama ni hali ya dharura basi iko Mlimba. Kila mkandarasi akipewa ile barabara kwa mwaka mzima aihudumie, akimaliza mkataba harudi tena kwa sababu ile barabara ni hatari, hivi tuseme nini mpaka muelewe? Ni dharura, naungaje mkono wakati barabara yangu haina lami? Naungaje mkono hii bajeti? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa dharura, wataalam mnanisikia mko hapa. Ndugu Mfugale uko hapa, watu wa Mfuko wa Barabara mko hapa nendeni sasa hivi Mlimba mumpigie Eng. Makindi yuko Mlimba sasa hivi karibu wiki wanahangaika na barabara hii. Leo vyote mnavyojadili hapa mimi kwangu naona ni kizunguzungu, tunaomba barabara, imeisha upembuzi yakinifu mwaka 2017 kuna haja ya kujenga ile barabara ili kuokoa wananchi wanaotoka Mlimba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nachangia suala lingine kuhusu watu wa TAZARA. Leo nimepata taarifa ukaguzi wa ndani umebaini yule mhasibu na ameshasimamishwa bilioni moja *point* kadhaa zimeliwa. Watumishi wa TAZARA wanaostaafu sasa hivi wakienda kwa huyo mhasibu kudai mafao yao wanajibiwa mambo ya ajabu, lakini cha kushangaza Meneja wa Mkoa wa Tanzania ameongezewa muda wakati ameshindwa kusimamia mpaka mhasibu ametafuna hizo hela, sijui wanashirikiana? (*Makofii*)

Mheshimiwa Waziri, angalia suala la TAZARA. Serikali inalipa watumishi pesa kwa kodi za watanzania wengine lakini pale pale TAZARA kuna mchwa huyo anakula pesa. Nendeni mkaiangalie TAZARA. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na wastaafu nimeshapeleka faili kwa Mheshimiwa Kijaji, wale 1072 mpaka leo wengine wanakufa, mafao yao hajjulikani, walistaafishwa kwa lazima wa umri wa miaka 55, mmewapunja, naomba muwape haki zao, tatizo nini? Leo nimeamua kulia na *TAZARA* na barabara ya Ifakara - Mlimba kilometra 126 *point* zake, mmeshafanya upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba kwa hali ya dharura hata tuma hapa mtaalam aende kule leo, hakuna gari inayopita, picha hizi hapa *excavator* limezama, gari gani itapita kwenye hiyo barabara ya *TANROADS*, hiyo ni dharura. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, watu watakuifa kule wakina mama na watoto na wagonjwa watakuifa kwa sababu tuna kituo cha afya kimoja tu Mlimba, basi madaktari wanne! Hospitali ya Wilaya ipo Ifakara, Hospitali ya Rufaa ya St. Francis ipo Ifakara, watu watafikaje huko?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mpango, sawa mnaweka hela tu kwenye ndege, kwenye nini hatukatai tutaendeleza uchumi lakini wananchi wa Mlimba tuna shida kubwa, naomba mtupe barabara tuendele na haya mambo mengine. Hizi ni kodi za Watanzania na wananchi wa Mlimba wanalipa kodi kama wanavyolipa wengine. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba, simalizi hata dakika saba kwa uchungu, ninyi wenyewe mnajua nachangiaga mpaka kwa sababu nitamaliza viyi dakika saba, nataka majibu. Ningombaa Waziri aje na neno la dharura kuhusu barabara ya Ifakara mpaka Mlimba mnawaambiaje wananchi wa Mlimba. Asante sana. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge mniruhusu nimpe kazi ya kumnumulie maji, Mheshimiwa Heche kamnumulie maji Mheshimiwa Susan maana kidogo koo limeshuka kidogo. Naamini Mheshimiwa Heche ataifanya hiyo kazi kwa uaminifu. (*Makof!/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, Mheshimiwa Ignas Malocha atafuatiwa na Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, kama muda utabaki basi tutamsikia Mheshimiwa Selemani Zedi.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kupata muda kuchangia Wizara hii ya Ujenzi. Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniweka hai mpaka siku ya leo. Napenda kabisa kumpongeza Mheshimiwa Waziri *Engineer Kamwelwe*, Naibu Mawaziri Mheshimiwa *Engineer Nditiye* na Mheshimiwa Kwandikwa, Katibu Mkuu *TANROADS EngineerMfugale* na watendaji wote wa Wizara hii. Vilevile bila kumsahau Meneja wangu wa *TANROADS* Mkoa wa Rukwa na wasaidizi wake wanafanya kazi vizuri sana, nawapongeza sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanza napenda kusema kwamba Mkoa wa Rukwa ni mkoa wenye mvua nyingi sana, kwa maana hiyo barabara zake za changarawe ni mara nyingi zinaharibika sana lakini fedha tunazopangiwa ni kidogo sana, hazikidhi mahitaji ya uharibifu wa barabara zile. Nishukuru Serikali kwa ujenzi wa daraja lile la Mto Momba kama wenzangu walivyoshukuru, sasa hivi tumeona urahisi hata malori yanayopita sasa hivi yaliyokuwa yanazunguka kule Kibaoni yamebeba nguzo, sasa hivi yanakatisha yanapita yanaingilia Songwe yanakuja kutokea Kamsamba na kuleta nguzo; tunashukuru sana kwa kweli Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, tunaishukuru Serikali kwa kilio cha wananchi wa Mji Mdogo wa Laela walikuwa wana kilio cha kivuko lakini kupertia TAMISEMI tumepata milioni 163 kujenga kivuko kile, tunashukuru sana Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie barabara ya Kiliamatundu, Muze, Ntendo na Kasansa. Waziri aliyepo sasa hivi ni Waziri ambaye huwezi ukamwambia chochote juu ya barabara hii. Anaifahamu vizuri umuhimu wake na jinsi inavyounganisha mikoa hii mitatu; tunashukuru mmejenga daraja lakini tunaomba sasa muweke nguvu kuiwekea lami. Na mmetenga kiasi cha milioni 180 kwa ajili

ya usanifu lakini naona fedha hii sidhani kama inaweza ikatosha kwa urefu wa ile barabara, ile barabara ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Eng. Kamwelwe wewe ni mwenyeji wa maeneo yale, tunaomba kabisa katika awamu yako hii weka nguvu ile barabara iweze kutengewa fedha ili kupata lami; kama tutakosa katika kipindi chako sidhani kama tunaweza tukapata tena. Ni kipindi muhimu kabisa na muafaka kwa sababu unajua umuhimu wa barabara ile kiuchumi, tunakuomba sana utilie maanani katika barabara hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kipande cha barabara cha Ntendo – Muze. Barabara hii ndiyo inayotumika katika kuingiza malighafi inayotoka ukanda wa Ziwa Rukwa, ni barabara ambayo ipo *busy* sana muda wote, malori ni muda wote. Nashukuru Serikali mwaka jana mlitupangia pesa tukaweza kutengeneza kilometra 2 za lami lakini nashangaa badala ya kuongeza, mwaka huu mmeponguzza badala ya kutuungeza kilometra 5 mmetuwekea kilometra 0.8 badala ya kuongeza. Sasa nashindwa kuelewa ni kwa namna gani tena mnarudi nyuma badala ya kwenda mbele, tunaomba sana Mheshimiwa *Engineer* Kamwelwe utuongezee pesa hii barabara iweze kutanuliwa na kumalizika kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiacha hilo, barabara hiyo kilometra 8 za Mlima ambao wakati mwingine barabara ni finyu, kama lori lilikwama lingine haliwezi likapita. Nakumbuka mwaka juzi Waziri Mkuu alikwama, tukaanza sisi wote kutafuta namna gani Waziri Mkuu atapita lakini *solution* ilipatikana, alikuja Katibu Mkuu ambaye sasa hivi hayupo hapo akashauri tuipanue lakini nashangaa katika bajeti hii sijaona. Mheshimiwa *Engineer* Kamwelwe naomba hilo na lenyewe uweze kuliangalia, eneo la Mwilimani linahitaji kabisa kupanuliwa na kuwekwa zege sehemu zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara nyingine ni ya Kalambanzite – Illemba kilometra 24; kilometra 12 zipo mlimani. Hii barabara tunashukuru *TANROADS*ilishaichukua, tunaomba

na yenye we basi iweze kujengwa kwa kiwango kizuri cha changarawe na mlima wote uwekwe zege lakini nimeona kwenye bajeti mmetenga pesa kidogo kama milioni 30, milioni 30 utatengeneza kitu gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba sana Mheshimiwa Waziri uweze kuliona hili, tena ahadi ya Rais wa Awamu ya Tano aliahidi kuiwekea lami, sasa nashangaa sasa hivi suala badala ya lami hata changarawe, hata kuweka zuge mlima wa kilometra 12 tunashindwa kuweka fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyingine ni barabara ya Miangalua – Chombe...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa kengele ya pili imegonga.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, tutamalizia na Mheshimiwa Selemani Zedi.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kwanza naomba niipongeze sana Serikali yangu ya Awamu ya Tano kwa kazi kubwa sana inayofanyika ya ujenzi wa miundombinu mingi mbalimbali nchini na pengine tu kabla sijaenda mbali zaidi, njaribu kugusia kidogo hii hoja iliyotolewa na mchangiaji mmoja aliyezungumzia kuhusu suala la mchango wa Sekta ya Ujenzi kwenye uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti unaonyesha kwamba katika miradi yote ya ujenzi, asilimia isiyozidi 30 ndio huwa mchango wa wakati wa mradi, asilimia 70 huwa inapatikana pale mradi unakuwa umekamilika na kuanza kutumika. Jana tulimsikia mzee wangu Mheshimiwa Ndassa hapa alizungumzia kwamba Mji wa Ngudu umedumaa kwa sababu hauna barabara. Ukienda sehemu zote ambazo barabara zimejengwa, hali ya maisha na shughuli za kiuchumi zinakwenda kasi zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo, tunavyozungumza kujenga reli ya kiwango cha *standard gauge* tunategemea reli hii ikikamilika ndiyo itakayoleta manufaa na itakayoonyesha sasa uchumi kukua kwa kasi zaidi kuliko wakati wa utekelezaji wa mradi wenyewe. Faida zinazokuwepo wakati wa ujenzi ni kidogo sana kwa wastani hazizidi asilimia 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niseme tu pamoja na kwamba Mheshimiwa Zitto namuheshimu sana lakini ukweli huu anaufahamu ni vizuri tukalionia hilo kwamba *investment* zinazofanyika leo zina *multiply effect* kubwa kwa baadaye hasa baada ya sekta tarajiwa kama kilimo na viwanda. Huwezi ukajenga kiwanda leo Kigoma cha *cement* ambayo huwezi ukaisafirisha kuipeleka kwenye soko Dar es salaam; ukishaweka reli ndiyo utawezesha kiwanda kujengwa kule. Leo hili muulize Dangote anavyohangalika kufikisha *cement* yake kwenye maeneo ambayo hayana miundombinu ya barabara. Kwa hiyo, miundombinu inachochea uchumi baada ya kuwa imekamilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya ufanuzi huo na pongezi hizo kwa Serikali, niendelee kuipongeza sana Serikali yangu kwa miradi hii mikubwa ambayo pia inafanyika katika Mkoa wetu wa Shinyanga. Kwa muda mrefu sana nimekuwa nikiomba barabara ya kutoka Kahama kwenda Geita ijengwe kwa kiwango cha lami, ninashukuru sana nimeona kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri aya ile ya 28, amesema taratibu za kupata wakandarasi ndizo zinaendelea na kwa bajeti hii ile aya ya 248 ametenga bilioni 5 kwa ajili ya kuanza ujenzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sana Mheshimiwa, bahati nzuri Mheshimiwa Naibu Waziri Kwandikwa yupo na anafahamu barabara hii umuhimu wake kwamba mchakato wa kupata wakandarasi ambao sasa tunakwenda mwaka wa tatu toka 2016, 2017 na 2018 ukamilike na barabara ianze kujengwa. Ni barabara ya muhimu sana kiuchumi, inaunganisha migodi ya Bulyanhulu na Buzwagi; ni barabara yenye sifa katika zile barabara za kipaumbele kwa sababu

inaunganisha Mkoa wa Shinyanga na Mkoa wa Geita. Vilevile ni barabara ambayo ipo kwenye ahadi zetu za kipaumbele. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais mwaka 2017 amefika, ameongea na wananchi wa Segese akawaahidi wananchi wa Bukoli kwamba barabara hii itaanza kujengwa kwenye kipindi hiki na hii ndiyo bajeti ya mwisho ya utekelezaji tunayofanya, bajeti ijayo tutakuja kuipitisha na kwenda kwenye uchaguzi. Ni muhimu sana hizi bilioni 5 tulizozisema na mchakato wa kupata wakandarasi ambao umeanza miaka mitatu sasa ukamilike ili ujenzi uweze kuanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara nyingine ya kutoka Kahama kwenda Nyang'wale hadi Busisi. Barabara hii haijaguswa kabisa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, tuliahidiwa kwenye bajeti iliyopita kwamba ingeanza kufanyiwa upembuzi yakinifu, sasa hivi hata kutajwa haijatajwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hata ile barabara ya kutoka Kahama – Solwa – Managwa ambayo pia inaunganisha Mkoa wa Shinyanga na Mkoa wa Mwanza, ilikuwemo kwenye upembuzi yakinifu na ilishakamilika lakini kwenye orodha ya barabara ambazo zimetajwa kwamba zimekamilika kufanyiwa upembuzi zinatafutiwa fedha ili zianze kujengwa, haijatajwa. Nilikuwa naomba sana rekodi zikae sawa, muda wote tuwe tunataja tumeefika hatua gani ili kesho na keshokutwa tusijetukarudi tena kuanza kuzungumza kwamba tunaomba ifanyiwe hatua fulani wakati ilishakamilika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe la mwisho, Mheshimiwa Waziri Mpango yupo hapa, nimeona kwenye taarifa ya Waziri kuna ujenzi wa vituo Dakawa na Muhalala; mkandarasi amesimama kwa sababu ya suala la VAT. Nilikuwa naomba suala la VAT ambalo linahusu kuwezesha miradi ya ujenzi kukamilika kwa wakati, mzungumze mlimalize; Mheshimiwa Rais aliagiza akiwa Mwanza wakati ule wa

uzinduzi wa ujenzi wa vivuko kule, ninaomba mmalize mkandarasi arudi *site*, kuna hasara tunapata kwa kutokumaliza mazungumzo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimegongewa kengele ya pili, nisingependa kuchukua zaidi muda. Nakushukuru sana kwa nafasi na naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Selemani Zedi.

MHE. SELEMANI J. ZEDI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia. Kwanza, nianze kwa kuwapongeza Waziri na Naibu Mawaziri wawili wa Wizara hii kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi uliopita nliuliza swali hapa Bungeni kuhusu barabara ya kilometra 149 inayoanzia Tabora kuititia Mambali – Bukene- Itobo na hatimaye Kagongwa. Barabara hii ndiyo barabara pekee iliyo bado kwenye hali ya changarawe inayotoka Tabora mpaka Kahama na barabara hii kwanza ni ahadi ya Mheshimiwa Rais na pili, imo kwenye llani yetu ya uchaguzi. Nichukue fursa hii kuipongeza Serikali kwa kutupatia milioni 789 ambazo zimekamilisha usanifu wa awali na mwezi uliopita Waziri alijibu swali langu kwamba mwezi wa sita ule usanifu wa kina unakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, rai yangu kwamba Wizara ijitahidi kwamba kama ilivyoahidi (*commit*) kwamba ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami utaanza kabla ya 2020 wakati ambako tutaingia kwenye uchaguzi. Kwa hiyo, nina imani na Serikali yangu najua hili litafanyika lakini ni wajibu wangu kulikumbushia.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii wakati tunasubiri iweze kujengwa kwa kiwango cha lami, inapaswa iwe inapitika wakati wote. Ninaipongeza Wizara kwamba nimeangalia kwenye kitabu cha hotuba ya Waziri kuna fedha zimetengwa kwa ajili ya kuhakikisha barabara hii wakati wote

inapitika. Fedha hizo zipo kwenye mafungu mawili; fungu la kwanza ni fedha zinazotoka Mfuko wa Barabara na fungu la pili ni fedha zinazotoka Mfuko wa Serikali Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa Mfuko wa Barabara, barabara hii imepangiwa milioni 332 na upande wa fedha zinazotoka Serikali Kuu, barabara hii pia imepangiwa milioni 330. Ni rai yangu kwa Wizara kwamba fedha hizi zilizotengwa zipatikane na zipelekwe ili barabara hii iweze kuwa inatengenezwa kila wakati na hasa yale matengenezo ya muda maalum (*periodic maintenance*) wakati wa mvua barabara hii huwa inaharibika vibaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna fedha ambazo zimepangwa kwa ajili ya Mkao mzima wa Tabora kama bilioni 2.4 kwa ajili ya kutengeneza kilometra 1180. Sasa hoja yangu hapo ni kwamba fedha hizi zimepelekwa kwa ujumla, zinasema tu ni za Mkao wa Tabora kwa ajili ya kutengeneza kilometra 1180 lakini Mkao wa Tabora una Wilaya 7 na zote zina barabara hizi za changarawe. Kwa hiyo, hotuba ya Waziri hajiaainisha kwamba ni kiasi gani kitatengeneza barabara zilizopo Nzega, kiasi gani Sikonge, Kaliua au Urambo. Kwa hiyo, imewekwa jumla na hatari yake ni kwamba fedha zote zinaweza zikaelekezwa Wilaya 1 au 2 halifu zingine zikakosa. Kwa hiyo, tuainishiwe kabisa hizi bilioni 2 ni kiasi gani kitakwenda kila Wilaya ili angalau tuwe tunajua ufuatiliaji utakuwaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote. Miaka miwili nyuma hapa niliomba minara ya simu ya Kata 4; Kata ya Kahamahalanga, Kata ya Karitu, Isagehe na Semembela lakini ni kata mbili tu ambazo zimepata hiyo minara ya simu; Kata ya semehembela na Kata ya Karitu bado hazijapata ingawa zilikuwa kwenye orodha ambayo Mheshimiwa Waziri aliitoa ya kata ambazo zitapatiwa minara ya simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tunajua kwamba sasa hivi maisha ya sasa ni mawasiliano ya simu, kwa hiyo, kunapokuwa na maeneo tunayaacha bila kuyapatia

mawasiliano ya simu za mkononi kama ilivyo Semembela na Karitu, maana yake ni kwamba tunawaacha nyuma ya ulimwengu wa kisasa. Sasa hivi maisha ya kisasa kwa sehemu kubwa simu za mkononi zinachangia, ukiwa na simu za mkononi utaweza kulipa ada za watoto, ankara au madai mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tunapeleka umeme vijijiini, tunataka wananchi wetu wa vijijiini waweze kulipia LUKU na bili za umeme huko huko wakiwa vijijiini. Kwa hiyo, kuna umuhimu sana wa maeneo ambayo hayana minara ya simu yaweze kupatiwa minara ya simu. Nitumie nafasi hii kuikumbusha Wizara kwamba Kata ya Semembela na Kata ya Karitu ambayo tangu miaka miwili nyuma ipo kwenye orodha, safari hii na yenye we kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote iweze kupata mawasiliano hayo muhimu sana ya simu za mkononi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii na ninaunga mkono hoja asilimia mia moja, asante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge tumemaliza wachangiaji wetu wa kipindi cha kwanza. Niwataje Wabunge wachache tutakaoweza kuanza nao mchana, Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka, Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama, Mheshimiwa Zakaria Paul Issay, Mheshimiwa Godfrey Mgimwa na Mheshimiwa Hasna Mwilima. Wengine wataendelea kutajwa kadri tutakavyokuwa tukiendelea.

Jambo lingine, kulikuwa na uchangiaji katika hiki kipindi chetu niwakumbushe tu Waheshimiwa Wabunge, tunapoitana dada, kaka, shemeji sjui babu ama nani humu ndani tukumbuke tu kwamba tunatakiwa kuitana Waheshimiwa. Wakati mwingine watu wanasahau akishaita hivyo anaita jina la mtu moja kwa moja. Sasa pale tunapoanza kukumbushana inakuwa tabu kidogo. Kwa hiyo, tukumbuke tunapochangia kuwataja Wabunge ambao wameshachangia hata kama unawajibu ama unawajibu

kwa mchango wao ambao umeshapita kuwaita Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge lipo pia tangazo kutoka Idara ya Utawala na Rasilimali Watu ya Bunge. Mnatangaziwa Wabunge wote kuwa wataalam wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (*NIDA*) wapo hapa Bungeni kwa ajili ya kutoa vitambulisho kwa Wabunge waliokuwa wamejiandikisha. Kwa hiyo, huduma hiyo inatolewa katika viwanja vya Bunge nyuma ya jengo lililokuwa la zahanati ya Bunge, lile Jengo la Msekwa kule nyuma kulikokuwa na zahanati zamani. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge waliokuwa wamejiandikisha wakachukue vitambulisho vyao na wale ambao hawakupata fursa ya kujiandikisha pengine wanaweza kupata hapo maelezo ya nini cha kufanya.

Waheshimiwa Wabunge baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi kamili Alasiri leo.

(Saa 7.00 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi saa 10.00 Jioni)

(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)

NAIBU SPIKA: Tukae.

HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi,
Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020**

(Majadiliano Yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano, tutaanza na Mheshimiwa Joyce Bitta Sokombi dakika saba, atafuatiwa na Mheshimiwa William Mganga Ngeleja.

MHE. JOYCE B. SOKOMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nami nafasi hii niweze kuchangia Wizara hii ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, hasa kwa

manufaa ya wananchi wa Mkoa wa Mara na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti kwa miaka mitatu zimetengwa shilingi triliuni 13. Naitaka Serikali itueleze, tunapata ajira kiasi gani na *return* yake ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha nyingi za maendeleo kila siku tunaambiwa zinafanya upembuzi yakinifu. Maana toka nimekuwa Mbunge, sasa hivi ni mwaka wa nne, kila ukiuliza swali unaambiwa ni upembuzi yakinifu, sasa sijui huo upembuzi yakinifu utaisha lini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nasema hivyo? Sasa hivi Wilaya ya Rarya, TARURA haijapata fedha za maendeleo ya barabara takribani miaka miwili mfululizo na ukiangalia Wizara hili Imetengewa pesa nyingi sana. Naomba tafadhali Mheshimiwa Waziri asikilize kilio cha wananchi wa Mkoa wa Mara apeleke fedha zikamalize ujenzi wa barabara ambazo zinatakiwa kujengwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Musoma – Busekela ina kilometra 42, lakini fedha zilizopelekwa ni za kilometra tano tu, kilometra 37 bado hazijajengwa. Sasa sijui Mheshimiwa Waziri atatuambia ni lini zile kilometra 37 zitaenda kumalizwa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Wanyele – Kitario imekatika na kila siku nimekuwa nikizungumzia hapa kwenye maswali; na majibu yamekuwa ni yale yale ya marudio. Ile barabara ya Wanyele – Kitario ni barabara ambayo inahitaji kuwekwa daraja na ilishasababisha maafa. Kuna takribani watoto 20 walishafariki na nilishasemba katika hili Bunge lako tukufu, lakini mpaka sasa hakuna hatua yoyote ambayo imeshachukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba tafadhali, hizi mvua zinazonyesha, wasije tena watoto wengine wakaendelea kufa tukaendelea kupata maafa katika Mkoa wetu wa Mara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna miradi viporo mingi tu. Kwa mfano, Bunda – Kisoria, Makutano – Sanzate, Mugumu – Tabora B, zinahitajika fedha kuweza kukamilisha miradi hii viporo. Mpaka leo hii hakuna pesa yoyote ambayo imeshapelekwa na barabara zile zimekaa tu, hatuelewi hatma ya hizi barabara. Tunaomba Mheshimiwa Waziri aone umuhimu wa kwenda kumalizia miradi hii viporo iweze kukamilika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilivile kuna *round about* Tarime. Ile *round about* ya Tarime Mjini mara nyingi imekuwa ikisababisha madhara. Imesababisha ajali nyingi sana. Naishauri tu Serikali ihakikishe eneo lile inaweka angalau zile taa za kuongoza wale watu wa magari, hata wale waenda kwa miguu. Kwa mfano, kama ile barabara ya pale Mwenge kwenda Mjini, Mwenge kwenda Mikocheni, Mwenge kwenda Kawe, Mwenge Kwenda Ubungo, ni taa ambazo zinaongoza vizuri sana. Naishauri sana Serikali ione umuhimu kwa sababu ile *keep left* pale ni ndogo na eneo lile ni dogo sana. Naomba na kuishauri Serikali ituwekee taa eneo lile.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukienda Uwanja wa Ndege wa Musoma, ule uwanja ni mdogo. Sasa hivi wanataka kuutanua ule uwanja uwe mkubwa, lakini kuna wale watu ambao wamezunguka lile eneo la Uwanja wa Musoma na wale watu walishawekewa X toka mwaka na miezi mitano mmoja sasa hivi. Wale watu walishafanyiwa tathmini, lakini wale watu walifanya tathmini walifanya bila kuwashirikisha wananchi husika. Mpaka sasa wale wananchi hawajui hatma yao kwa sababu wanatembea tu hati, hawawezi kwenda benki kukopesheka wala kufanya kitu chochote cha maendeleo yoyote katika maeneo yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba na kuishauri Serikali wakarudie kufanya tathmini kwa kushirikiana na wananchi wa eneo husika ili mtu anapofanyiwa tathmini ajue nyumba yake inafanywa tathmini kwa kiasi gani? Kwa sababu mnapofanya tathmini tu na kuondoka bila kumwambia mhusika kwamba tathmini tumefanya nyumba yako ina thamani ya kiasi fulani kwa kweli inasikitisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naenda upande wa *TBA*. Kwa kweli *TBA* hawafanyiwi ushindani na makampuni binafsi, ndiyo maana kazi zao zimekuwa ni *substandard*. Matokeo mengi tunaona kazi nyingi za Serikali zinafanywa na *TBA* na kazi zao nyingi zimekuwa za kiwango cha chini sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naongea hivyo kwa sababu gani? Kuna zile nyumba za mradi wa Bunju. Ule mradi, yaani kwa ushauri wangu mdogo tu, sana sana wangeanza kuweka *social services* kwa kuanza kuweka zahanati, wakaweka shule, wakaweka barabara nzuri ili mtu anapokwenda kule kwa sababu zile nyumba ziko pembezoni sana, angalau hata ziwe ni nyumba za kufikika kwa urahisi.

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. JOYCE B. SOKOMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, zile nyumba malengo ilikuwa ni kwa ajili ya wafanyakazi na wafanyakazi wengi wamehamishiwa Dodoma, kwa maana hiyo zile nyumba zinakaa tu hazina wapangaji. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Kengele ya pili ilishagonga Mheshimiwa, ahsante sana.

Mheshimiwa William Mganga Ngeleja atafuatiwa na Mheshimiwa Zacharia Issaay na Mheshimiwa Joseph Mhagama ajiandae.

MHE. WILLIAM M. NGELEJA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ili nichangie hoja iliyoko mbele yetu. Awali ya yote kabisa naungana na wenzangu kuiunga mkono hoja hii ya Mheshimiwa Waziri, *Engineer Kamwelwe*. Pamoja na hayo, nitumie nafasi hii kumpongeza ye, kuwapongeza Waheshimiwa Naibu Mawaziri; Mheshimiwa *Engineer Kwandikwa* na Mheshimiwa *Engineer Nditiye*, Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu na Watendaji wote katika taasisi ambazo ziko chini ya Wizara hii kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo imejitokeza hapa na mjadala unavyoonyesha, ni kwamba Wizara hii imepata fedha nyingi na imekuwa ikiendelea kupata fedha nyingi kwa sababu ni mhimili wa uchumi wetu kwa kadri ambavyo tunaelekea kuifikia nchi ya viwanda. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajadili hoja iliyoko mbele yetu tukiwa tuko katikati kama Taifa kwenye majonzi ya msiba wa Marehemu Mzee Mengi na tunafahamu kwamba jana amelazwa katika makazi ya milele, nasi ndio tunasubiri ratiba yetu kwa kadri Mwenyezi Mungu atakavyotujalia. Kwa hiyo, natumia nafasi kuungana na Watanzania wenzangu kutoa pole kwa familia ya Mzee Mengi, ndugu na jamaa, lakini kuungana na Watanzania kumwombea Mzee Mengi aendelee kulazwa mahali pema Peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie kuhusu Jimbo la Sengerema. Kitabu hiki ambacho kwa ujumla wake kinaomba karibu shilingi trillioni tano, Sengerema ni mojawapo ya wanufaika katika miradi ambayo imekuwa ikitekelezwa na ile ambayo iko katika hatua za mwisho kabisa kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwaarifu wananchi wa Jimbo la Sengerema kwamba ile barabara yetu ya kutoka Sima kwenda Ikonini inayosimamiwa na *TANROADS* Mwanza, Barabara yetu ya kutoka Sengerema kwenda Ngoma A zinaendelea vizuri. Pia ile ya Sima – Ikonini, Mkandarasi wetu *KASCO* anamalizia kipande cha kutoka Sengerema kwenda Nyamazugo. Atakapokimaliza kile, anahamia Sima kwenda Ikonini kuunganisha na Jimbo la Geita Vijijini. Kwa hiyo, ni kazi inayoendelea vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiingia kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Serikali imetukumbusha kupitia hotuba hii kwamba maandalizi ya bajeti hii yamezingatia pia Ilani ya Chama cha Mapinduzi, maelekezo ya Viongozi Wakuu pamoja na Mpango wetu wa Miaka Mltano. Sasa kwenye ukurasa wa 60 pale wa Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi kuna barabara inayotajwa pale ya Kamanga – Sengerema kilometra 35.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kwani hatua za awali zilishafanyika; upembuzi na usanifu wa kina tayari na sasa nawaarifu Wana-Sengerema kwamba wajiandae kwa sababu mipango yote sasa imeshahamia Serikalini na hasa kwa Mtendaji Mkuu wa *TANROADS*, Engineer Mfugale. Nimekuwa na mawasiliano naye, iko kwenye mpango, tunasubiri muda muafaka utakapofika, itatangazwa tenda kwa ajili ya kupata mkandarasi kuanza ujenzi wa lami kwa barabara ya Kamanga – Sengerema na ule mchepuko wake wa Katunguru kwenda Nyamazugo, kilometra 21. Kwa hiyo, naishukuru sana Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu pia kwamba upembuzi yakinifu unaendelea na usanifu wa kina kwenye barabara ya Nyehunge kuja Sengerema ama Sengerema – Nyehunge, kilometra 78. Napo tunaishukuru Serikali kwa sababu ni kazi inayoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilimsikia Mheshimiwa Maige asubuhi na Waheshimiwa Wabunge wengine wamezungumzia barabara inayotunganisha mikoa mitatu. Nazungumzia barabara ya Busisi kwenda Buyagu – Ngoma A mpaka Nyang'hwale ambalo ni Jimbo liliopo ndani ya Mkoa wa Geita na kuelekea Jimbo la Msalala ambako ni Mkoa wa Shinyanga. Hii ni barabara muhimu na tunaombaa Serikali iendelee kujipanga vizuri na sisi tunaikumbusha ili kwamba tunapofika mwaka kesho, basi ama maandalizi yake yawe yameshamiliaka ama ujenzi uwe umeanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa *Engineer Nditiye*, kwa kazi nzuri aliyofanya alivyotembelea Jimbo la Sengerema kuhusu mawasiliano, ambako bado kuna upungufu, nafahamu kwamba Mheshimiwa Kwandikwa amefika na Mheshimiwa *Eng. Kamwelwe* kama Waziri amekuwa akipita maeneo mbalimbali pamoja na wasaidizi wake. Pia kwa hili natambua kazi kubwa ambayo Mheshimiwa *Engineer Nditiye* alifanya alipofika Jimbo la Sengerema kuhusu maeneo ambayo yana upungufu wa mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Daraja la Kigongo – Busisi, daraja kubwa mionganoni mwa madaraja makubwa kabisa katika Bara la Afrika linajengwa pale. Sasa hivi mkandarasi wachambuzi wanaendelea na tathmini ya kumpata kwa sababu tenda imeshafunguliwa. Tunaipongeza Serikali tunasema ahsanteni sana kwa kazi kubwa inayofanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengine ambayo nilitaka niyakumbushe, wenzangu wamezungumza. Ukiangalia jiografia ya nchi hii, naomba ATC na ninaamini kwamba wanasililiza hapa, ile mipango yenu ya kuanzisha *route* nydinge kutokea hapa Dodoma kwenda Mbeya na kuanzia hapa Dodoma kwenda Mwanza kwa maana ya kuhudumia Mikoa ya Kanda ya Ziwa ifanyike haraka, kwa sababu tunaamini kwamba itarahisisha sana kuokoa rasilimali fedha nydingi inayotumiwa na watumishi wanaokuja hapa kama Makao Makuu ya nchi kwa ajili ya kufanya shughuli za kikazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona kuna ujenzi wa meli unaendelea, Ziwa Victoria na maziwa mengine, lakini viwanja vyatundege ikiwemo Kiwanja cha Mwanza, tunasema ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo moja nataka nizungumze. Tuna miradi mikubwa na ukisoma Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ukurasa wa 67 tulipokuwa tunajadili, katika ajira ambazo zimezalishwa mpaka mwezi wa pili mwaka huu tumeambiwa kwamba asilimia 66 imetokana na ajira zilizotokana na uwekezaji wa Serikali kwenye miradi mikubwa, hasa ujenzi wa miundombinu na asilimia 34 imetokea *Private Sector*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka niiombe Serikali katika hili, wanaofuatilia mitandaoni, mwezi wa Pili mwishoni pale kulitokea taarifa iliandikwa na mwandishi mmoja akisema asichokijua Mheshimiwa Rais kuhusu ujenzi wa *SGR*. Alichokuwa anasema ni unyanyaswaji wa

Watanzania wanaopata kazi kumsaidia mjenzi mkuu wa miradi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumze hili kwa kina kwamba katika fedha ambazo tunaziingiza katika miradi mikubwa hii, lazima tuwe na utaratibu wa kuwasaidia Wakandarasi wetu wadogo ambao ni *subcontractors* katika *main contractors* hawa. Yule mwandishi aliandika akasambaza mitandaoni akataja na jina lake na namba yake ya simu. Mtu mwingine anaweza kusema tusifuate mambo ya mitandao, lakini mtu anapokuwa ameandika na akataja kinachowakera Watanzania, kinachowasibu katika maeneo hayo akaweka na jina lake, ule utayari wake lazima utushtue sisi na liwe ni fundisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa *Eng. Nditiye*, namtaja kama Naibu Waziri kwa sababu nilisikia alifuatilia kwa kile ambacho wananyanyaswa wale *subcontractors* kwenye ujenzi wa miradi yetu na hasa mradi wa *SGR*. Wanaingia katika kazi hizo, wanapewa kazi malipo hawalipwi ndani ya muda, matokeo yake wanafilisika kwa sababu wameingia katika ujenzi na wengine wanategemea mikopo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, yule bwana mpaka alitaja baadhi ya makampuni. Sasa sitaki kuwa *specific* nitaje baadhi ya makampuni kwa sababu sina *interest* yoyote. Ninachotaka niseme, kama Taifa, kwa fedha ambazo tunaziwekeza kwa sababu ni za walipa kodi, lazima tuziandalie utaratibu mzuri wa kuwasaidia Watanzania wenzetu ambao wameingia kule kusaidia. Kwa kadri wanavyonufaika hawa, ndivyo Taifa litakavyokuwa linanufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, chagizo langu ni kuiomba Serikali tuandae utaratibu mzuri wa kusimamia na hasa kuratibu wale *subcontractors* kwa maana ya *local content*, wale Watanzania wenywewe hasa ili manufaa haya ya miradi mikubwa tuyaone kwa uhakika na yawe na madhara chanya katika uhai wa uchumi wetu.

Mheshimiwa Niabu Spika, yapo mambo mengi yamekuwa yakizungumzwa hapa. Limezungumzwa deni kuhusu *TRC* na Serikali kwa ujumla wake na baadhi ya wachangiaji. Mimi sitaki kujibu, lakini ninachotaka kusema, tuwe makini sana. Unapozungumzia deni linaloihusu *TRC* inawezekana kukawa na deni ambalo linahusu Serikali kwa ujumla kutokana na mkopo ambao tulikopeshwa na Serikali ya Uchina kwa maana ya ujenzi wa Reli ya *TAZARA*, lakini siyo malimbikizo kwa ujumla wake kwa fedha ambazo zimetajwa hapa kama vile ndiyo zinazostahili kwenda kwa wastaafu au wafanyakazi. Kwa hiyo, naomba nitahadharishe, tuyachambue kwa kina haya tusije tukapeleka taarifa potovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja na Wanasengerema wajlandae kunufalka na mipango mizuri ya Serikali ambayo imeoneshwa hasa katika ujenzi wa miundombinu ya barabara. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Zacharia Issaay, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Mhagama, Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa ajiandae.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwanza nitoe shukrani za dhati kwa Rais mpendwa Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, Rais wa Awamu hii ya Tano, kuitia salamu zao kwangu mimi Mbunge wa Jimbo la Mbulu Mjini. Kwa kweli ni Serikali iliyofanya kazi kubwa sana katika Tanzania hii na hasa nikizungumzia Jimbo la Mbulu Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipoingia Bunge hili nilikuwa mkorofi sana, nilikuwa nachangia vibaya pia, lakini nilikuwa nafikiri ni lini matatizo haya ya wananchi wa Mbulu yatatatuliwa. Yamefanyika kwa kasi kubwa sana. Nitoe salamu za shukrani pia kwa Mheshimiwa Waziri na timu yake nzima, Naibu Mawaziri na watendaji wote Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani hizi kwa sababu kulikuwa na mambo magumu sana yalikuwa hayafanyiki, lakini sasa yanafanyika. Nashukru sana kwa timu hiyo kufanya kazi toka walivyoingia madarakani pamoja na *TANROADS*. Barabara za Halmashauri ya Mji wa Mbulu zilikuwa hazipitiki nyakati nyingi za mvua na akina mama walikuwa wanapata shida. Kwa sasa ni miaka mitatu barabara hizo zinapitika nyakati zote pamoja na mvua hizi ambazo zinanyesha za mwezi wa Nne hadi wa mwezi wa Sita; na ni historia kubwa kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kulikuwa na daraja la Magara. Natoa shukrani za dhati kwa Katibu Mkuu ambaye sasa ni Katibu Mkuu wa Wizara ya TAMISEMI. Daraja la Magara ni daraja lenye upana wa mita 84, siyo rahisi ingejengwa kwa sababu mbele ya hilo daraja kuna mlima ambapo wewe Mheshimiwa Naibu Spika, ullipita, mlima wenyewe kona 130, haupo Tanzania nzima kwa maeneo ambayo nimetembea, lakini leo hilo daraja linajengwa liko katika hatua za mwisho. Naishukuru sana Serikali, nasema ahsanteni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ule mlima uliokuwa umepanda siku ile ulipokuja Mbulu, sasa karibu robo yake au asilimia 30 ya mlima una zege. Kwa hiyo, usiposhukuru wakati fulani utaonekana na wewe huna shukrani na hutambui jitihada za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile mnara uliojengwa katika Tarafa ya Nambis ambako wamehangai sana Wabunge wenzangu waliotangulia, lakini Tarafa hiyo ambayo ndiyo asisi ya khabila letu kule Nambis, sasa hivi kuna Halotel wananchi wanawasiliana. Naishukuru kwa dhati sana Serikali ya Awamu ya Tano pamoja na maboresho yoyote yaliyofanyika katika Mji wa Mbulu hadi sasa yanayoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije sasa kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa *Eng.* Kamwelwe. Utakuwa Waziri wa kwanza kuweka historia katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu kwa kilometra hizo 50 unazofikiri za kutoka Mbulu kwenda Haydom.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuna namna nyingine. Jimbo la Mbali Mjini tunapakana na Jimbo la Karatu, tunapakana na Jimbo la Babati, tunapakana pia wakati fulani na Jimbo la Vijijini, lakini eneo hilo la kilometra kama 389 inayozungumzwa, eneo letu ndiyo tuko katikati tumezengukwa na ukanda wa Bonde la Ufa ambako hakuna njia nyingine zaidi kutokea Haydom kuja Mbulu ama kutokea Karatu - Mto wa Mbu kuja Mbulu. Kwa hiyo basi, hizo kilometra 50 ni muhimu sana, ni za thamani. Mheshimiwa Waziri tunakushukuru kwa mpango wako unavyofikiri wa hata hizo kilometra 50 ili baadaye tuunganishwe kutoka Karatu mpaka kule Shinyanga kutokana na umbali huu kupunguzwa kwa awamu kwa sababu ya uwezo wa Serikali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme ninaishukuru pia Serikali na ninaiomba isibadilishe mpango wake huu wa usanifu wa barabara ya Mbuyu wa Mjerumani – Magara – Mbulu ambapo barabara hiyo inaunganisha Mji maarufu wa Arusha, lakini pia inaunganisha Makao Makuu ya Mji wetu wa Babati. Kwa hiyo, ni shukrani pekee tunazitoa, lakini pia tunaomba mpango huu uzingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawaomba sana Wizara hii pia iangalie utaratibu wa kuweka minara ile iliyopanga katika bajeti ya mwaka huu unaoisha Juni katika Tarafa ya Nambis ambako tulipagiwa minara. Basi tunamwomba Mheshimiwa Waziri na timu yake utekelezaji wa ile minara ufanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunaomba watutumie wataalam wa viwanja vyta ndege kwani Mkoa wa Manyara hauna uwanja wa ndege, kwa sababu sisi tulio juu ya bonde la ufa kwa maaana ya Mji wa Mbulu huwa usafiri wetu wa dharura ni mgumu. Kwa hiyo, hata tukipata uwanja wa ndege kule Babati, Manyara utasaidia kuunganisha mkoa wetu na mikoa mingine ya nchi kwa kadri ambavyo itawezekakana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hii ni kubwa, ukisoma kitabu cha bajeti kwa kadri ambavyo fedha hizi kidogo

kidogo ambazo zimewekwa ili kutatua changamoto zilizoko, zipo jitihada kubwa zimefanyika katika kila Wizara katika Jimbo la Mbulu Mjini ndiyo maana wakati fulani nanyamaza, nasema nitoe tu salama za shukrani lakini zaidi kuomba omba Serikali ihakikishe basi ni kwa namna gani hatua hii inayokusudiwa ya barabara hizi za Dongobeshi - Dareda kupata usanifu na Mbulu - Magara - Mbuyuni kupata usanifu, lakini na hizo kilomita 50 za kwenda Haydom, ambapo itakuwa imepunguza, tutakuwa na kipande cha Mbulu kwenda Karatu na kipande Haydom kwenda Shinyanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, eneo hilo ni muhimu sana, naona anasemeshwa, lakini hili ni ombi kwa niaba ya Serikali na nasema Waziri huyu ni msikivu atakuwa ameweka historia, barabara hiyo inaweza ikaitwa kwa jina lake, ikaitwa Kamwelwe *Road* kwa sababu illikuwa haipo, haipatikani, sasa angalau kuna dalili, tunaishukuru Serikali na tunamshukuru na Rais. Naomba Mheshimiwa Waziri afanye ziara alikataa kupita Magara, alisema kona hizo ni nydingi anaogopa, akapita Karatu, safari hii akija apite Magara ili aone huo mlima tunaoulalamikia na hiyo barabara ya Magara ilivyo ngumu na Wanambulu wakiillilia wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana Serikali na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Mhagama, atafuatiwa na Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa na Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka ajiandae.

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi. Kwanza kabisa nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Manaibu Waziri wote wawili kwa ushirikiano ambao wanatupa wananchi wa Madaba kwenye masuala yote ya barabara na mawasiliano na nitoe salam za pekee kutoka kwa wananchi wa Ifinga ambao tangu nchi hii ipate uhuru hawakuwa na mawasiliano kabisa, walikuwa wanasafiri zaidi ya kilomita 30 kwenda kupiga simu,

Iakini sasa tatizo hilo limekwisha, tunawashukuru sana. Pia watu wa Madaba wanamkumbuka sana Mheshimiwa Waziri, alianza utumishi Madaba na leo ameshirikiria Wizara muhimu sana katika Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiifuatilia historia ya Madaba utagundua kwa nini ina matatizo makubwa ya barabara, Madaba ilikuwa ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Songea miaka minne iliyopita. Katika kipindi hicho, barabara ambayo ilikuwa inahudumiwa na Serikali kwa kupitia fedha za halmashauri ilikuwa kilometra 48 tu na sasa Madaba ni Halmashauri ya Wilaya na ni Jimbo na kilometra zinazohitaji kuhudumiwa kwa maana ya mtandao wa barabara Madaba umefikia kilometra 642. Mpaka sasa bajeti tunayopata Madaba kwa kupitia *TARURA* ni ya kilometra 48 tu, haizidi shilingi milioni 400.16. Madhara yake barabara nydingi za Madaba ni mbovu hazifai na hazipitiki katika kipindi cha masika na hata kiangazi bado kuna makorongo mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo barabara za kimkakati ambazo naamini Mheshimiwa Waziri tumeanza kuzungumza kwenye vikao vyetu ambavyo siyo rasmi na yeze, Iakini hapa naongea mbele ya Bunge hili Tukufu kumwomba akubali kupokea baadhi ya barabara zitoke *TARURA* ziende *TANROADS*. Moja katika barabara hizi ni hii barabara ya kutoka Wino kwenda Matumbi - Ifinga. Barabara hii inaunganisha Mkoa wa Ruvuma na Mkoa wa Morogoro na barabara hii ndiyo barabara ambayo itachangia sana kwenye kuipata Tanzania ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ninavyozungumza hekta za ardhi zimewekeza kule kwa ajili ya kilimo cha miti na muda si mrefu kama Mheshimiwa Waziri atatusaidia, hawa watani zangu wa Iringa tutawapita kiuchumi. Uchumi wetu utafafana na uchumi unaouona Mafinga leo kwa kutokana na miti, Iakini kinachotuangusha ni hii barabara. Hii ni barabara ya kimkakati, ni barabara yenye uchumi mkubwa sana. Barabara hii ina urefu wa kilometra 57, pia inaunganisha na mbuga ya Selou ambako tayari kuna vitalu ambavyo wawekezaji wamewekeza kwenye kuwinda na kwenye utalii.

Kwa hiyo ina mchango mkubwa sana kwenye uchumi na hatuwezi wana Madaba kushiriki kwenye uchumi wa viwanda kama barabara hii Mheshimiwa Waziri hatakubali kuipokea. Namwomba sana kwa niaba ya wananchi wa Ifinga akubali kuichukua barabara hii iende *TANROADS* ili ijengwe kwenye viwango tunavyovitaka na matokeo yake ni uchumi ambaa utatokana na kazi kumbwa inayofanyika katika maeneo yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ukiangalia kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri aghalabu utakuta mahali pameandikwa Madaba, najua kwa sababu labda Madaba barabara zake ni fupi na ni barabara ambazo wanadhani *TARURA* itazikamilisha, lakini kiuhalisia sivyo hivyo, *TARURA* hawana fedha za kuweza kumaliza zile barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo barabara nyingine ya kimkakati inayounganisha Madaba na Njombe kwa kuititia Kijiji cha Maweso na kama Mheshimiwa Waziri alifanya kazi Madaba wakati ule, ili uje Dar es Salaam ilikuwa unapita Maweso unaenda Mikongo unatokea Kifanya unakwenda Njombe, ile barabara ya zamani, barabara kubwa ya kutoka Dar es Salaam kwenda Madaba, kwa sasa unaweza kwenda mwisho Maweso, baada ya pale huwezi kuendelea na ile barabara. Namwomba Mheshimiwa Waziri barabara hii pia aichukuwe kwa maana ya Mfuko wa *TANROADS* aihudumie ili kukuza uchumi wa wananchi wa Madaba na wananchi wa Maweso, lakini wananchi wa Njombe kwa sababu hilo ndilo eneo kubwa ambalo lina ardhi kubwa ya uzalishaji, lakini pia lina matukio ya kihistoria. Barabara hii ina kumbukumbu za kudumu za mashujaa wa vita ya Uganda...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa
Mzungumzaji)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mhagama muda wako umekwisha.

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makof)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa atafuatiwa na Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka na Mheshimiwa Maftaha Nachuma ajiandae.

MHE. MAHMOUD H. MGIMWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushurkuru sana kwa kunipa nafasi. Pia naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Waziri, Mheshimiwa Kamwelwe; Naibu Waziri, Mheshimiwa Nditiye pamoja na mtani wangu kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hii ya miundombinu. Vile vile naomba nichukue fursa hii kusema kwamba naungana na taarifa ya Kamati, taarifa ya Kamati imekuwa nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mionganoni mwa maoni ya Kamati, imeelekeza kwa Serikali na Wizara kwamba umefika wakati kuwe kunatengwa bajeti ya kujenga barabara kwa kiwango cha lami kwa barabara zinazounganisha mkoa na mkoa. Katika Jimbo la Mufindi Kaskazini nina barabara kubwa tatu; barabara ya kwanza inaanzia Kinyanambo C, Itimbo mpaka Kihansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ni muhimu sana kwa uchumi wa Wilaya ya Mufindi, ndiyo kwenye bwawa la Kihansi ambalo linatoa umeme *megawatt* 180, lakini cha kusikitisha barabara hii haina hata kilometa moja ya lami. Pia barabara hii inaunganisha Mkoa wa Iringa na Mkoa wa Morogoro kwa maana ya Wilaya ya Mufindi na Wilaya ya Kilombero, sasa ufile wakati Serikali ione kuna haja ya kupeleka barabara ya lami kwenye eneo hili ambako kuna umeme wa uhakika na siyo umeme tu, hata eneo mkubwa wa msitu wa *Sao Hill*liko katika Tarafa ya Kibengu. Kwa hiyo, uchumi mkubwa katika Jimbo la Mufindi Kaskazini unalala katika barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ni eneo la barabara kutoka Kinyanambo A, Isalavanu, Igombavanu, Sadani mpaka Ludewa, barabara hii ina kilomita za mraba 151. Katika llani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005, sisi CCM tulisema barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami, tukarudia 2010 na tukarudia 2015 -2020, lakini cha

kusikitisha hakuna hata kilomita moja ya lami iliyojengwa katika eneo hili. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha aje hapa atueleze sababu zipi zinapeleka barabara hii isijengwe kwa kiwango cha lami. Mwaka 2009 ilifanyika tathmini ya kuangalia zile nyumba zote ambazo ziko kando kando ya barabara ambazo mpaka leo wananchi wamekaa mkao wa kula lakini miaka kumi imepita, hakuna hata mwananchi moja aliyelipwa fidia. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha atatuambia wale watu waendelee kusubiri au kuna utaratibu mwingine ambaao Serikali imejipanga kuhakikisha watu wanalipwa fidia? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara nytingine ambayo ni barabara muhimu inaunganisha tena Mkoa wa Iringa na Mkoa wa Morogoro, ni barabara inayoanzia Kijiji cha Mtili, Ifwagi, Mdabulo, Ihanu, Isipii mpaka *TAZARA* mpaka Mlimba. Barabara hii ina kilometra za mraba 136, lakini barabara hii haipitiki kabisa, ni tatizo katika Jimbo la Mufindi Kaskazini. Kwenye barabara hii nako kuna uchumi mkubwa, kuna bwawa ambalo linatoa umeme *megawatt* saba, barabara hii kuna uchumi wa chai, uchumi wa msitu na uchumi wa pareto, lakini barabara haipitiki kabisa. Sasa ni vyema Serikali ikaona kwamba kuna haja barabara hii kuihamisha kutoka *TARURA* kuipeleka *TANROADS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TARURA* hawana uwezo hata wa kutengeneza kilomita 20 kwenye barabara hii. Kwa hiyo hali imekuwa mbaya, hivyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri alione hili. Mheshimiwa Rais alipokuwa Waziri wa Miundombinu alikuwa ameshaanza mkakati wa kutaka kuihamisha barabara hii kuipeleka *TANROADS*, lakini hilo zoezi limekufa ghafla na sielewi tatizo liko wapi.

Vilevile Mheshimiwa Rais alipokuwa amekuja pale Mufindi aliahidi kwamba atahakikisha yale maeneo yenye utata kama barabara hii inachukuliwa na kuwa ya *TANROADS*. Kwa hiyo namwomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha atuambie anatusaidiaje watu wa Mufindi ili tuendelee kuwa na uchumi uliokuwa imara.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ambalo nataka kulizungumzia ni eneo la mawasiliano. Katika Jimbo la Mufindi Kaskazini kuna matatizo ya mawasiliano katika Kata tatu au nne hivi; ya kwanza Kata ya Ikweha hakuna mawasiliano kabisa; pili Kata ya Mapanda hakuna mawasiliano kabisa; tatu Kata ya Ihanu; na nne Kata ya Mpangatazara. Tumekuwa tunauliza maswali mara kwa mara hapa na Waheshimiwa Manaibu Waziri wameniahidi mara nydingi kwamba watakuja kutembelea na kuja kuangalia matatizo ya mawasiliano katika hayo maeneo, lakini mpaka leo hawajafika. Sasa nataka wanapohitimisha hapa wanihakikishie mbele ya Bunge lako Tukufu, ni lini watakuja kwenye maeneo haya kusudi wawze kujua matatizo ya mawasiliano katika maeneo haya...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa, Kengele ya pili imeshagonga.

MBUNGE FULANI: Sijui wanaweka dakika tatu yaani hii kengele.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka atafuatiwa na Mheshimiwa Maftaha Nachuma na Mheshimiwa Pascal Haonga ajiandae.

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia kidogo katika Wizara hii ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijatoa mchango wangu kwa ujumla naomba tu nizungumze kidogo kuhusu sheria iliyounda mawakala ikiwepo *TANROADS* maana nitazamia kwenye *TANROADS*. Kifungu namba 12(2)(a) cha Sheria ya Wakala wa Serikali Na. 30 ya mwaka 1997 kinataka wakala wote wafanye kazi kibashara na mapato yao yatoshe kulipia matumizi yao. Hii sheria imetekelizwa kwa kiwango kidogo sana. Kwa mwaka 2015/2016, mapato ya

ndani ya mawakala wengi yalishuka kutoka asilimia 45 hadi kufikia asilimia 16 mwaka 2020. Ni mawakala wachache tu walioweza kujitegemea, lakini mawakala wengi ikiwemo *TANROADS* wanetegemea Serikali kwa kiwango cha asilimia 84.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka Waziri atakapokuja kuhitimisha atueleze tatizo ni nini ambalo linafanya Wakala wa Barabara *TANROADS* wasiweze kujitegemea angalau kwa kiwango kikubwa. Kama tatizo ni sharia, basi sheria iangaliwe upya, lakini kama si sheria tuambiwe tatizo ni nini. Pia *TANROADS* kwa mwaka uliopita unaoishia Juni walikuwa na deni la bilioni 833 na katи ya hizo bilioni 57 ni riba ambayo inatokana kutowalipa wakandarasi kwa wakati. Tatizo hili siyo la *TANROADS*, ni Wizara ya Fedha ambayo imeshindwa kuapelekea hela kwa wakati, matokeo yake *TANROADS* wanadaiwa na wakandarasi kiasi kwamba ukiangalia riba ya bilioni 57 ni kubwa sana kiasi ambacho ingeweza kutengeneza barabara nyingi. Kwa hiyo, niseme kwamba sisi tuiambie Serikali inakwamisha sana wakala hawa kufanya kazi, maana nia ya kuanzisha hawa Wakala ni ili kazi zetu ziende kwa tija, lakini unapowakwamisha inapelekea kuonesha kwamba mawakala hawa hawafanyi kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba niingie kwenye hoja yangu ambayo naongea kwa niaba ya Wabunge watano kuhusu barabara ya Same - Kisiwani – Mkomazi. Barabara hii ambayo inatumiwa na Mbunge wa Same Magharibi, Mheshimiwa Mathayo ambayo pia inatumiwa na Mbunge wa Mkinga, Mheshimiwa Kitandula; Mheshimiwa Mnzava wa Korogwe Vijijini; Mheshimiwa Shangazi wa Mlalo na mimi mwenyewe. Ni barabara ambayo ina tija sana kwa Taifa kama ingetengenezwa kwa kiwango cha lami. Ni muda mrefu sana barabara hii tumeipigia kelele, tangu nilipoingia mara ya kwanza. Imeshafanyiwa upembuzi yakinifu mara tatu na mpaka mara ya mwisho nimeongea na *Engineer Mfugale* ambaye anaheshimika Kitaifa na Kimataifa, akaniambia alikuwa katika hatua ya mwisho ya kufanya *design*.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha ajabu barabara hii imetengewa milioni 300 kwa kilomita moja. Sasa hebu angalia barabara ambayo inatumiwa na Wabunge watano, wanaume wanne na mwanamke mmoja; wa CCM wane na wa CHADEMA mmoja; Viongozi wa Kamati za Kudumu wawili, bado Waziri haoni umuhimu kwamba hii barabara inategemewa na wapiga kura wengi wanaotokana na majimbo haya matano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli nasema barabara yoyote ukiitengeneza, unaangalia kwamba ina manufaa gani kwanza kiuchumi *because lazima kuwe na return to capital, return kwenye investment*, hatutengenezi barabara tu kumfurahisha mtu, nimeshaona barabara nyiningine inatengenezwa kutoka kata kwenda kata ikawekwa lami na ukiangalia *ina-produce* nini pale, inabeba watu wangapi. Nasema na ndiyo maana nimesema niangalie hii sheria ya kuunda mawakala ili tuje, je, tunafanya kazi kibashara au tunafanya kazi kihasara? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe, Tanzania tutokane na kufanya kazi kana kwamba sisi hatujali uchumi wetu, Rais Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, anajali sana kwamba nchi hii ipige hatua, tuingie nchi ya viwanda, ya uchumi wa kati, lakini kwa mtindo huu unampa kabarabara kamoja kadogo yaani kilomita moja unaangalia tija yake ni nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema *TANROADS* wamejitatihidi, lakini kuna barabara zimetengenezwa kwa kiwango cha kutisha kibaya mno, Kamati yangu ilitembelea barabara kutoka Dodoma kwenda Iringa, ilikabidhiwa miaka minne iliyopita, inatisha na nafikiri niliona kama imetengewa tena hela. Sasa kama barabara zetu kwa muda mfupi inaharibika inarudi kuanzia kutengeneza tena na hii iko katika *Great North Road*, lakini imetengenezwa kwa kiwango cha chini kiasi kwamba tunaonekana kwamba *laissez-faire*. Hivyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri tuangalie utengenezaji wa barabara zetu, ametoka kwenye Maji, ameletwa kwenye eneo lake la kujidai tunaomba aangalie sana wakandarasi alionao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama barabara zetu kwa muda mfupi zinaharibika inaanza kutengenezwa tena na hii iko katika *Great North Road* lakin imetengenezwa kiwango cha chini kiasi kwamba tunaonekana Watanzania ni *laissez-faire*. Naomba Mheshimiwa Waziri tuangalie utengenezaji wa barabara zetu. Mheshimiwa Waziri umetoka kwenye Wizara ya Maji umeletwa kwenye eneo lako la kujidai, tunaomba uangalie sana wakandarasi ulionao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimeona kule kwenye barabara hii ninayozungumzia ya Same - Kisiwani - Mkomazi mara nydingi inatengewa fedha ambayo mnaziita *Upgrading DSD*, labda mtanieleza maana yake, inatengewa hela lakini kila nikipita sijaona mahali ambapo pamfanyiwa *upgrading* hapo hapo hiyo *DSD* inatengewa hela. Kwa mfano, hiyo *upgrading DSD* shilingi milioni 175 na mwaka huu imetengewa shilingi milioni 200 lakin nikipita sioni mahali palipotengenezwa. Labda baada ye utanielimisha maana ya haya maneno ni nini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kibaya zaidi *unpaved roads* zinatengewa hela nydingi sana, shilingi milioni 848, mwaka jana shilingi milioni mia nane sijui ishirini na ngapi, mwaka juzi shilingi milioni mia nane na kitu. Sasa najiuliza, hivi kwa nini upeleke hela nydingi kwenye kuparura barabara wakati hela hizo hizo ungeweza kusema uziongezee utengeneze barabara ya kiwango cha lami? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli kuna mambo mengi ya kutafakari, muda wetu wa kuongea ni mdogo lakin nafikiri ifike mahali tufanye *analysis* kwamba hivi hizi barabara tunajenga kisiasa au tunajenga kiuchumi ili uchumi wetu upande? Tukijenga kiuchumi tutapata pesa kutokana na kusafirisha mazao ya kilimo na kusaidia sekta nydingine kama za afya na maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ambayo nairudiarudia imechezewa kwa muda mrefu sana. Naja haitengenezwi kwa kiwango cha lami, maana ni rahisi *ku-trace* lami inatengenezwaje lakin mkandarasi anapopita

anaiparura tu barabara hii kwa miaka yote na kila mwaka shilingi milioni mia nane arobaini na kitu, kwa kweli nafikiri kuna aina ya ufisadi ndani yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri atakapojuisha anieleze kwa nini barabara hii moja inawekewa pesa nyingi kwenye *unpaved road?* *I do not know* utaita *unpaved* nini lakini kwenye laki unaweka kilomita 1, kwenye ku-*upgrade* unaweka nusu kilomita lakini kwa shilingi milioni 200, maana yake ni nini? Mimi napenda nijue haya yote na hii pia ingetusaidia kuangalia kwa nini barabara hii ya Same, Same ina-control/39% ya Mkoa wetu wa Kilimanjaro lakini ndijo wilaya maskini kuliko wilaya zote za mkoa ule. Kwa hiyo, naomba barabara hii iangaliwe kwani Same ingesaidiwa ina sehemu kubwa ya ku-expand social economically hasa kwa upande wa kilimo lakini Same hiihii ndijo imewekwa pembezoni ...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Muda wako umekwisha Mheshimiwa, kengele ya pili imeshagonga.

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Maftaha Nachuma atafuatiwa na Mheshimiwa Paschal Haonga. Mheshimiwa Paschal Haonga ana dakika sita atafuatiwa na Mheshimiwa Edwin Sannda

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema nami niweze kuchangia Wizara hii ya Uchukuzi na Mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanza tu kwanza niseme kwa moyo wa dhati kabisa kwamba miundombinu ni jambo ambalo nchi za wenzetu, nchi zote za Ulaya na kule

Marekani watumwa walipelekwa nchi hizi kwa ajili ya kwenda kujenga miundombinu. Leo hii nchi za Ulaya na Amerika zimeweza kuendelea kwa sababu ya miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nieleze kwamba kwa kasi hii ambayo tunaiona ya ujenzi wa miundombinu Tanzania, Wizara hii imefanya kazi kubwa sana. Jambo la kipekee ambalo naweza kuzungumza pamoja na kwamba kuna miradi mingi sana sasa hivi imeanzishwa katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu na ni imani yangu kwamba baada ya miaka 10, 15 Tanzania tutafikia ule uchumi wa kati 2025 na kuendelea huko kama kasi ya miundombinu itaenda hivi hivi kama ilivyo hivi sasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala ambalo wenzangu wamezungumza na hasa taarifa ya Kamati imezungumzia kwa kina sana kwamba illi tuweze kuendelea hivi sasa na hata nchi za wenzetu kama niliviotangulia kusema waliwekeza kwenye miundombinu na hasa miundombinu ya reli. Kwa muda mrefu imekuwa ikizungumzwa takriban miaka mitatu hivi sasa kila mwaka katika vitabu vya bajeti inatajwa Reli ya Kati (*Standard Gauge*) ambayo hii inajengwa lakini Reli ya Kanda ya Kaskazini na Kanda ya Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Reli ya Kanda ya Kusini ni muhimu sana kiuchumi kwa sababu reli hii itaanzia Mtwara Mjini kuelekea Mchuchuma na Liganga ambako kuna makaa ya mawe na chuma. Hii reli kwa taarifa tulizokuwa nazo mpaka hivi sasa kwa sababu Serikali imejipanga kwenda kujenga kwa kutumia mfumo wa *PPP* (*Public Private Partnership*) na kuna wawekezaji wengi wameamua kujitokeza kuwekeza kwenye hii reli, mimi niishauri Serikali isiwe na kigugumizi cha ujenzi wa hii reli kwa sababu *economic viability* yake ni kubwa sana kuliko reli zote Tanzania.

Tunaomba Serikali itenye fedha za kutosha isiwe kila mwaka tunaelezwa kwamba upembuzi yakinifu umekamilika, pesa tunaenda kuzitoa sijui wapi, wapewe hawa wawekezaji ambao wako tayari kuwekeza katika hii Reli ya Kusini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, reli hii ikijengwa maana yake tunaenda kufufua ule mpango unaoitwa *Southern Development Corridor* yaani Maendeleo ya ule Ukanda wa Kusini. Tunaamini reli hii ikiisha kutokea Bandari ya Mtwara Mjini tutaenda kufufua uchumi na hata nchi zote za Ukanda wa Kusini watatumia reli hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana kwa sababu Serikali imeweka kwenye mpango kwa muda mrefu kazi iliyobaki ni kutekeleza. Tunahitaji Reli ya Kusini na hata taarifa ya Kamati imeeleza kwa kina sana kwamba reli hii inaenda kuleta uchumi mkubwa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wananchi waweze kuondokana na umaskini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo naomba kuzungumza ni suala hili la usafiri katika bahari zetu. Serikali imekuwa na kizungumkuti, siku zote Serikali haiwekezi kwenye uwekezaji wa meli katika Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka ya nyuma wakati si tunakua, sisi tunaishi kule Pwani Mtwara, tulikuwa tunatumia sana usafiri wa meli kutoka Mtwara kuelekea Dar es Salaam na maeneo mengine mpaka kule Zanzibar. Kama kweli tunahitaji kufufua uchumi wa Tanzania tusiwekeze kwenye kujenga tu barabara hizi tununue meli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tunazungumzia uwekezaji, kuna ile taasisi ya Serikali inaitwa *Marine Service* ambayo inajenga meli katika Maziwa Makuu. Neno *marine* maana yake ni bahari, kwa hiyo, nashauri sana Serikali inunue meli kwa ajili ya kusafirisha *cement* kutoka pale Mtwara, Mheshimiwa Dangote anatumia magari kusafirisha kwa njia ya barabara ya Kilwa na inaharibika sana. Kama Serikali ingenunuia meli au ingewekeza kwenye meli usafiri wa meli ni rahisi kuliko usafiri wowote duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule hakuna kutengeneza barabara, maji Mwenyezi Mungu kayaweka, kazi ya Serikali ni kusafirisha tu. Kwa hiyo, *cheapest transport* duniani ni usafiri

wa meli, kwamba Serikali ikiwekeza kwenye meli tunaamini kabisa barabara zetu za Ukanda ule wa Kusini hazitaharibika kwa malori makubwa makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine naomba sana Mtwara Mjini baadhi ya maeneo hakuna mawasiliano ya simu. Nimekuwa nazungumza kwa muda mrefu na nilimwandikia Naibu Waziri, Mheshimiwa Nditiye ananisikia, nilimweleza kwamba kuna maeneo ya Mtwara Mjini ambapo hakuna mawasiliano ya simu yaani ukifika kule mawasiliano hakuna. Maeneo kama ya Mkunja Nguo, Naulongo, Mkandala, Dimbuzi na Mwenge mawasiliano ya simu kule hayapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilimwambia Mheshimiwa Nditiye kwamba tunahitaji awekeze ili watu wa Mtwara waweze kupata mawasiliano ya simu kwenye maeneo haya. Baadhi ya maeneo ya pembezoni ya Mtwara Mjini tunahitaji minara ya simu ili wananchi waweze kuwasiliana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho, tunahitaji hizi ndege ambazo Serikali imeamua kununua za ATC zifike Mtwara. Taarifa tunazoambiwa kwamba Mtwara hakuna abiria si kweli, *Precision* kila siku asubuhi wanakuja Mtwara na kurudi na wanajaza iweje leo ATCwanatuambia kwamba eti Mtwara hakuna abiria. Sisi tunahitaji hizi ndege kwa sababu ni za bei nafuu, kazi yake ni kutoa huduma kwa wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wana-Mtwara tunahitaji ndege hizi tuweze kuzipanda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni ucheleweshaji wa miradi. Ni kweli kuna kasi kubwa ya uanzishwaji wa miradi ya barabara lakini wakandarasi wanacheleweshwa sana kupewa fedha zao. Kwa mfano, barabara ile ya uchumi ambayo inaanzia pale Mtwara Mjini - Mnivata - Tandahimba mwaka huu nimeona kwenye kitabu hapa kwamba zimeongezwa kilomita zingine 50 lakini hiyo kilometa 50 kutoka Mtwara Mjini - Mnivata zinasuasua sana kwa sababu yule mkandarasi hapati pesa kwa wakati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri, alikuwa anaafanya kazi kubwa sana akiwa kwenye Wizara ya Maji Mheshimiwa Nditiye, Mheshimiwa Kwandikwa rafiki yangu kabisa na amekitembelea kipande kile cha kutoka Mtwara Mjini – Mnivata mkandarasi anasua fedha hapati kwa wakati. Naomba mumpe fedha kile kipande cha barabara kiweze kuisha na kipande kuanzia Mnivata - Tandahimba na maeneo mengine yale tunaomba mwaka huu fedha zitoke kwa wakati yule mkandarasi aweze kumaliza ili na sisi barabara hii tuweze kuitumia. Hii barabara ndiyo chanzo kikuu cha uchumi, korosho zote zinapita kwenye barabara hii kutokea Tandahimba - Mtwara Mjini pale bandarini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara nyingine ni barabara ya ulinzi ambayo nimekuwa naizungumzia kwa muda mrefu ambayo inaanzia Mtwara Mjini – Tangazo – Mahurunga – Kitaya - Kiromba na ukanda ule wote mpaka Mozambique. Barabara hii ni muhimu sana kwa sababu ndiyo chanzo cha ulinzi wa Ukanda ule wa Kusini naomba nayo ipewe kipaumbele. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Paschal Haonga, dakika sita atafuatiwa na Mheshimiwa Edwin Sannda, Mheshimiwa Hasna Mwilima ajiandae.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na barabara zangu za Jimboni lakini na zile zinazounganisha mkoa na mkoa. Barabara inayounganisha mkoa mmoja na mwingine hili ni suala la kisera ambapo sera inataka zitengenezwe kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa sana na Mheshimiwa Silinde amezungumza lakini pia yuko Mbunge hapa wa Kwela amezungumza na nimekuwa nikizungumza mara kwa mara, kuna barabara hii ya kutoka pale Mloo - Kamsamba, Mloo kwa maana Jimbo la Mbozi, Mkoa wa Songwe kwenda Kamsamba, Wilaya ya Momba lakini pia kwenda Kwela, Mkoa wa Rukwa lakini pia kwenda sehemu moja hivi inaitwa Kasansa hadi Kibaoni kwa maana ya Mkoa wa Katavi. Barabara hii inaunganisha karibu mikoa mitatu ya Songwe, Rukwa na Katavi na ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti iliyopita walitenga fedha kwa ajili ya upembuzi yakinifu naona safari hii tena wametenga fedha kwa ajili ya upembuzi yakinifu, sasa huu upembuzi yakinifu hatujui mwisho ni lini kwa sababu miaka yote sasa wanatenga fedha kwa ajili ya upembuzi yakinifu. Barabara hii kwa sababu ya umuhimu wake, tulitegemea kwamba Serikali ingekuwa sasa imeshaanza kujenga hii barabara kwa kiwango cha lami kwa sababu tayari Daraja la Kamsamba lilishaisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili ambalo nalizungumza mazao yote yanayoingizia pato kubwa Taifa kama kahawa, mpunga, kwa maana ya mchele lakini pia ujumlishe mazao kama ufuta, alizeti na mazao mengine mengi sana ya misitu na kadhalika yanatoka kwenye eneo hilo.

Kwa hiyo, kutengeneza barabara hii kwa kiwango cha lami maana yake inaenda kuongeza kipato cha Mikoa ya Songwe, Rukwa, Katavi lakini pia pato la Taifa kwa ujumla. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ili Mheshimiwa Waziri kuacha alama Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, nadhani ni kuhakikisha kwamba barabara hii inatengenezwa kwa kiwango cha lami. Hakuna namna nyingine unaweza ukafanya kuwaaminisha watu wa Kanda za Nyanda za Juu Kusini kwamba kuna kazi imefanyika kama hii barabara itabaki kama ilivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Pinda alijitahidi sana barabara kutoka pale Tunduma - Sumbawanga, nadhani anaweza akajivunia. Sasa Mheshimiwa Waziri wewe unatoka Katavi sijui utawaambia nini watu wa Katavi, Rukwa na Songwe kwa sababu barabara hii ni muhimu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kuna barabara inayotoka Jimbo la Songwe kule kwa Mheshimiwa Mulugo kuna Kata inaitwa Magamba kuja Magamba ya Mbozi, kwa sababu kuna Kata mbili za Magamba, Mbozi kuna Magamba lakini pia Songwe kuna Magamba, watu kutoka Jimbo la Mheshimiwa Mulugo wanalazimika kupita Mbalizi kwa maana Mkoa mwingine wa Mbeya wakati Makao Makuu yako Mbozi pale ndani ya mkoa mmoja hakuna barabara inayounganisha kati ya wilaya ya Mbozi na wilaya ya Songwe. Kwa hiyo, hili ni Jambo ambalo kwa kweli Waziri atakapokuja hapa atuambie wanafanya nini kushughulikia changamoto hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine naomba nizungumze kuhusu suala la Wakala wa Ndege za Serikali kuhamishiwa Ofisi ya Rais Ikulu, Fungu 20. Naomba hapa Serikali iweze kuwa makini kusikiliza vizuri sana. Wakala huyu wa Ndege za Serikali kuhamishiwa *Vote 20*, ukiangalia majukumu ya Wakala wa Ndege za Serikali, moja ni kusimamia mikataba ya ukodishwaji wa ndege kwa kampuni ya ndege ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbili, kufanya matengenezo na ununuzi wa vipuli vya ndege za Serikali. Leo Ikulu inaenda kusimamia ununuzi wa vipuli vya ndege halafu haitakaguliwa imenunua vipuli wapi na kwa gharama gani hamna atakayekagua kwa sababu *Vote 20* haikaguliwi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kufanya matengenezo kwa maana kufanya ukarabati wa karakana ya ndege za Serikali. Yaani leo watafanya ukarabati wa karakana za Serikali maana yake hawatakaguliwa...

TAARIFA

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Haonga, subiri kidogo kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge anayezungumza hivi sasa kwamba Fungu 20 kama yalivyo mafungu mengine yote linakaguliwa na lina *Auditor Resident* kutoka Ofisi ya CAG. Kwa hiyo, hakuna sababu kwa nini Fungu hilo halikaguliwi, si kweli kwamba halikaguliwi. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Haonga unaipokea taarifa hiyo?

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Naibu Spika, anaposema Fungu 20 linakaguliwa, Wabunge mara kadhaa hapa tumetaka watuambie, kwa mfano *Vote 20* inahusu pia suala la bajeti yao ya Usalama wa Taifa, mbona Bungeni hapa hatujawahi kuambiwa kwamba Usalama wa Taifa wanakaguliwa kwa sababu nayo iko kwenye *Vote 20*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 20 maana yake hata CAG mwenyewe hatakagua na hatutajua nini kinafanyika. Bunge lako Tukufu halitajua fedha za walipa kodi, za wavuja jasho, wauza michichia, wauza nyanya zinazoenda pale kwenye ndege hamna atakayejua kwamba ni shilingi ngapi zinaenda pale na zinafanya kazi gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia Waziri atuambie kwa sababu wanasema jukumu lingine la kitengo hicho ni kulipia gharama za bima za ndege, hakuna atakayejua kwa sababu ni kwenye *Vote 20* ambayo haikaguliwi. Kwa hiyo, niseme tu kwamba Serikali katika vitu ambavyo wamebugi, kwa mfano, tunasema Serikali hii inafanya kazi na inajali kweli

kodi za Watanzania hii Wakala wa Ndege za Serikali wasiipeleke kwenye *Vote 20* ili Wabunge tuwe na uwezo wa kuhoji, Watanzania wajue fedha zao zinafanya nini na mwisho wa siku tujue kwamba tunasonga vipi mbele. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni kuhusu suala la *TBA*. *TBA* wanapewa miradi mingi sana.

TAARIFA

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Haonga, naona Waziri amesimama tena.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tena nirudie na Watanzania wote wasikie Fungu 20 linakaguliwa kama mafungu mengine. Kama Mheshimiwa Mbunge anayezungumza anao ushahidi kwamba Fungu 20 halikaguliwi alete ushahidi mbele ya Kiti chako Mheshimiwa. Si kweli hata kidogo Fungu 20 linakaguliwa. (*Makofii*)

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Naibu Spika...

NAIBU SPIKA: Ngoja kidogo Mheshimiwa Haonga.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Sawa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Haonga, ili tusizikosee Kanuni zetu nadhani umemsikia vizuri Mheshimiwa Waziri aliposimama mara mbili. Katika ule mchango wako kuhusu kukaguliwa ama kutokukaguliwa kwa *Vote 20* kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri nadhani umeyaelewa na matakwa ya Kanuni zetu pia unayafahamu.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Haonga tunaomba utunyooshe vizuri hayo maelezo yako kwa mujibu wa taarifa aliyoitoa Mheshimiwa Waziri.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niseme tu kwamba suala hili la Fungu 20 tunapozungumza kwamba halikaguliwi kwa mfano nisaidie kitu kimoja umeshawahi kusikia matumizi kwa mfano fedha zinazonda *T/C* kwa maana usalama wa taifa zikajadiliwa hapa Bungeni.

MBUNGE FULANI: Taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa kaboyoka ngoja tulinyoshe hili tunakupa fursa. Mheshimiwa Heche naomba unyamaze nazungumza. Mheshimiwa Heche naomba ukae nazungumza, nazungumza naomba unyamaze Mheshimiwa Heche, toka nje Mheshimiwa Heche naomba utoke nje Mheshimiwa Haonga ongea halafu nitampa yeye fursa ongea ulichokuwa unataka kuongea. Mheshimiwa Heche naomba utoke nje ukiwa umeshapewa hiyo taarifa ya kutoka nje usiende kuzungumza ukiwa humu ndani funga mlango nyuma yako ondoka. Mheshimiwa Haonga. (*Makofi*)

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kanuni zetu, kwa kanuni zetu tulizonazo Bungeni hapa mtu anayesema anapotosha Mbunge ndio anayomamlaka kwa maana ya nafasi yakuweza kuweza ukutuambia kwamba ushaidi ni huu kwa maana haikaguliwi. Ninajua kwamba hapa Bungeni hajjawahi kuna kuba baadhi ya vifungu havijawahi kuletwa hapa Bungeni kwa mfano kama suala la taarifa hizi za *T/C* kwa maana ya usalama wa Taifa hazijawahi kujadiliwa Bungeni hapa.

NAIBU SPIKA: Basi Mheshimiwa Kaboyoka.

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kama mwenyekiti wa PAC niweke taarifa vizuri, kwamba Fungu namba 20 linakaguliwa lakini hatujawahi kulikagua halijawahi kaguliwa. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimwa Wabunge tusikilizane Mheshimiwa Haonga ulikuwa unapewa taarifa na Mhehimwiwa Kaboyoka unaipokea taarifa hiyo.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niipokee taarifa ya Mheshimiwa Kaboyoka hapa na ninaomba niendelee baada ya kupokea.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jenista naomba ucae kidogo, naomba ucae kidogo nakupa fursa. Mheshimiwa Haonga umesema unaipokea taarifa ya Mheshimiwa Kaboyoka?

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema kwamba baada ya Mheshimiwa Kaboyoka kunipa taarifa nimeipokea na taarifa ya Waziri pia nimeipokea lakini kwamba haijawahi kuletwa hapa kwa maana ya haijakaguliwa muda mrefu.

NAIBU SPIKA: Sawa naomba ucae tusikie kanuni inayovunjwa. Mheshimiwa Jenista Mhagama.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu nikwenda kanuni ya 64(1) ambayo inaenda sambamba na kanuni hiyo ndogo ya (1)(a) inayokwenda sambamba na kanuni ya 63. Unapotaka kuzungumza Bungeni lazima uwe unasema ukweli na unakuwa na uhakika na kile unachokisema. Mheshimiwa Waziri wa Fedha ametoa maelezo fasaha hapa, *Vote 20* inakaguliwa, na *Vote 20* sio *Vote* ya Usalama wa Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mbunge ameendelea kusitiza kwamba wakala wa ndege za Serikali kuwekwa kwenye *vote 20* tunakwenda kuficha jambo kwa sababu *vote* hiyo haikaguliwi. Jambo ambalo si kweli kwa maelekezo ambayo tumepewa na Waziri wa Fedha. Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya *PAC* anasema *vote* inakaguliwa halafu akasema

wao hawajawahi kukagua lakini wao hawana mamlaka ya ukaguzi wa vote hizo kwa mujibu wa sheria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Mheshimiwa Haonga Mbunge anayechangia hoja hii afute kauli yake, na kama hataki kufuta kauli yake tunaomba alithibitishie Bunge hili kama kweli ana ushahidi. Suala ukaguzi ni kazi ya CAGsio suala la Mbunge kuthibitisha kwama *vote* imekaguliwa au hajjakaguliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

MBUNGE FULANI: Taarifa.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge naomba tusikilizane, Mheshimiwa Jenista Mhagama amesimama kwa mujibu wa Kanuni 64 ambayo inazungumza kuhusu mambo yasiyoruhusiwa Bungeni. Mheshimiwa Jenista ametoa hoja yake akieleza kwamba mchango wa Mheshimiwa Haonga kuhusu ukaguzi wa *vote* namba 20 namna alivyozungumza kwenye hoja yake ametoa taarifa ambayo haina ukweli. Lakini pia amezungumza kuhusu matakwa ya kanuni ya 63 inayozungumza kuhusu kutokusema uwongo Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge nadhani wote tumeona mjadala namna ulivyoenda kwanza Mheshimiwa Haonga alikuwa anasema wakala kuhamishiwa pale hataweza kukaguliwa na kwa hivyo Bunge halitaweza kupata taarifa yoyote kuhusu jambo hilo.

Mheshimiwa Waziri wa Fedha akasimama kumpa taarifa kwamba *vote* namba 20 inakaguliwa na yeye aksaulizwa kama anaipokea na yote yaliyofutwa baada ya hapo nadhani sote tunafahamu alijibu vipi mwanzoni na baadaye akapewa tena taarifa na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali. Baada ya mwenyekiti wa Kamati Hesabu za Serikali kumpa taarifa Mheshimiwa Haonga kwamba *vote* 20 inakaguliwa isipokuwa Bunge halijawahi

kukagua ndio maneno Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa haonga akasema anaipokea alipouliwa kwa mujibu wa kanuni zetu alisema anapokea taarifa hiyo ya Mheshimiwa Mwenyekiti wa kamati ya *PAC*. Lakini wakati huo huo akiwa anatoa maelezo yake kabla sijampa fursa ya kuzungumza Mheshimiwa Jenista akasema pia anaipokea taarifa ya Mheshimiwa Waziri kuhusu kukaguliwa kwa *vote 20*.

Mheshimiwa Jenista amesimama kuomba ufanuzi kwa sababu anaona kanuni ya 64 lakini pia kanuni ya 63 imetumika katika matumizi ya maneno ya kutokukaguliwa kwa *vote 20* na kwa hiyo, Mheshimiwa Jenista anataka tutumie kanuni ya 64 na 63 tukintaka Mheshimiwa Mbunge atumie uhuru wake uliyowekwa katika kanuni hizil mbili kufuta kauli yake kuhusu kutokukaguliwa kwa *vote* namba 20 na katika maelezo yake amesema kwamba kuhusu kukagua hiyo ni kazi ya Mkaguzi wetu wa Hesabu za Serikali na si Bunge. Kwa sababu Mbunge huletewa taarifa na CAG.

Kwa muktadha huo na kwa kuwa Mheshimiwa Haonga alishaipokea taarifa ya Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka kwamba *Vote 20* hata kama mwanzo alisema hakaguliwa sasa kwa kuwa alipokea taarifa amekiri inakaguliwa na pia akakubali maelezo ya Mheshimiwa Waziri kuhusu kukaguliwa. Sasa kuhusu mambo yanayofuata baada ya hapa yale yanayoletwa huku Bungeni *PAC* na *LAAC* inafanya kazi baada CAG kuwaleta kinachokuwa kimeshakaguliwa.

Kwa hiyo jambo lolote ambalo CAGhakulileta maana yake ye yeameona halipaswi kuletwa, kwa muktadha huo maneno aliyoyazungumza Mheshimiwa Haonga kuhusu kukaguliwa ama kutokukaguliwa kwa *Vote* namba 20 ameyanyosha hapa mwishoni kwamba anaikubali taarifa ya Mheshimiwa Waziri lakini pia Mheshimiwa Mwenyekiti wa kamati ya *PAC*. (*Makofii*)

Wakati huo huo nitamtaka sasa kwa mujibu wa kanuni zetu kuhusu hayo maelezo mengine ya taarifa kuweza kufika ama kutokufika yale sasa sio ya Bunge hili yale anatakiwa ayafute kwa sababu hayakuwa sehemu ya taarifa aliyokuwa akipewa. Nadhani utakuwa umeelewa vizuri Mheshimiwa Haonga. La kwanza la kuhusu ukaguzi ulilimaliza kwa maelezo yako ya mwisho, lakini lile la taarifa kufika hapa au kutokufika hilo ndio unatakiwa kuliondoa ili umalizie mchango wako.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kwanza nishukuru sana kwa kuweka vizuri nione kwamba umesimamia kanuni vizuri na umeenda vizuri. Niseme kwamba cha msingi ni kwamba hapa nilijaribu kuliweka sawasawa kwamba hii inakaguliwa lakini tangu nimekuwa Mbunge kwa miaka hii mingapi hii taarifa haijaletwa hapa Bungeni kuhusu *Vote* 20 nadhani haijaletwa hapa kukaguliwa. Lakini hili llingine ulivyoelekeza naona maagizo yako yachukuliwe kama yalivyo kwamba maagizo yako tumeshaweka sawasawa na ninaomba nichangie kitu kingine kwenye hilo tumeshamaliza na ninaomba unisaide muda wangu.

NAIBU SPIKA: Ngoja sasa nitakupa muda wako umalizie. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge kwa ajili ya kuliweka sawasawa hili la Mheshimiwa haonga hoja ya kwanza alishaikubali kwamba *Vote* namba 20 inakaguliwa ile sehemu ya pili kuhusu kuleta taarifa hapa au kutokuletwa taarifa huletwala na *CAG*, kama *CAG* hakuleta basi hakuona umuhimu ama hatakiwi kuleta hilo. Na yeye kwa ajili ya kupunguza matumizi ya muda amesema maelezo haya ndio ambayo yanachukuliwa. Kwa hiyo, sehemu hiyo ya mchango wake inakuwa imeondolewa Mheshimiwa Haonga malizia muda wako.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana naomba niendelee kama ambavyo umetaka niendelee. Kuhusu suala la *TBA*, mheshimiwa *TBA* wana miradi mingi ambayo wanapewa, wanamiradi mingi karibu miradi 90 wanapewa. Lakini cha ajabu *TBA* wanaopewa mradi mingi ya ujenzi, miradi mingi haikamiliki

kwa wakati. Na kama miradi haikamili kwa wakati tafsiri yake ni kwamba fedha za walipa kodi maana yake mwisho wa siku inakuwa zinatumika nyingi sana maana yake unapochelewesha mradi gharama za mradi zinaongezeka, gharama ya mradi ikiongezeka anayeingia hasara ni watanzania wanaolipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba niseme tu kwamba hata kule kwetu Mkao wa Songwe tuna ofisi ya Mkao wa Songwe zimeanza kujengwa muda mrefu sana ni kama miaka minne sasa hizo ofisi zinajengwa na *TBA* hazijawahi kukamilika na ni muda mrefu mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa atuambie ana mkakati gani wa kuwapunguzia *TBA* miradi. Kusudi hii miradi wapewa wengine na kuwe na ufanisi wa miradi wanapomrundikia mtu mmoja miradi hii miradi, miradi haiwezi kufanyika kwa ufanisi. Na wakati huohuo fedha za watanzani zitakuwa zinapotea kwa hiyo niombe Mheshimiwa Waziri utakapkuja hapa utuambie mna mikakati wa kuwapunguzia *TBA* miradi ili sasa na wengine waweze kupata miradi na mwisho wa siku iweze kufanyika kwa ufanisi na tuweze kupata ile *value for money*.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa
Mzungumzaji)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa kengere imeshagonga shukrani. Ahsante sana Mheshimiwa Edwin Sannda atafuatiwa na Mheshimiwa Hasna Mlimwa Mheshimiwa Godfrey Mgimwa ajandae.

MHE. EDWIN M. SANNDA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru kwanza kabisa nichukue fursa hii kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Jemedari makini kabisa Dkt. John Pombe Magufuli, kwa kazi nzuri sana ambayo imeendelea kuifanya na ama kwa hakika watanzania tunaona mwanga mbele kule kwamba tunaona tunaenda kuipata tanzania mpya. Na tanzania mpya kweli inawezekana chini ya Dkt. Magufuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake wote wawili ndugu yangu Mheshimiwa Kwandikwa na na mwenzangu Mheshimiwa *Engineer Nditiye* nimpongeze katibu Mkuu wa Wizara hii *architecture* mwenzangu Mwakalinga lakini pamoja na watendaji wote pamoja na wakuu wa taasisi zote zilizopo chini ya Wizara hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na pongezi zote hizo kwa kazi inayoendelea naomba nichangie mambo machache kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa nitapenda kuongelea barabara yetu ya kutoka Dodoma kwenda Babati ambayo inapita pale kwangu Kondoa Mjini ni barabara nzuri na ya viwango ambavyo havina shaka wakati mwингine unaweza kuendesha mpaka unaweka ile *cruise control* sina hakika katika nchi ya Tanzania ama na sehemu nyingine barabara nzuri kama ile unaipata wapi nawapongeza sana kwa viwango vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo karibu kidogo naunafika kondoa mjini lipo daraja moja linaitwa Msangalale. Daraja lile limekaa sehemu ambayo kama inamtego kidogo kuna mlima halafu kuna kona kunamteremko wa hatari sana kumekuwa kukisabisha ajali nyingi, watu wamekuwa, watu wengi sana wamepoteza maisha pale na wengine wamepata vilema. Sasa niliwahi kuzungumza siku moja kwenye RCC na ninamshukuru sana *Engineer* wa Mkoa wa Dodoma Eng. Leonard Chimagu alili-*react* haraka na wakafanya utaratibu wakweka alama za hatari lakini pia wakweka tuta la kupunguza *speed*.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati mbaya eneo lilipowekwa lile tuta na eneo ilipowekwa ile alama ni karibu sana na lile daraja matokeo yake bado ajali zimeendelea nakuja mtu huko na spidi yake kwa sababu barabara ipo tamu, anakuja na *speedy*yake anaona alama hii hapa ghafla tuta, na tuta lenyewe bahati mbaya pia halina ubora wa sahihi ukiligonga lile watu wanarukia mtoni. Mara kadhaa

malori yamedondoka na mara kadhaa gari ndogo zimedonga na zimesabisha kupoteza maisha kwa wapita njia pale. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sasa basi ushauri wangu ni nini, alama zisogeze nyuma na ninaomba sana Wizara ilizingatie na kulifuatilia hili, alama isogezwe nyumba na lile bampu lilekebishwe vile viwango vyake vilivywewka lisiwe la kustukiza wakati mwingine linaharibu hata gari. Halafu kabla ya bampu huwa kunakuwa wanaita kama rasta hivi zisogee nyuma kidogo takribani viwango ninyi mnavijua na ninaamini suala hili kadri nilivyolieleza mtaweza kulirekebisha kwa upande kama unatoka Dodoma na kwa upande kama unatoka Kondoaa sehemu zote mbili alama za hatari ziwekwe mbali ile kona imekaa vibaya sana hilo ni moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini jambo la pili kwa upande wa barabara nataka niongelee barabara inao younganisha Kondoaa kwenda mpaka Kateshi mmtenge bilioni 50 kwa ajili ya barabara ya Munguri Iakini hapa Kondoaa Mjini lipo daraja la mto mkondoa si daraja kuna daraja dogo ambalo sio la barabara ya *TANROADS maximum* ni tani 10 malori makubwa hayawesi kupita ili barabara ile ya *TANROADS* maroli makubwa yapite yanapita korongoni. Sasa napo pale lazima kuweka daraja kwa sababu kunganisha usafiri kati ya kondoa mpaka Kateshi lile daraja la Mto Mkondoa la lenyewe lazima lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana hilo mlingalie vinginevyo magari yatakuwa yanapita halafu yanakwamia pale kwenye Mto Mkondoa. Ukitaka kupitia hili daraja hili la tani 10 malori makubwa hayawesi kupita halafu inaingia mjini kuna kona dongo sana malori makubwa hajawesi kupita naomba sana hilo liangaliwe hilo ni jambo la kwanza. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili Jimbo la Kondoaa lipo mjini kabisa Iakini bado tunazo kata kama sita hivi suala la masiliano ni changomoto kubwa tunazungumzia Kata ya Kingare. Mheshimiwa Naibu Waziri *Engineer Nditiye* niliwha kukugusia hii na orodha nilikupa Kata kingare maeneo

ya Kampori na mengineyo tunazungumzia Kata ya Suruke, tunazungumziea Kata ya Seria maeneo ya Hurumbi na Dumu na Chandimo tunazungumzia Kata ya Koro maeneo ya Chora na Hachwi, tunazungumzia Kata ya Borisa, tunazungumzia na Kata ya Kondoja Mjini yenyewe hebu fikiria mjini kwenye kuna maeneo ya Tumbero na Chang'ombe hakuna mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili nakuomba sana Mheshimiwa Naibu Waziri hebu lifanyie kazi pale mjini tujisikie nasi tunaweza kupata huduma muhimu vinginevyo sisi tupo Makao Makuu, kweli tupo Makao Makuu halafu tunakosa mawasiliano jamani. Jiji la Dodoma Makao Makuu ya nchi hebu naomba tusaidie sana kwenye hili nilitamani sana niseme zaidi lakini naona kama dakika zangu umenipa mbili sijui... (*Makofii*)

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa
Mzungumzaji)*

NAIBU SPIKA: Muda wako umeshaisha Mheshimiwa ahsante sana. Mheshimiwa Hasna Mwilima atafutiwa na Mheshimiwa Godfrey Mgimwa Mheshimiwa Omar Kigua ajindae.

MHE. HASNA S. K. MWILIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru nianze kwa kumpongeza Waziri, pamoja na Manaibu wake Mawaziri na Watendaji wote wa Wizara hii muhimu sana katika majimbo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kuzungumzia madaraja, jimbo langu lina eneo moja korofi sana tunaita kwenye kivuko cha Malagarasi kwenye ukurasa wa 167 nimeona mmeelezea kujenga daraja la Mto Malagarasi sasa nilikuwa nataka ufanuzi Mheshimiwa Waziri atakapokuja, hapa nione je, hili daraja la Mto Malagarasi mnalenga daraja gani, Kwenye ukurasa wa 167? Ndiyo daraja la llagala kwa sababu linapita pale kwenye Mto Malagarasi au mnalenga daraja lipi? Kwa sababu nilipomwuliza Mheshimiwa Waziri aliniambia niangalie ukurasa

wa 340. Ukurasa wa 340 mnazungumzia kujenga daraja kwenye Mto Rwegere. Mto Rwegere upo kwenye Kijiji cha Mgambazi, unakwenda mpaka kwenye Kijiji cha Rukoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naona hapa kuna *contradiction* ambayo ningependa Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri mliangalie vizuri, kama mtakuwa mnalenga llagala, basi nadhani ni hili daraja la Mto Malagarasi. Kwa hiyo, naomba kwa faida ya wananchi wa ukanda huo, basi Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha ataweza kunifafanulia vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili nizungumzie suala la gati. Tunazo gati mbili kubwa zinazojengwa; gati ya Sibwesa na gati ya Mgambo. Naomba tu gati ile ya Sibwesa sasa ikamilike kwa sababu imekuwa ni muda mrefu sana. Gati ile mara kwenye kitabu mmendika ukamilishaji asilimia 91. Bajeti ya mwaka 2018 mlisema ukamilishaji asilimia 90. Sasa kila mwaka mnapokuja hapa mnaongeza asilimia fulani ya ukamilishaji. Naomba mnisaide kukamilisha bandari ile. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nizungumzie suala la *SGR*. Nimeangalia kwenye ukurasa wa 212, ule mtandao wa *SGR* mnazungumzia tu Dar es Salaam mpaka Tabora, Tabora – Isaka, Isaka – Mwanza. Tumekuwa tunalia hapa Bungeni mbona hamwoneshi ule mtandao wa kutoka Tabora mpaka Kigoma? Hata kama itachukua miaka mitatu, miaka minne kukamilika lakini tunaomba kwa sababu mpango unatambua huu mtandao wa kwenda Tabora, basi tunaomba Mheshimiwa Waziri aweze kuzingatia kuonyesha na ule mtandao wa kutoka Tabora kwenda Kigoma. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie barabara ukurasa wa 164. Ninayo barabara yangu ya Uvinza mpaka Malagarasi kilometra 51.1 na kilometra 36 kutoka Chagu mpaka Kazilangwa. Ninajua kwamba kwenye Mfuko ule wa Maendeleo ya Abudhabi Mheshimiwa Waziri wa Fedha alishatia saini kupokea pesa takribani miaka miwili iliyopita. Sasa ninachoomba ni utekelezaji. Ni lini Serikali

itatangaza tenda kwa ajili ya Mkandarasi kuanza ujenzi wa barabara hiyo ya kutoka Uvinza - Malagarasi na hicho kipande cha Chagu mpaka Kazilambwa? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, tunayo hii barabara yetu hii ya kutoka Simbo mpaka Kalya ina kilometra 250. Kila mwaka mnaitengea fedha shilingi bilioni 1.9, shilingi bilioni 1.8 lakini tusipoteze hizi fedha za Serikali, tunatenga pesa nyingi kwa ajili ya kujenga barabara kiwango cha udongo na changarawe, sasa kwa nini tusiende kwenye kiwango cha lami? Hii barabara tangu mmeanza kujenga ni takribani miaka zaidi ya 20. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri aangalie namna ya kupandisha hadhi barabara hii iweze basi kujengwa kwa kiwango cha lami. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie bandari ya Kigoma. Asubuhi nilimsikia Mheshimiwa Zitto anaongelea bandari. Bandari hii ni kwa faida ya Wabunge wote na wananchi wote ndani ya Mkoa wa Kigoma. Leo ninavyoongea, tunao Mkutano mkubwa pale Kigoma ambaa ulikuwa Mheshimiwa Makamu wa Rais awe Mgeni Rasmi, lakini amemtuma Mheshimiwa Kandege kumwakilisha. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna wafanyabiashara kutoka Zambia, tuna wafanyabiashara kutoka Burundi, tuna wafanyabiashara kutoka Congo na Rwanda; wameanzia jana, wako kwenye mkutano mkubwa wa wafanyabiashara wanaozunguka Ziwa Tanganyika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naiomba Serikali waone umuhimu wa bandari ya Kigoma. Bandari hii ina umuhimu sana. Tunafanya biashara na watu wa Zambia, Congo na Burundi, wanachukua mizigo yao Dar es Salaam wanaipeleka Congo, Zambia na Burundi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa bandari hii, kwa sababu Benki ya Afrika iko tayari kutusaidia fedha, tunaomba

Serikali iangalie kwa jicho la huruma ili basi bandari hii na italingizia fedha Serikali, ni chanzo cha mapato, yaani...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hasna muda wako umekwisha.

MHE. HASNA S.K. MWILIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Godfrey Mgimwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Omari Kigua na Mheshimiwa Seif Gulamali ajiandae.

MHE. GODFREY W. MGIMWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nitambue kazi nzuri ambayo anafanya *Engineer Mfugale*, kazi nzuri anayofanya *Engineer Kindole* wa pale Iringa na Ma-engineer wote wa *TANROADS* Tanzania nzima ninawapongeza sana kwa kazi nzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya yote namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Manaibu wake wawili wote kwa kazi nzuri ambazo wanaendelea kufanya. Juu ya yote, namshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri na kubwa ambayo anaendelea kufanya kwa ajili ya mabadiliko ya nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza kwa kuzungumzia suala la Uwanja wa Ndege wa Nduli. Uwanja huu upo Mkoani Iringa. Naipongeza sana Serikali kwamba kipindi hiki cha bajeti ya 2019/2020, tumetengewa jumla ya zaidi ya shilingi bilioni tisa kwa ajili ya ujenzi na uboreshaji wa uwanja huu wa ndege. Uwanja huu wa ndege, kwa kweli ukifika sasa hivi pale Iringa ni burudani tupu. Tunajiandaa kwa ajili ya upanuzi na kuelekea sasa kwenye utalii katika upande wa Nyanda

za Juu Kusini. Kwa hiyo, tumejipanga na tunaishukuru Serikali kwamba kazi inaonekana na tunaendelea kuipongeza Serikali kwa ajili ya kazi nzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumza pia juu ya takwimu ambazo zimetolewa na Kamati ambayo inahusu masuala ya *SUMATRA* na ajali kwa ujumla. Ni jambo la kusikitisha sana kwamba unaona ajali kwa kipindi hiki cha mwaka 2018/2019 bajeti iliyopita, unakuta inasema makosa ya kibinadamu kwenye ajali ilikuwa asilimia 76. Ubovu wa magari asilimia 16, miundombinu na mazingira ni 8%. Sasa mimi nataka nijikite kwa 8%. Tuna barabara mbalimbali ambazo zinajengwa na zimeendelea kuboreshwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumza barabara inayotoka Dodoma kuelekea Iringa ambayo imekamilika miaka minne iliyopita. Barabara hii ukilangalia katika kipindi kifupi imeharibika na haitamaniki tena. Sasa unajuliza, ni kwa nini tunawatafuta Wakandarasi ambao sio waaminifu? Barabara ile ukipita sasa hivi ina makorongo, ina mashimo na ndiyo inayosababisha ajali kubwa katika maeneo mbalimbali hasa katika njia hii kutoka Dodoma kuelekea Iringa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda pia kuishauri Serikali kwamba tunapotafuta Wakandarasi, basi tutafute Wakandarasi wenyewe viwango na tuwaadabishe Wakandarasi wote ambao wanafanya kazi bila kujali maslahi ya Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisemi kwamba kuwe na Wakandarasi wa nje au wa ndani, lakini ninachokisema ni kwamba Wakandarasi waweze kutazamwa kwa namna ya tofauti, kwa sababu fedha nydingi zinatumika lakini matokeo yanakuwa ni mabovu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumza pia suala moja kubwa sana ambalo lipo katika Mkoa wangu wa Iringa kwa barabara ambayo inatoka Iringa Mjini kuelekea *Ruaha*

National Park, ambayo hata juzi niliongea. Barabara hii ni ya muhimu sana; na umuhimu wake ni kule kwenye mbuga za wanyama za *Ruaha National Park*. Mbuga hii ya *Ruaha National Park*, ndiyo mbuga kubwa katika nchi yetu ya Tanzania. Vilevile katika ukanda wa Afrika Mashariki ni mbuga yenye maslahi makubwa sana, ni mbuga ambayo ingetuingizia fedha nyngi. (*Makofí*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitakwimu Ngorongoro kwa mwaka inaingiza watalii 400,000, Serengeti 150,000, Mikumi 70,000, *Ruaha National Park* ambayo ndiyo mbuga kubwa ina watalii 35,000. Sasa sioni kama kuna sababu ya kuendelea kutojengwa barabara hii ya *Ruaha National Park*, kutoka Iringa kwenda *Ruaha National Park* ambayo ni kilometra 104. Tumetengewa shilingi milioni 650 tu. Hili jambo lina umuhimu, litatuingizia kipato kikubwa nchi yetu ya Tanzania kama tutakuwa makini kuiangalia kwa namna nyngine. (*Makofí*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nikumbushe kwamba kuna maeneo mbalimbali katika Jimbo langu la Kalenga ambayo hayana mawasiliano ya kutosha. Kijiji cha Lyamzungwe, Kijiji cha Kihanga, Kijiji cha Magunga, Sadani, Kikombwe, Makota, Ulata, Mwambao, Ikungwe, Kidilo, Kaining'ombe, Makombe, Malagosi, Kihanzi na Lyasa. (*Makofí*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana Wizara iweze kutazama kwa jicho la kipekee tuweze kupata mawasiliano ya simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba niseme yafuatayo. Naomba ninukuu Biblia Takatifu, Luka 11:9 inasema hivi, "Nami nawaambieni ombeni nanyi mtapewa."

MBUNGE FULANI: Kweli.

MHE. GODFREY W. MGIMWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nimeomba. Inasema, "tafuteni nanyi mtaona," nimetafuta; sasa naamini nitapata. "Bisheni nanyi mtafunguliwa," nimebisha naamini Mheshimiwa Waziri utafungua milango.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho mstari wa 10 inasema: "kwa kuwa kila aombaye hupokea, naye atafutaye huona, naye abishaye atafunguliwa," jamani naombeni mnifungulie. Mstari wa 11 unasema: "maana ni yupi kwenu aliye baba ambaye mwanaye akimwomba mkate atampa jiwe au samaki? Badala ya samaki atampa nyoka? Au akiomba yai, atampa ng'e." (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeomba barabara inayotoka Iringa Mjini kuelekea *Ruaha National Park*. Haya yote naomba yaweze kunukuliwa na Mheshimiwa Waziri muweze kuyafanya kazi, Iringa tuweze kupata barabara ya *Ruaha National Park*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, Mungu awabariki, tuko pamoja sana. Ahsanteni sana. (*Kicheko/Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Omari Kigua, atafuatiwa na Mheshimiwa Seif Gulamali na Mheshimiwa Hussein Amar ajiandae.

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya jioni ya leo nami niweze kusema machache juu ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Manaibu Waziri wote wawili kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuchangia nataka nitoe somo dogo tu, dhana ya uwekezaji katika miradi mikubwa. Serikali imedhamiria kujenga *SGR*. Huu ni mradi mkubwa sana. Sasa wapo waliozungumza kwamba wanatarajia mafanikio ya muda mfupi. Huu ni mradi mkubwa sana ambao *return* yake itapatikana baada ya miaka 50 ijayo. *Ku-recoup costs* zake au *payback period* ni zaidi ya miaka 20. Kwa hiyo, usitarajie kwamba faida utaipata kwa

muda mfupi, lakini lazima tuangalie *multiplier effect* ya mradi huu. Huwezi ukajenga *SGR* kwa sababu ya kubeba abiria peke yake, hapana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Tanzania tunapakana na nchi ambazo hazina bahari; Uganda, Burundi na Rwanda. Tunatarajia *SGR* ndiyo ambayo itakayoweza kupeleka mizigo huko. Kwa hiyo, lazima tutarajie mafaniko makubwa sana kutokana na mradi huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna mtu amesema hapa kwamba suala la mradi huu halina kitu kinaitwa *local context*, siyo kweli hata kidogo. Naomba nitibitishe kwamba *SGR* ina mafanikio makubwa sana. Nitataja machache tu eneo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *SGR* itakapokamillika, tunatarajia viwanda vyetu vya *cement* vya ndani vitaweza kuzalisha takribani mifuko milioni 110.2. Vilevile tunatarajia viwanda vyetu vya ndani, vitaweza kuzalisha nondo tani 115,000. Kama hiyo haitoshi, viwanda vya kokoto vitatoa mita milioni 2.7. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni suala la ajira. Ajira mpaka sasa hivi, kutokana na *SGR* ni takribani watu 9,639 wamepata ajira. Hii ni dhana ya *local context* kwenye *SGR*. Kwa hiyo, mtu asipotoshe kusema kwamba *SGR* katika suala la *local context* haijazingatiwa. Siyo kweli hata kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, sasa naomba nizungumzie suala lingine la *ATCL*. Umuhimu ni mkubwa sana sana. Narudia kusema kwamba faida ya *ATCL* au katika mambo ya ndege huwezi ukaiona moja kwa moja na wala usitegemee kwamba *ATCL* irekodi *profit* katika muda mfupi. Hata Mashirika yale kwa mfano, *Rwanda Airlines*, *Ethiopian Airlines*, hawajawahi kurekodi *profit* hata siku moja, lakini kuna suala la *multiplier effect*, hili lazima lizingatiwe na umuhimu wa jambo hili ni mkubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo sasa naomba nirudi kwenye barabara ambayo inaunganisha Mikoa minne. Barabara hii ni muhimu sana, nayo ni barabara ambayo ipo katika llani ya Chama cha Mapinduzi. Barabara hii ina kilometa 460 ya kuanzia Handeni, Kibirashi, Kibaya na Singida. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika,...

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa. Taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kigua kuna taarifa. Mheshimiwa Msigwa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, mzungumzaji anasema ujenzi wa *SGR return* yake tutaipata baada ya miaka 50. Sasa nataka nimpe taarifa, mimi nimepitia kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri hapa sijaona hayo anayoyasema, sijui ameyatoa wapi? Anaweza akatupa *reference?* Kwa sababu analipa tahiruki Taifa.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, haijasomwa. Hayajaandikwa humu.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Msigwa, zungumza na mimi, si umeshamaliza. Zungumza na mimi. Usizungumze na...

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mchana huu! Bangi ya Iringa hiyo.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninachosema, naomba unilinde basi.

MBUNGE FULANI: Wakemee wale.

MBUNGE FULANI: Wakemee wale.

MBUNGE FULANI: Wakemee hawa huku.

MBUNGE FULANI: Kwani anaye...

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tusiwashe *microphone*.

MBUNGE FULANI: Msukuma.

NAIBU SPIKA: Kwa sababu amepewa nafasi ya kuzungumza Mheshimiwa Msigwa, tafadhalii. Mheshimiwa Msigwa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nilichokuwa nasema Waziri ametupa kitabu na ndiyo tunakijadili. Mchangiaji anasema *return* ya *SGR* tutaipata baada ya miaka 50. Sasa nilikuwa nataka nimpe taarifa kwenye kitabu cha Waziri hatuna, hizi *data* anazitoa wapi? Ili tusiwape taharuki wananchi kwa kitu ambacho anakitoa hewani.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane. Mheshimiwa Msigwa anauliza swali, lakini kwa sababu alisimama kwa ajili ya taarifa, hulazimiki kujibu swali lake, wala hutakiwi kujibu swali lake, lakini je, unaipokea taarifa aliyoitoa?

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Naibu Spika, siipokei kwa sababu hili ni suala la kitaalamu zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unapofanya *investment...*

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Naibu Spika, unapofanya *investment* maana yake, *return* yake hutarajji kupata kwa muda mfupi na maana yake *SGR* hii faida yake itakuwa kwetu sisi na vizazi vijavyo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kigua kuna taarifa nyingine. Waheshimiwa Wabunge, muda wetu pia ni mfupi, nadhani wote tunaangalia saa pale na wachangiaji bado niko nao hapa kwenye orodha. Kwa hiyo, tutaenda vizuri tu wote kwa pamoja. Mheshimiwa Ally Saleh.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Msemaji anayezunguma sasa hivi alisema kwamba hata *Ethiopian Airlines* hawatengenezi faida. Nataka nimwambie kwamba mwaka 2017 faida yao imetoka kwenye Dola milioni 233, imepanda mpaka Dola milioni 229 asiseme kwamba haipati faida.

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Naibu Spika, siikubali taarifa yake kwa sababau hajasema chanzo cha taarifa hii ni wapi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kigua unaipokea taarifa hiyo?

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Naibu Spika, siipokei kwa sababu hajataja *source* ya taarifa ni wapi.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

WABUNGE FULANI: Endelea.

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee.

MHE. ALLY SALEH ALLY: *Reuters, Reuters Financial.*
(Kicheko)

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie barabara hii ambayo nimesema ni barabara ya Handeni – Kiberashi - Kibaya na Singida. Barabara hii ni muhimu sana. Kama katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri alivyosema kwamba barabara hii ndiyo ambapo bomba la mafuta litapita, nami nataka niseme kwamba pamoja na kwamba bomba la mafuta kutoka Uganda kwenda Tanga litapita katika eneo hili, pia barabara hii ina umuhimu mwininge ambapo watu wa mikoa hii minne nilioitaja wanahitaji barabara hii sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri ametenga kiasi cha shilingi 1,450,000,000/=, namshukuru sana na ninampongeza katika hilo. Namwomba Mheshimiwa Waziri, barabara hii ni muhimu sana, sana, sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba Serikali ya Tanzania imetenga kiasi hicho nilichokitaja, lakini naomba tuangalie namna ambavyo inaweza kujengwa kwa kiwango cha lami, kwa sababu eneo hili ambalo barabara hii inapita, ina uzalishaji mkubwa sana, sana, sana; na ukizingatia kwamba kuna matarajio ya kutengeneza Bandari ya Tanga, kwa hiyo, ni matumaini yangu kwamba barabara hii ikitengenezwa kwa kiwango cha lami, basi mizigo yote ambayo inatoka Tanga kwenda Magharibi huko itapita katika barabara hii. Nina imani kwamba Mheshimiwa Waziri atazingatia katika hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine naomba nizungumzie huku minara. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwamba Wilaya ya Kilindi ni mionganoni mwa maeneo ambayo yamepata minara mingi sana, lakini lipo eneo moja ambalo linapakana na Wilaya ya Simanjiro, Kata ya Saunye, hajapata minara. Naomba sana Mheshimiwa Waziri kuititia Mfuko huu wa Mawasiliano wahakikishe kwamba Kata hiyo inapata mawasiliano kwa sababu ni eneo muhimu sana, ni

eneo ambalo lina mbuga ya utalii, lakini maeneo haya hayasikiki kabisa. Ni matumaini yangu kwamba Serikali itasikia tuweze kupata mawasiliano katika eneo hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema maneno hayo machache, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Seif Gulamali atafutiwa na Mheshimiwa Hussein Amar na Mheshimiwa Dua William Nkurua ajiandae.

MHE. SEIF K. S. GULAMALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika Wizara hii ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nipende kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli, kwa kuamua kuleta mabadiliko katika nchi yetu. Nchi yetu ilikuwa na changamoto na maamuzi makubwa na maamuzi sasa yanafanyika, pongezi kubwa sana ziende kwake, hasa ununuzi wa ndege, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais; ujenzi wa viwanja vya ndege, kazi kubwa zinafanyika, sisi wote ni mashahidi katika maeneo yetu; ujenzi wa madaraja na barabara kubwa zinazojengwa ndani ya nchi yetu. Haya yote ni maamuzi ambayo Mheshimiwa Rais ameamua binafsi na wananchi wa Jimbo la Manonga tunampongeza na kumuunga mkono Mheshimiwa Rais na tunasema aendelee kuchapa kazi, sisi tuko tayari kumuunga mkono mchana na usiku. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niwapongeze watendaji wakuu, Mkurugenzi Mkuu wa *TANROADS*, Mheshimiwa *Engineer Mfugale*; lakini pia nimpongeze mwalimu wangu aliyenifundisha chuoni, Mkurugenzi Mkuu wa *SUMATRA*, Mheshimiwa *Mr. Ngewe*, pongezi ziende kwake. Amefanya kazi nzuri sana na nimeona juzi kapata hati ya utumishi bora, kwa hiyo nitumie nafasi hii kumpongeza mwalimu wangu kwa kazi nzuri anazozifanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nimpongeze Mkurugenzi Mkuu wa Viwanja vya Ndege, Mheshimiwa Dkt. Hamza Johari, Mwalimu wangu, naye anafanya kazi nzuri, hawa wote Walimu wangu wanafanya kazi nzuri sana, nafurahia, naona jinsi gani wanavyo-perform katika maeneo yao, bila kumsahau Mkuu wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji, naye nampongeza kwa siku ya leo. Nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kumteua tena kwa mara nydingine aendelee kuhudumu kwa nafasi hiyo ya ukuu wa chuo. Natambua alikokitoa chuo, hali ilivyokuwa na ilivyo sasa hivi ni chuo tofauti sana, pongezi nydingi sana ziende kwako Dkt. Mganiwa, kwa kazi kubwa unazozifanya, tunakupongeza, sisi wanafunzi wako tuko Bungeni tunaona matunda unayoyafanya huko ulipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, niwapongeze Mawaziri; Mheshimiwa *Engineer* Nditiye pamoja na Mheshimiwa Kwandikwa bila kumsahahu Waziri wake, Mheshimiwa *Engineer* Kamwelwe; Mheshimiwa Waziri anafanya kazi nzuri sana, pongezi nydingi sana ziende kwake maana yake leo nilisema niwapongeze kwa kazi wanazozifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nisisahau kumkumbusha Mheshimiwa *Engineer* Kamwelwe, Waziri kwamba wananchi wake wa Mpanda kule wanapokuwa wanatoka huwa wanapewa rufaa kwenda kutibiwa Tabora, wakienda Tabora na kwenyewe wanapewa tena rufaa ya kwenda kutibiwa pale Hospitali ya Nkinga lakini wakifika pale Ziba kwenda Nkinga barabara ni mbaya sana. Naomba Mheshimiwa Waziri aweke lami pale ili wagonjwa wanaotoka Mpanda, Katavi, Majimoto wapate huduma safi pale Nkinga ili kuwarahisishia wananchi wake wapite kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, naomba nimkumbushe Mheshimiwa *Engineer* Kamwelwe kwamba aanze basi na usanifu; barabara ya Ziba- Nkinga – Puge; barabara ya Ziba – Choma na kwa kutambua kwa sababu Choma Chankola kuna kiwanda kikubwa cha pamba. Kwa hiyo kwa sababu tuna kiwanda lazima miundombinu

tuiboreshe na Serikali hii tunanadi ni awamu ya viwanda. Kwa hiyo namwomba sana Mheshimiwa Waziri katika bajeti yake sijaona akitenga angalau usanifu na barabara hii ya Ziba – Choma, Ziba – Nkinga – Puge ni barabara inayomilikiwa na TANROADS, nimwombe Mheshimiwa Waziri aikumbuke barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, Mheshimiwa Waziri,
Engineer Nditiye ile minara...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa
Mzungumzaji)*

NAIBU SPIKA: Muda wako umekwisha Mheshimiwa, kengele ya pili imeshagonga.

MHE. SEIF K. S. GULAMALI: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Wizara hii, lakini minara Mheshimiwa *Engineer Nditiye* pale...

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa.

Mheshimiwa Hussein Amar, atafuatiwa na Mheshimiwa Dua William Nkurua na Mheshimiwa Daniel Mtuka ajiandae.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako hili Tukufu. Pia napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii pamoja na Naibu Mawaziri na watendaji wote kwa kazi nzuri ambazo wanazifanya katika Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo moja ambalo natakiwa nianze kulisema, leo ni mwaka wa nane niko Bungeni, kulikuwa na ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne, aliahidi ujenzi wa barabara ya lami kutoka Kahama – Bukwimba – Nyijundu – Busisi Sengerema na Rais wa Awamu ya Tano naye pia ameahidi. Hata hivyo, cha ajabu kwenye

kitabu hiki nimejaribua kuanzia ukurasa wa kwanza mpaka wa mwisho sijaona upembuzi yakinifu wa barabara hiyo. Kwa hiyo naomba njue, ahadi za Marais hawa zimepuuzwa ama zitatekelezwa na kama zitatekelezwa ni lini? Kwa sababu barabara hii ina umuhimu sana, inaunganisha mikoa mitatu; inaunganisha Mikoa ya Shinyanga, Geita na Mwanza. Barabara hii ikifunguliwa uchumi wa Nyang'hwale utapanda. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri aingize angalau basi niweze kuona kwamba upembuzi yakinifu umeanza tuwe na matumaini, leo miaka nane nazungumzia barabara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, nimejaribu kuangalia kwenye kitabu chake, ameweza kunitengea karibu milioni 900 kwa ajili ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha changarawe kutoka Nyankumbu hadi Nyang'hwale, lakini kutoka Nyang'olongo mpaka Nyang'hwale. Barabara hii ina kiwango cha changarawe lakini imepangiwa kujengwa kwa kiwango cha lami kutoka Geita- Nyankumbu kuja Nyang'hwale. Cha ajabu, miaka nane imepita, lakini tumejengewa kilometra tano tu za lami na imesimama. Miaka miwili iliyopita hatukuweza kutengewa, je, 2019/2020 kwa nini tena haikutengewa ama imeondolewa kwenye utekelezaji? Naomba Mheshimiwa Waziri aiangalie barabara hiyo kwa sababu ilishaahidiwa kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kuna barabara ambayo ameiweka, barabara hii kwa kweli ikifunguliwa itakuwa imefungua maendeleo makubwa sana katika Wilaya ya Nyang'hwale. Ameweza kututengea pesa kufungua barabara ya wilaya kwa wilaya kutoka Mbogwe kuja Nyang'hwale; kutoka Bwelwa – Bukoli – Nyijundu mpaka Bumanda na Makao Makuu Kharumwa, Makao Makuu ya Nyang'hwale, barabara hiyo ikifunguka naamini mambo yatakuwa mazuri. Nimpongeze sana kwa hilo, naomba tu utekelezaji ufanyike kwa haraka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Waziri anayehusika na masuala ya mawasiliano, kuna kata kama

tano kwangu zina matatizo ya mawasiliano. Kata hizo zikiwa ni Shabaka, Nyamtukuza, Nundu, Nyabulanda na Nyugwa, mawasiliano slo mazuri, Mheshimiwa Waziri alitupa fomu tukajaza maeneo ambayo hayana mawasiliano mazuri, nami nilijaza ile fomu mwaka jana, lakini cha ajabu mpaka leo fomu hii haijafanyiwa kazi na wananchi wangu wanapata tatizo kubwa sana la mawasiliano. Namwomba Mheshimiwa Waziri atekeleze ahadi zake, aliahidi kwamba atashughulikia maeneo yote ambayo yana matatizo ya simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza hayo machache, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dua William Nkurua atafuatiwa na Mheshimiwa Daniel Mtuka na Mheshimiwa Charles Mwijage ajiandae.

MHE. WILLIAM D. NKURUA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Natoa pongezi kwa Serikali na Wizara kwa kazi nzuri wanazozifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu muda si rafiki, nakwenda moja kwa moja kwenye Jimbo langu la Nanyumbu. Hapa naanza na watu wa ujenzi; napenda niwakumbushe kwamba Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, alitoa ahadi ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami toka Nangomba mpaka Nanyumbu. Barabara hii ni barabara inayoelekea nchi jirani ya Msumbiji, ni barabara muhimu sana kwa uchumi wa Tanzania. Kwa hiyo naomba Serikali katika vipaumbele vyake iiweke barabara ya kutoka Nagomba hadi Nanyumbu kwa sababu wananchi wana imani sana na ahadi ile na ukizingatia kwamba viongozi hawa wanakuwa wakweli. Kwa hiyo, naomba Serikali iiweke katika mpango wake ujenzi wa barabara kutoka Nangomba hadi Nanyumbu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Sekta ya Mawasiliano, naupongeza sana Mfuko kwa kazi kubwa inayofanya na kwenye Wilaya yangu ya Nanyumbu nataka

niwape maeneo muhimu ambayo kwenye bajeti hii tuyazingatie. Kwanza kabisa nataka Kata yangu ya Napacho; kata hii ina shida kubwa ya mawasiliano, hasa kwenye Vijiji vya Mpombe, Ndekela, Mburusa, Napacho, Kazamoyo na Chimika, hawa watu mawasiliano ni magumu sana, naomba eneo hili tutafute eneo tuweke mnara, tukiweka mnara mmoja katika eneo hili tutahakikisha kwamba wananchi watapata mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Kata ya Likokona; kata hii pia haina mawasiliano, hata makao makuu ya kata mawasiliano ni magumu sana. Kwa hiyo naomba tutafute namna ya kuhakikisha kwamba Likokona na Vijiji vyake vya Msinyasi, Namaka na vitongoji vyake vipate mawasiliano ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naongeza Kata ya Mkonona; kata hii ina Kijiji cha Mbangara Mbuyuni na Kitongoji chake cha Wanika, mawasiliano hayapatikani kabisa. Kwa hiyo naomba Serikali itupatiwe mnara kwenye kata hii ili wananchi wa kata hii nao wapate mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la mwisho kwa mawasiliano ni Kata ya Maratani katika Wilaya ya Nanyumbu. Kata hii pia ina Vijiji vya Maratani, Malema na Mchangani B, havina mawasiliano kabisa. Naomba tupatiwe mnara katika maeneo hayo kutokana na viwango vyao vya kutambua wapi tuweke mnara ili vijiji hivi nilivoyovitaja vipate mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri; minara hii itakayojengwa ijengwe kwa viwango ambavyo tutapeleka mawasiliano kama ilivyokusudiwa kwa sababu kuna baadhi ya vijiji minara imejengwa lakini haifanyi kazi ilivyokusudiwa. Kwa mfano, ukienda kwenye Kata ya Sengenya, Kijiji cha Sengenya, kuna mnara pale lakini mnara ule hata pale kijijini haufanyi kazi vizuri. Kwa hiyo naomba Serikali tunapoweka hii minara tuhakikishe kwamba inafanya kazi tuliyokusudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Kata ya Mkonona, Kijiji cha Marumba, kuna mnara wa *TTCL* pale, lakini mnara

ule haufiki hata kilometa tano, Vitongoji vyake vya Namaromba *network* haipatikani kule. Kwa hiyo naomba tutakapokwenda kupeleka minara hii, vijjji hivi na vitongoji vyake viweze kupata *network* na wananchi wetu waweze kupata mawasiliano kama tulivyokusudia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu muda si rafiki, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Daniel Mtuka atafuatiwa na Mheshimiwa Thimotheo Mzava na Mheshimiwa Pauline Gekul ajiandae.

MHE. DANIEL E. MTUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi hii ili nami angalau kwa dakika chache hizi nitoe mchango wangu katika Wizara hii ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Kwanza nilpongeze Rais wangu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, anachapa kazi. Ukiitazama nchi hii ya Tanzania ni kubwa, lakini ninavyozungumza kila mahali naona barabara zinajengwa; madaraja, *flyovers* zinajengwa; na mabwawa, visima, naona vinajengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hospitali, vituo vya afya, zahanati naona zinajengwa; ukienda Kinyerezi Bonde la Mto Ruvu kule mitambo ya umeme inajengwa; *REA* nguzo naona zinatambaa kila mahali, kila kona ya nchi hii zinachimbiwa na umeme unakwenda; Viwanja vya ndege vinakarabatiwa, vingine vinajengwa vipyta; lakini kuna ujenzi wa meli, vivuko, magati kwenye maziwa, bahari pamoja na mito yanajengwa; lakini kuna ujenzi wa reli ya kisasa unaendelea; vyumba vya madarasa vinajengwa; matundu ya vyoo yanajengwa; ukarabati wa shule kongwe unaendelea; ujenzi wa vituo vya *VETA* unaendelea; ujenzi wa viwanda mbalimbali unaendelea; lakini bajeti ya dawa imepanda, kutoka bilioni 31 mpaka 270; lakini elimu bure pia shule ya msingi mpaka *Form Four*.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile amedhibiti matumzii ya fedha; kwa hiyo anapodhibiti matumizi ya fedha maana

yake ni kwamba ameokoa fedha nyingi. Kwa mfano amedhibiti sana rushwa, amedhibiti wafanyakazi hewa, kwa hiyo pesa ile imeongezeka inakwenda kwenye kazi; naona kasi ya Mheshimiwa Rais ni kubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizi niwapongeze pia Waziri na Naibu Mawaziri pamoja na timu nzima ya Wizara. Nilet maombi machache kabla sijapigiwa kengele; kule Jimboni kwangu Manyoni kuna kituo kikubwa sana kile cha kat i cha ukaguzi wa mizigo ya magari makubwa, pale Mhalala. Naona kwenye ukurasa wa 256 wametenga bilioni nne sawa, lakini ule ujenzi umesimama tangu Septemba, mwaka jana, naomba ile kasi iongezeke, tunataka kile kituo kikamilike.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuhusu Daraja la Sanza; nimeona kuna millioni 60 imetengwa hapa. Upembizi yakinifu umeshafanyika, lakini imebakia tu ile *process* ya ujenzi ianze na mwaka huu tulitegemea kwamba fedha zile ziwekwe ujenzi uanze, lakini sioni fedha yoyote hapa, milioni 60 si kitu, yaani ni kama hakuna. Watutenge fedha watuongezee kwenye lile daraja, lile daraja ni muhimu kwa sababu ile barabara inayotoka kule Manyoni kwenda Sanza na kuvuka lile daraja kwenda Dodoma ni ya kiuchumi kwa Wilaya ya Manyoni kwa sababu lile eneo lote ndilo linalozalisha chakula kwa Mkoa wa Singida na Mkoa wa Dodoma sehemu pia wanapata. Kwa hiyo hilo daraja ni la msingi na la muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimeangalia barabara yetu ya Rungwa – Mkiwa; wenzetu kule wa Chunya tayari wameshapewa hela Chunya – Makongorosi, lakini Mbalizi – Makongorosi pia wameshapewa fedha nimeziona hapa, lakini sijaona Mkiwa kwenda Noranga, hakuna fedha pale, sijui kwa nini na ilikuwa tupewe fedha hizi tangu mwaka jana, hakuna fedha, hatuzioni. Kwa nini sisi hawajatenga ile fedha wanawatengea wenzetu wa upande ule? Nadhani utaratibu ulikuwa wakandarasi wakutane katikati, lakini wanatenga upande mmoja, watenge na huku basi ili wakutane katikati.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, minara ya simu; nimekuwa nikuliza mara nydingi sana, kuna Kata yangu moja inaitwa Makuru, hasa Kijiji kimoja kinaitwa Hika, kule tunahitaji minara. Njia ile ya kutoka Manyoni kwenda Sanza, mule njiani ukisafiri hakuna minara, kwa hiyo mawasiliano yanakatika, naomba sana Wizara hii iniangalie. Nimeshauiliza mara nydingi sana hapa Bungeni, wameshajibu kwamba wataleta minara, lakini nimetazama sioni fedha yoyote iliyotengwa, naomba sana sehemu hii ya minara na mawasiliano ili tuweze kuwasiliana kwa sababu mawasiliano ni maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo machache, nashukuru sana, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni yetu ya 28(5), naongeza nusu saa ambayo haitakwisha, wachangiaji bado watatu, ili tukamilishe kazi za siku ya leo kwa sababu mambo yalikuwa mengi kidogo.

Nilikuwa nimeshamwita Mheshimiwa Timotheo Mnzava, atafuatiwa na Mheshimiwa Pauline Gekul, Mheshimiwa Janeth Masaburi atamalizia.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini pia nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake, wanafanya kazi nzuri, lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nitumie nafasi hii kuzungumza mambo machache; kule Korogwe tuna barabara inaitwa Korogwe – Dindira – Bumbuli – Soni, ni barabara ya kilometra 77. Kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010 ambayo ninayo mkononi hapa, kwenye ukurasa wa 48 kulikuwa na ahadi ya kufanya usanifu kwenye barabara hii. Kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015, kwenye ukurasa wa 58 kuna ahadi ya chama chetu kwenda kutengeneza barabara hii kwa kiwango cha lami. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipoingia kwenye Bunge liliopita, kwa maana ya Mkutano wa Kumi na Nne, niliuliza swalii, Mheshimiwa Waziri akaniambia wametenga shilingi milioni 130 kwa mwaka huu wa fedha unaoisha Juni kwa ajili ya usanifu, lakini mpaka sasa hivi hela zile hazijafika, na usanifu umeshafanyika kwenye kilometa 20 za kutoka Soni kwenda Bumbuli, bado kipande cha kutoka Bumbuli – Dindira – Korogwe na ahadi hii imekuwa ni ya muda mrefu kwa watu wa Korogwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepitia kitabu cha Mheshimiwa Waziri, nimeona kwenye ukurasa wa 181 kuna hela, bilioni sita, wametenga kwa ajili ya barabara pale, wamesema kuanza matengenezo ya lami. Hata hivyo, nilipokwenda ndani zaidi kwenye kitabu, kwenye ukurasa wa 275 wametenga shilingi milioni 770 kwa ajili ya ukarabati, lakini wameweka kwenye ukurasa wa 317 wametenga shilingi milioni 140 kwa ajili ya usanifu. Kwa ukubwa wa kilometa zilizobakia, shilingi milioni 140 haiwezi kutosha kukamilisha shughuli ya usanifu kwenye barabara ile, hata ile 130 ambayo bado haijafika ikija haiwezi kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua kwamba matengenezo ya barabara hii ni muhimu, lakini kwa kuwa watu wa Korogwe wamekuwa na kiu ya barabara hii kwa muda mrefu na ni ahadi ya chama chetu; ni ahadi ya viongozi wa Serikali akiwemo Mheshimiwa Rais, akiwemo Mheshimiwa Waziri Mkuu, nimwombe Mheshimiwa Waziri, kama hatuna mahali pengine pa kupata fedha ya kukamilisha usanifu ili tuanje kujandaa kwenda kujenga, basi hizi 770 tupeleke kwenye usanifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu tumefanya matengeneo na nimpongeze Meneja wa *TANROADS*, Mkoa wa Tanga, *Enineer Ndumbaro*, anafanya kazi nzuri sana, sisi Wabunge wa Mkoa wa Tanga tunaisifia kazi yake, anafanya kazi nzuri sana. Mwaka huu tumefanya matengenezo, sehemu iliyobakia ni maeneo machache yaliyobaki, nina hakika hizi milioni 140 na zile milioni 60 nyingine wametenga zinaweza kutosha kumaliza hii kazi. Hebu hizi milioni 770

tupeleke kwenye usanifu ili kazi ya usanifu ikamilike, halafu tuendelee na kutafuta hela kwa ajili ya kutengeneza barabara kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara ya *Old Korogwe* kwenda mpaka Magoma ambayo inakwenda kuunganisha mpaka na wenzetu wa Mkinga, ni barabara muhimu, lakini haijawahi kufikiriwa kuwekwa kwenye kiwango cha lami. Tunaomba sana Serikali iikumbuke hii barabara. Pia nawakumbusha watu *TANROADS* wameweka alama za X kwenye nyumba za watu na kuna wengine wamekaa miaka mingi kama watu wa pale maeneo ya Kerenge Kibaoni waende wakapewe elimu juu ya hatma ya makazi yao pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipongeze sana Shirika la Reli kwa kazi kubwa ya kufufua hii reli, reli ya kutoka Tanga kwenda mpaka Moshi na sehemu ya Tanga- Same imeshakamilika. Ninachoomba tu, *SGR* wakati ukifika watukumbuke, lakini kwa sasa hivi yale maeneo ambayo kuna makazi ya muda mrefu, watuwekee vivuko ili wananchi waweze kuvuka kutoka upande mmoja wa reli kwenda upande mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Nditiye na kaka yangu *Engineer Ulanga* wamefanya kazi kubwa kule Kizara tulikuwa na shida ya mawasiliano, lakini bado yako maeneo nimeyapeleka kwao maeno ya Lewa, Lutindi, Makumba na Kata ya Mkalamo, tunaomba watupelekee huduma ya mawasiliano kwa ajili ya watu wetu pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda sio rafiki sana. Kuna jambo limezungumzwa hapa na kiti chako kimeshalisemea. Tunazungumza yapo malalamiko kwamba kwa nini Wakala wa Ndege amehamishwa kwenda kwenye Ofisi ya Mheshimiwa Rais? Lazima tukumbuke nchi yetu inaongozwa kwa mujibu wa sheria za nchi yetu aliyepewa dhamana ya kuongoza Taifa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hawa walio chini yake wanamsaidia na hata ukiosoma *Presidential Affairs* inaeleza, hakuna dhambi kwa Rais

kuamua kazi ipi ya Serikali isimamiwe chini ya Wizara ipi au ofisi ipi siyo dhambi. Ni vibaya kusema kwamba Rais amefanya makosa au ana nia ovu, sheria inamruhusu, hakuna sheria inayovunjwa ni utaratibu wa kawaida. (*Makofii*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umekwisha. Mheshimiwa Pauline Gekul tutamaliza na Mheshimiwa Janeth Masaburi

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niseme machache katika Wizara hii kwanza niwapongeze Mheshimiwa Waziri na timu yako kwa jinsi ambavyo wanaipeleka Wizara hii iweze kusonga mbele. Pia niwape hongera sana hasa kwa kazi wanayofanya kwa ATCL wamekuwa na vituo tisa katika nchi lakini vitano katika kanda hongereni sana. Vile vile wamekuwa na *destinations* tano nje ya Nchi za Rwanda, Burundi, Zimbabwe, Zambia, Comoro, lakini mna matarajio ya *destinations* katika nchi tano Thailand, India, Afrika Kusini na China na haya wanayatekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze pia kwa sababu sasa wana mpango wa kuongeza ndege mbili tena *dreamliner* na *bombardier* tena ambazo zitaingia mapema mwakani hongereni sana. Pia wanafanya kazi kubwa ya kuwafundisha Marubani wetu 51, Wahudumu 66, Wahandisi 14, lakini abiria wameongeza kutoka 200,000 mpaka 300,000, hongereni sana. Naomba wasikate tama, hii kazi ni kubwa na wameitambulisha nchi yetu katika nchi zingine, jambo ambalo lilikuwa halijawahi kufanyika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, nimekuwa nikiongea kuhusu *bypass* ya Babati kutoka Arusha kuja Dodoma na Singida, sasa nimeona bilioni ambazo ametutengea kwa ajili ya fidia ya wale wananchi wa Babati, Mruki, Hangoni, Sigino na hii *bypass* inakwenda kutekelezwa, jambo ambalo lilikuwa halijawahi

kufanyika hongereni sana na tunashukuru. Pia niwaombe kuhusu suala zima la uwanja wa ndege katika Mkoa wetu wa Manyara. Mheshimiwa Waziri Mkoa wa Manyara hatuna uwanja wa ndege, tumesema sana muda mrefu sana tunaomba watuwekee hata kwa changarawe, sio lazima lami kwa sasa, naomba hili walichukue kwa sababu mengi tumekuwa tukiyasema na wamekuwa wakiyachukua, naamini na hili pia watalichukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri suala la malipo ya fidia kwa wale ambaao mita za barabara zimeongezeka sasa, nimekuwa nikisema kwamba tunahitaji kuwafidia wale ambaao nyumba zao sasa zimeathirika na zile *reserve*. Ni vizuri wakaliangalia hili kwa sababu neema tulioipata ya Babati kuunganishwa na barabara Singida-Arusha-Dodoma pia imezaa hili linguine, naamini watalifanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu watu wa *TBA* wako nao siku ya leo niwaombe pia maeneo ya *National Housing* yamekabidhiwa kwa *TBA* pale mjini, Mheshimiwa Waziri nilishamjulisha hili tunahitaji eneo la pale mjini kwa ajili ya matumizi ya halmashauri sasa na kuwapanga vijana wetu wale Wamachinga ambaao wanahitaji kutumia eneo hilo naamini na hili watatupatia pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ufupi pia barabara yetu ile inayoanzia Singe nishukuru wameiweka na inaendelea na ujenzi kila mwaka kwenda Kiteto, ni vizuri sasa wakatuongezea fedha kwa sababu itatupunguzia kilomita zaidi ya 78 kuja Dodoma. Sasa kwa sababu hii imekamilika ya Kondoaa-Babati naamini hii ya Singe, Sukulo na maeneo mengine inaweza ikaturahisishia sana watu wa Babati kuelekea Dar es Salaam, hii barabara wakiikamilsha kwa kiwango cha lami jambo linaendelea sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niwaombe barabara ya Dareda-Dongobeshi kuelekea Hospitali ya Rufaa ya Hydom wamekuwa wakiweka, nashukuru pia wameweke hata mwaka huu, lakini sasa ni vizuri tukafikiria kuunganisha

na hii inayotoka Karatu kuelekea Mbulu na Singida kwa kiwango cha lami. Nishukuru hiyo ya Karatu - Mbulu, Hydom - Singida mmeshai-cover lakini sasa hii ya Babati - Dareda - Dongobeshi - Hydom Mheshimiwa Waziri wakiweka pia itatusaidia sana. *Otherwise wanafanya kazi nzuri hongereni na niwapongeze wamepokea zaidi ya asilimia 60 ya bajeti, nipongeze Wizara ya Fedha na Wizara yao na wanachapa kazi.* Pia niwapongeze kwa kuwa wazalendo wameona kwamba wawe na bajeti ambayo inatekelezeka zaidi ya triliioni mbili mpaka 1.5

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na ahsante. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimemwita Mheshimiwa Janeth Masaburi atachangia siku ya Jumatatu.

Ninayo matangazo mawili moja ni tangazo la wageni walioingia jioni hii, tunao wageni 111 wa Mheshimiwa Selemani Jafo ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais,TAMISEMI ambaao ni wanafunzi 100 na Wahadhiri 11 kutoka Dar es Salaam *Institute of Technology (DIT)* wakiongozwa na Dkt. Anthony Tomsa. (*Makof*)

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Venance Mwamoto ambaao ni wawekezaji toka nchini Japan Ndugu Satoshi Sakamoto na Ndugu Kunihiro Fujushima, karibuni sana. (*Makof*)

Tunao pia wageni 47 wa Mheshimiwa Venance Mwamoto ambaao ni wanakwaya wa Amkeni kutoka Ilula, Mkoani Iringa wakiongozwa na Mchungaji Philip Kikoti, karibuni sana. (*Makof*)

Ninalo pia tangazo kutoka kwa kocha wa Bunge *Sport Club* anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa kesho kutakuwa na mechi kati ya Bunge na Polisi Jamhuri wote mnakaribishwa, hajasema muda lakini mechi huwa zinaanza

saa kumi, kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa huko.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kifupi mwongozo ambao nilikuwa nimeombwa asubuhi utaingia kwenye Taarifa Rasmi za Bunge lakini kwa kifupi ni kwamba swalililokuwa limeulizwa na Mheshimiwa Mohamed Khatibu ambalo aliliombea mwongozo kuhusu majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Naibu Waziri alikuwa sawasawa kwa sababu kanuni ya 44(1) inataka maswali ya nyongeza yatokane na swalilambsingi. Kwa hiyo Mheshimiwa Mohamed Khatibu anashauriwa kwa mwongozo wangu huu wa leo kuleta hilo kama swalilambsingi ili ajibiwe kuhusu maendeleo ambayo Serikali imechukua katika mkataba huo unaohusu wengine kunyanyaswa ama wengine kuumizwa wakiwa polisi. Kwa hiyo mwongozo wangu ni huo na utaingia kwenye Taarifa Rasmi za Bunge kama ulivyo.

**MWONGOZO WA SPIKA ULIOOMBWA NA
MHESHIMIWA MOHAMED JUMA KHATIB (MB)
KUHUSU KUTOJIBIWA KWA UKAMILIFU SWALI LAKE LA
NYONGEZA LILILOTOKANA NA SWALI LA MSINGI
NAMBA. 205 KAMA ILIVYOWASILISHWA BUNGENI**

Waheshimiwa Wabunge, leo asubuhi tarehe 10 Mei, 2019 katika Kikao cha Ishirini na Tano, Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge la Bajeti, baada ya kipindi cha Maswali na Majibu kumalizika, **Mheshimiwa Mohammed Juma Khatib, (Mb)** aliomba Mwongozo wa Spika chini ya Kanuni ya 68(7) na 46 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Mhe. Mohammed Khatib (Mb) aliomba Mwongozo huo kutokana na kutoridhishwa na majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Swalilambsingi Namba 205.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mohammed Juma Khatib (Mb) alieleza kuwa alipouliza maswali mawili ya

nyongeza, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi alijibu swali moja tu na kuliacha swali la pili. Vile vile alieleza kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri katika majibu yake alidai kuwa aliyajibu maswali yote mawili kwa pamoja. Aidha, alieleza zaidi kuwa katika swali lake la pili la nyongeza alitaka kujua kwamba pamoja na Katiba yetu kukataza askari polisi kuwatesa watuhumiwa, kuna Mkataba wa Kimataifa unaokataza utesaji (*International Convention Against Torture*), hivyo alitaka kujua ni kwa nini mpaka leo Serikali haijauridhia?

Waheshimiwa Wabunge, nilitoa majibu kuwa nitapitia Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*) ili niweze kufahamu kama maswali mawili ya nyongeza yaliyoulizwa na Mhe. Khatibu (Mb) yaliyibiwa kwa ukamilifu. Vilevile niliwakumbusha kuhusu masharti ya Kanuni yanayosimamia uulizaji wa maswali ya nyongeza kwamba Mbunge anayeuliza maswali hayo hutakiwa aulize kutaka kupata ufanuzi kwenye majibu yaliyotolewa kwenye Swali la Msingi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuititia Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*), Swali la Msingi Namba 205 liliulizwa kwamba ni katika mazingira gani askari polisi anapaswa au hulazimika kumtesa mtuhumiwa wa makosa mbalimbali wakati akiwa mikononi mwake au kwenye kituo cha polisi?

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi alijibu swali hilo kuwa kifungu cha 11 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20 hakimruhusu askari kumpiga au kumtesa mtuhumiwa wa makosa mbalimbali wakati akiwa mikononi mwa polisi au kwenye kituo cha polisi. Aliongeza kuwa, Kanuni za Kudumu za Utendaji wa Jeshi la Polisi (PGO) zinakataza na kuelekeza utendaji mzuri wa askari polisi, ambapo askari yeoyote atakapobainika kufanya vitendo vya kumpiga au kumtesa mtuhumiwa huchukuliwa hatua za kinidhamu ikiwepo kufukuzwa kazi na au kufikishwa mahakamani.

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyofafanua awali, Kanuni ya 44 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti

kuhusu maswali ya nyongeza. Kanuni hiyo inasema kama ifuatavyo (nanukuu):-

"Maswali ya nyongeza yanaweza kuulizwa na Mbunge ye yote kwa madhumuni ya kupata ufanuzi zaidi juu ya jambo lolote lillotajwa katika jibu lillotolewa"

Waheshimiwa Wabunge, swali la nyongeza ambalo Mheshimiwa Mbunge aliuliza kuhusu uridhiaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Kukataza Utesaji (*International Convention Against Torture*) ni swali jipya ambalo kimsingi halikulenga kutaka kupata ufanuzi wa majibu yaliyotolewa katika swali la msingi kwa mujibu wa Kanuni niliyoitaja. Hivyo, swali hilo la nyongeza lillikiuka masharti ya Kanuni ya 44(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, kwa maelezo hayo na kwa mujibu wa Kanuni ya 44(1), Mheshimiwa Mohammed Juma Khatib (Mb) kama anataka kupata majibu ya Serikali kuhusu uridhiaji wa Mkataba wa Kimataifa kuhusu Kuzuia Utesaji, anapawa kuleta Swali la Msingi ili aweze kupata majibu ya Serikali.

Waheshimiwa Wabunge, huo ndio Mwongozo wangu.

Umetolewa leo tarehe 10 Mei, 2019.

Mhe. Dkt. Tulia Ackson, (Mb)

NAIBU SPIKA

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo naahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya Jumatatu saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.08 Jioni Bunge lilihairishwa hadi Siku ya Jumatatu,
Tarehe 13 Mei, 2019, Saa Tatu Asubuhi)*